WIZARA YA MAMBO YA NDANI

# MWONGOZO KWA ASASI ZA KIRAIA KATIKA KUTEKELEZA SHERIA YA KUPAMBANA NA USAFIRISHAJI HARAMU WA BINADAMU

## (NA.6 YA MWAKA 2008)

TANZANIA

2015

IOM - OIM

United Nations
TANZANIA
Delivering as One

Chapisho hili limewezeshwa na Mpango wa Umoja wa Mataifa wa Msaada wa Maendeleo Tanzania (UNDAP 2011-2016) chini ya kikundi kazi cha ulinzi wa jamii kikishirikiana na shirika la kimataifa linashughulikia masuala ya wahamaji (IOM)

# YALIYOMO


Shukrani ........................................................................................................................................................ iv

Utangulizi ........................................................................................................................................................ v

Kikundi cha wadau wa asasi za kiraia za kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu…………..…vi

Tafsiri ya maneno yaliyotumika ........................................................................................................ vii

**SURA YA KWANZA........................................................................................................................1**

Asasi za kiraia na utekelezaji wa sheria ya kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu Tanzania (Na.6 ya mwaka 2008) ............................................................................................... 1

1.1 Historia ya mwongozo ........................................................................................................ 1

1.2 Madhumuni ya mwongozo ................................................................................................... 1

1.3 Muundo wa mwongozo na kuwasilisha yaliyomo ................................................................. 1

**SURA YA PILI ................................................................................................................................2**

MBINU ZA MAFUNZO ............................................................................................................... 2

2.1 Utangulizi ............................................................................................................................ 2

2.2 Changamoto za utofauti. ...................................................................................................... 2

2.2.1 Kanuni za ufundishaji watu wazima .................................................................................. 2

2.2.2 Uwezeshaji wa mafunzo ................................................................................................... 3

**SURA YA TATU...............................................................................................................................6**

UELEWA WA USAFIRISHAJI HARAMU WA BINADAMU ........................................................... 6

3.1 Utangulizi wa sura................................................................................................................ 6

3.2 Maana ya usafirishaji haramu wa binadamu ....................................................................... 7

3.3 Usafirishaji haramu wa binadamu: mtazamo wa dunia ........................................................ 9

3.3.1 Taarifa na takwimu katika ngazi za kimataifa .................................................................... 9

3.3.2 Itifaki ya Umoja wa Mataifa ya Kuzuia, Kupambana na Kuadhibu Usafirishaji Haramu wa Binadamu, hasa kwa Wanawake na Watoto (‘Itifaki ya Palermo’)............................................. 11

3.3.3 Taarifa/ripoti ya marekani ya usafirishaji haramu wa binadamu ........................................ 13

3.4 Usafirishaji haramu wa binadamu Tanzania ....................................................................... 13

3.4.1 Maelezo kutoka katika taarifa ya usafirishaji haramu wa binadamu ya mwaka 2013-Tanzania ........................................................................................................................... 13

3.4.2 Sheria ya Kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu................................................ 14

3.5 Usaili na uhamasishaji......................................................................................................... 16

3.5.1 Mbinu za udhibiti (rejea sehemu ya pili, kifungu cha 4 cha Sheria) ..................................... 16

3.5.2 Aina za unyonyaji:.............................................................................................................. 18

3.5.3 Aina nyingine za unyonyaji................................................................................................. 19

3.6 Usafirishaji haramu wa binadamu dhidi ya magendo ya binadamu........................................ 20

3.7. Watoto kama kundi maalum................................................................................................ 26

3.7.1 Maelezo ya usafirishaji haramu wa watoto ......................................................................... 26

3.7.2 Kazi za watoto, ajira za watoto na usafirishaji haramu wa watoto ..... 26
3.7.3 Usafirishaji haramu wa watoto (aina za unyonyaji wa watoto) ..... 26

**SURA YA 4 ..... 28**
UTAMBUZI WA WAATHIRIKA ..... 28
4.1 Utangulizi wa sura ..... 28
4.2 Umuhimu wa utambuzi wa waathirika ..... 29
4.3 Kanuni elekezi katika kuwahudumia waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu ..... 30
4.4 Mambo maalum ya kuzingatia ..... 31
4.5 Utambuzi wa waathirika ..... 33
4.5.1 Maelezo ya viashiria vya awali ..... 34
4.5.2 Uthibitisho wa viashiria ..... 35
4.5.3 Maswali maalumu ya utambuzi ..... 36
4.5.4 Mwongozo wa mahojiano ..... 39
4.6 Usalama na usiri wa taarifa ..... 41

**SURA YA 5 ..... 42**
MSAADA WA MOJA KWA MOJA KWA WAATHIRIKA ..... 42
5.1 Utangulizi wa Sura ..... 42
5.2 Kutathmini Hatari ..... 43
5.2.1 Maswala ya usalama na tathmini ya hatari ..... 49
5.3 Msaada wa moja kwa moja kwa waathirika ..... 52
5.3.1. Huduma za msaada kwa waathirika kuwarejesha katika jamii zao ..... 52
5.3.2 Msaada kwa waathirika chini ya vifungu vya sheria ..... 55

**SURA YA 6 ..... 57**
USHIRIKIANO NA VYOMBO VYA KUTEKELEZA SHERIA: TASWIRA ..... 57
6.1 Utangulizi ..... 57
6.2 Ushirikiano katika taswira ya mashirika yanayotoa huduma ..... 58
6.3 Hatari zinazoweza kujitokeza kutokana na mikakati ya mashirika yanayotoa huduma ..... 59
6.4 Hatari zinazoweza kujitokeza kutokana na utendaji kwa mashirika yanayotoa huduma ..... 59
6.5 Ushirikiano na vitengo vya kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu. ..... 60
6.6 Ushirikiano wa kitaalamu na kujenga uwezo. ..... 60
6.7 Mambo ya muhimu kutambua ..... 60
6.8 Njia mbili za mchakato wa mabadilishano ..... 61
6.9 Utoaji wa taarifa za kiintelijensia moja kwa moja kwa polisi na muathirika ..... 61
6.9.1 Kutathmini hatari zinazotokana na kutoa taarifa maalum za kiintelijensia. ..... 62
6.10 Kutoa taarifa chini ya vipengele vya sheria ..... 63

**MAREJEO** ........ **64**
*ARTICLES* ........ 64
*BOOKS* ........ 64
*HANDBOOKS/ TOOLKITS* ........ 64
*CASE STUDIES* ........ 65
*WORKING PAPER* ........ 65
*REPORTS* ........ 65
*LOCAL STATUTES* ........ 65
*INTERNATIONAL INSTRUMENTS* ........ 65
*INTERNET SOURCES* ........ 66

**KIAMBATANISHO I** ........ **67**
**ITIFAKI YA PALERMO** ........ 67
**Protocol to Prevent, Suppress and Punish Trafficking in Persons Especially Women and Children, supplementing the United Nations Convention against Transnational Organized Crime** ........ 67

**KIAMBATANISHO II** ........ **73**
ORODHA YA UTAMBUZI KWA MUATHIRIKA ........ 73

# SHUKRANI

Mwongozo huu umeandaliwa ili kuzisaidia asasi za kiraia na wadau wengine wanaofanya kazi katika masuala ya kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu. Ni sehemu ya mpango mkubwa wa kutekeleza sheria ya kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu (Na. 6 ya mwaka 2008) nchini Tanzania.

Kwa niaba ya serikali ya jamhuri ya muungano wa Tanzania, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa shirika la kimataifa linaloshughulikia masuala ya wahamaji (IOM) wakishirikiana na wajumbe wa Sekretariati ya kamati ya kitaifa ya kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu kwa kutoa maelekezo katika mchakato wa kupitisha Mwongozo. Utengenezaji wa Mwongozo huu umezingatia Mwongozo wa Zambia kwa asasi za kiraia (ambao ulitengenezwa kwa msaada wa ofisi ya kutathmini na kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu, Idara ya Serikali ya Marekani-US JTIP) kama ulivyowasilishwa na wawakilishi wa ujumbe wa IOM Zambia, pamoja na kupatiwa msaada wa kitaalamu na kuhariri kutoka kwa mtaalamu wa kikanda wa ofisi ya IOM ya kanda ya mashariki na kusini mwa Afrika.

Zaidi ya hayo, napenda kutambua mchango wa kikundi cha asasi za kiraia cha kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu ambacho kimetoa mapendekezo ya msingi katika Mwongozo huu na kuujaribisha ili kuona jinsi utakavyotekelezeka.

Serikali ya Tanzania inalishukuru shirika la kimataifa la linaloshughulikia masuala ya wahamaji likishirikiana na mpango wa maendeleo wa msaada kwa pamoja wa umoja wa mataifa (UNDAP 2011-2015) chini ya kikundi kazi cha ulinzi wa jamii kwa kutoa mchango wake wa kifedha na kitaalam katika Mwongozo huu.



**Mbarak M. Abdulwakil**

Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Ndani

# UTANGULIZI

Usafirishaji haramu wa binadamu ni janga la kutisha la kisasa katika uhamaji wa kimataifa na linaendelea kusababisha uvunjifu wa haki za binadamu wa hali ya juu kwa wale ambao hujikuta ni waathirika. Chakusikitisha ni kwamba, pamoja na kuwa Itifaki ya umoja wa mataifa ya kuzuia, kupambana na kutoa adhabu ya usafirishaji haramu wa binadamu, hasa wanawake na watoto ina zaidi ya muongo mmoja, inasemekana kwa sasa watu wengi wanaishi katika mazingira ya kitumwa zaidi kuliko kipindi chochote katika historia yetu. Idadi ya kesi zilizoandikishwa katika miaka ya karibuni inaonesha kwamba Tanzania pia imedhurika na madhara ya usafirishaji haramu wa binadamu ndani na nje ya mipaka ya nchi, hasa kwa wanawake na watoto kwa ajili unyonyaji katika maeneo ya kazi na unyonyaji kingono.

Katika kukabiliana na tatizo hili, serikali, asasi za kiraia na mashirika ya kimataifa yamechukua hatua mbalimbali yakisaidiana na mpango wa pamoja wa msaada wa maendeleo Tanzania (UNDAP 2011-2015), ubalozi wa marekani na umoja wa ulaya. Hatua hizi zilizidi kukua mwaka 2011 baada ya kuanzishwa kwa kamati ya kitaifa ya kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu na kutengenezwa kwa mpango kazi wa kitaifa wa kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu ambao shughuli zake zinalenga, pamoja na mengineyo, kukuza uelewa kwa serikali, watekeleza sheria, wananchi kwa ujumla, na kwa kiasi fulani wanahabari. Hata hivyo, inafahamika kwamba jitihada hazijafanyika katika kukuza uelewa kwa asasi za kiraia na kuwahusisha katika utekelezaji wa sheria ya kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu. Upambanaji wa aina zote za usafirishaji haramu wa binadamu unahitaji ushirikiano kati ya serikali, vyombo vya kutekeleza sheria, mashirika ya kimataifa na asasi za kiraia.

Ushirikiano huu unaanza na uelewa wa pamoja kuhusu tatizo na njia za pamoja katika kulitatua. Kwa hiyo, ni muhimu kwa wadau wote kuwa na ufahamu na zana za kutatulia tatizo hili. Ni matumaini yangu kuwa mwongozo huu utazisaidia asasi za kiraia katika jukumu lao la kutekeleza sheria ya kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu na mwisho kufanikisha lengo la kitaifa la kutokomeza usafirishaji haramu wa binadamu Tanzania.



**Hon. Mathias M. Chikawe**

Waziri wa Mambo ya Ndani

## KIKUNDI CHA WADAU WA ASASI ZA KIRAIA ZA KUPAMBANA NA USAFIRISHAJI HARAMU WA BINADAMU

**Serikali inapenda kuyashukuru mashirika yafuatayo kwa mchango wao mkubwa katika kutengeneza mwongozo huu wa asasi za kiraia:**

African Network for Prevention and Protection against Child Abuse and Neglect (ANPPCAN)

Asylum Access Tanzania

Conservation of Hotels, Domestic Social Services and Consultancy Workers Union (CHODAWU)

C – Sema

Child in the Sun (CIS)

Dogodogo Centre Street Children Trust

Daughters of Mary Immaculate (DMI)

Friends of Don Bosco-Watoto Wetu Tanzania

House of Peace

Kiota Women Health and Development (KIWOHEDE)

Legal and Human Rights Centre (LHRC)

Mbagala Girls Home-Salvation Army

Tanganyika Law Society (TLS)

Tanzania Child Rights Forum

Tanzania Women Lawyers Association (TAWLA)

Women Legal Aid Centre (WLAC)

World Vision Tanzania

Msimbazi Centre

National Organization for Legal Assistance (NOLA)

Plan International Tanzania

Save the Children International

Faraja Trust Fund

Faraja Young Women Development Organization (FAYOWODO)

Catholic Diocese of Zanzibar

Zanzibar Legal Service Centre

Lindi Non-Governmental Organizations Network

Tanzania Network for Marginalized People

Children's Dignity Forum

Family Health International

Kivulini Women's Rights Organization

Adilisha Child, Youth Development and Family Preservation

Tanzania Domestic Workers Coalition

Mango Tree Orphan Support Trust

Care of the Needy

Major Alliance Education Centre

Rafiki Social Development Organization

Centre for Widows and Children Assistance

Orphans Relief Services Tanzania

Mkombozi Centre for Street Children

# TAFSIRI YA MANENO YALIYOTUMIKA

**Afisa kazi mkaguzi:** Afisa kazi mkaguzi aliyechaguliwa chini ya sheria ya kazi.

**Afisa uhamiaji:** Anahusisha afisa uhamiaji mkuu na maafisa uhamiaji wengine wote.

**Afisa ustawi wa jamii:** Afisa ustawi wa jamii kutoka wizarani anayehusika na maswala ya ustawi wa jamii.

**Afisa wa polisi:** Mtu ambaye ni mwanachama wa jeshi la polisi.

**Afisa wa umma:** Mtumishi wa umma.

**Ajira ya mtoto:** Kumuingiza mtoto katika utumwa na mazingira yanayofanana na utumwa; kumsafirisha mtoto ili kumnyonya kwa kumfanya mtoto afanye kazi mbali na nyumbani na mbali na malezi ya familia yake; kumlazimisha mtoto afanye kazi ili deni liweze kulipwa au namna nyingine ya kufanya kazi ambapo mtoto huwekwa rehani; au kumlazimisha mtoto kufanya kazi au kutumia silaha, au katika migogoro; au kuwa mali ya mtu ambaye anamiliki shamba na analazimishwa kufanya kazi katika shamba hilo;

**Daktari/Tabibu:** Mtu aliyefuzu kufanya kazi kama daktari na ambaye amesajiliwa na baraza la madaktari la Tanzania.

**Itifaki:** Itifaki ya umoja wa mataifa ya kuzuia, kupambana na kuadhibu usafirishaji haramu wa binadamu, hasa wanawake na watoto. Itifaki hii inaongezea mkataba wa umoja wa mataifa wa uhalifu wa kupangwa ambao unasimamiwa na ofisi ya umoja wa mataifa inayoshughulikia maswala ya madawa ya kulevya na uhalifu.

**Kamati:** Kamati ya kitaifa ya kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu Tanzania, iliyoundwa kuratibu shughuli za taasisi mbalimbali zinazofanya kazi kuhusiana na masuala ya kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu, pamoja na kushauri mipango ya kitaifa ya kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu na kushughulikia masuala mengine yanayohusu usafirishaji haramu wa binadamu.

**Kituo kwa ajili ya ulinzi wa waathirika:** Ni sehemu ambayo waathirika wanaweza kupata malazi ya muda. Rejea kifungu cha 20 cha sheria ya kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu kuhusu mazingira ambayo malazi yanaweza kuhitajika.

**Kufanyishwa kazi kinguvu:** Mtu hufanyishwa kazi kinyume na matakwa yake, ama kwa sababu ya vitisho, matumizi ya nguvu au kuwekwa kizuizini.

**Kuwekwa rehani:** Mtu anayelazimishwa kufanya kazi kwa sababu huduma zake zimeahidiwa kama amana kwa ajili ya deni. Huduma zinaweza kuahidiwa na mtu anayefanya kazi au mtu mwingine. Maana hii pia inatumika pale ambapo deni ni kubwa sana; au thamani ya huduma katika tathmini halisi haitumiki kulipa deni au deni linalosemekana; au pale ambapo urefu na aina ya kazi hazijaelezewa au kuwekewa mipaka.

**Magendo ya binadamu:** Ni kitendo cha kumsadia mtu ambaye si raia au mkazi wa kudumu kuingia nchi nyingine bila kufuata taratibu za sheria za nchi husika kwa lengo la kujinufaisha kifedha au faida nyingine.

**Majengo:** Majengo au majengo mengine yanayohamishika au makazi. Miundo iliyozungukwa na maji pia inajumuishwa.

**Matendo ya kufanana na utumwa :** kuwekwa rehani, utumwa, mfumo wa kulazimishwa ndoa baada ya kuwalipa wazazi au walezi, kurithi wajane, kumpatia mtoto mtu mwingine kunakofanywa na wazazi au walezi ili mtoto huyo akanyonywe.

**Matumizi mabaya ya nafasi kutokana na mazingira magumu ya mtu:** Inahusu hali yoyote ambapo mhusika hana njia nyingine mbadala au inayokubalika bali kukubaliana na unyonyaji. Hii ni kukubali kwamba waathirika wengi wako katika mazingira hatarishi; kwa mfano mtu mwenye nafasi ya madaraka, au mzazi au mwenza. Mtu aliye katika mazingira hatarishi anaweza kuwa mtu yeyote ambaye yupo ndani ya nchi kinyume na sheria au bila kuwa na nyaraka sahihi; mtu ambaye hawezi kufanya baadhi ya vitu kwa sababu ya ulemavu; mjamzito; mtu aliyeathiriwa na madawa ya kulevya; au mtu ambaye hawezi kutoa maamuzi kwa sababu ni mtoto.

**Matumizi ya nguvu:** Vurugu zinazotumia au zisizotumia nguvu ambazo husumbua akili ya mtu na kumfanya aamini kuwa kama hatafanya kazi au kutoa huduma, yeye au mtu mwingine wa karibu yake atapata madhara makubwa. Hii inaweza kuwa kwa namna ya vitisho vya kupata madhara au vitisho vya kutumia vibaya mchakato wa kisheria.

**Mfuko:** Mfuko wa kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu, ulioundwa chini ya sheria ya kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu, kwa ajili ya kuwasaidia waathirika pamoja na kuwarejesha katika hali zao za awali na kuwaunganisha na jamii zao kwa kuzingatia maslahi yao ya msingi.

**Mkurugenzi wa mashitaka:** Huchaguliwa chini ya katiba ya Tanzania.

**Mlezi:** Mtu ambaye anahusika na malezi ya mtoto kwa kipindi fulani.

**Mtoto:** Mtu mwenye umri chini ya miaka kumi na nane

**Mtu:** mtu wa asili au shirika

**Muathirika:** Mtu ambaye amenyonywa na haki zake za msingi zimevunjwa na ameathirika kisaikolojia au kimwili kutokana na kusafirishwa kiharamu.

**Mzazi:** Mzazi wa kibaiolojia, mzazi wa kuasili au mlezi.

**Unyonyaji kingono:** kumlazimisha mtu kujiingiza kwenye ukahaba au matendo mengine ya ngono kwa nguvu, vitisho na njia nyingine zisizo za hiari.

**Unyonyaji:** Matendo kama vile utumwa na matendo yanayofanana na utumwa, kuwekwa rehani, au ndoa za kulazimishwa, unyonyaji kingono, utumwa, kufanyishwa kazi kinguvu, utumikishwaji wa watoto na kutolewa viungo vya mwili.

**Usafirishaji haramu wa binadamu:** ni usaili, usafirishaji, uhamishaji, uhifadhi au upokeaji watu, kwa njia ya vitisho au matumizi ya nguvu au aina nyingine ya matumizi ya nguvu, utekaji nyara, udanganyifu na matumizi mabaya ya madaraka au cheo, mazingira magumu au kutoa au kupokea malipo au faida ili kupata ridhaa ya mtu na udhibiti, kwa lengo la unyonyaji.

**Utumishi wa umma:** Utumishi wa umma.

**Utumwa:** Kumlazimisha mtu kufanya kazi au kutoa huduma kwa njia zozote, kwa sababu anaamini kwamba asipofanya hivyo, basi yeye au mtu mwingine atapata madhara makubwa.

**Utumwa:** kuwa na umiliki wa mtu ili mtu huyo achukuliwe kama bidhaa/mali.

**Wakili:** Mtu aliyefuzu kufanya kazi kama wakili Tanzania ambaye ana cheti cha kufanya kazi za kisheria au ameajiriwa na serikali.

# SURA YA KWANZA

## Asasi za kiraia na utekelezaji wa sheria ya kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu Tanzania (Na.6 ya mwaka 2008)

### 1.1 Historia ya mwongozo

Usafirishaji haramu wa binadamu ni uhalifu wa kimataifa unaovuka mipaka ya nchi na mamlaka mbalimbali. Unaweza pia kutokea ndani ya mipaka ya nchi. Kosa hili linatambulika kama mkusanyiko wa makosa mbalimbali na uvunjifu wa haki kwa pamoja na siyo kitendo kimoja; mchakato wa jinai na si tukio la jinai. Utatuzi wa usafirishaji haramu wa binadamu unahitaji ushirikiano wa hali ya juu miongoni mwa asasi za kiraia na vyombo vya kutekeleza sheria katika ngazi ya kitaifa. Pamoja na kwamba mazingira ya maeneo mbalimbali yanatofautiana, baadhi ya changamoto ambazo asasi za kiraia hukumbana nazo katika kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu ambao mara nyingi hujulikana kama utumwa wa kisasa hufanana dunia nzima. Kwa mfano, kesi za usafirishaji haramu wa binadamu mara nyingi huwa hazitolewi taarifa kwa sababu jamii kwa ujumla ina uelewa mdogo kuhusu usafirishaji haramu wa binadamu na pia mara nyingi waathirika huogopa kutoa taarifa kwa kuwaogopa wanaowasafirisha. Kwa kuwa kosa hili hufanyika kwa usiri sana, huwa ni vigumu kuwatambua wasafirishaji haramu wa binadamu na vivyo hivyo kupata hukumu dhidi yao. Ushirikiano kwa ajili ya kutoa huduma madhubuti kwa waathirika na njia za kuzuia ili wasisafirishwe vinatakiwa kuwa ni sehemu ya mkakati katika kukabiliana na changamoto hizi.

Usafirishaji haramu wa binadamu ni janga la kitaifa linalotiliwa mkazo, hasa kutokana na kuongezeka kwa kesi hizi miaka hii ya karibuni. Juhudi za kitaifa za kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu zinahakikisha kwamba wadau muhimu wana uwezo wa kupambana na janga hili. Tangu mwaka 2007 mafunzo yamekuwa ni msingi wa mkakati wa kuzuia usafirishaji haramu wa binadamu. Hata hivyo, mpaka leo mafunzo yamekuwa yakiandaliwa na kulenga maafisa wa kutekeleza sheria. Asasi za kiraia hazijatiliwa mkazo pamoja na kuwa zimekuwa zikisaidia katika utambuzi, kutoa msaada na kuwarejesha waathirika katika hali zao za awali pamoja na kushiriki katika jitihada za kuzuia usafirishaji haramu wa binadamu. Mipango ya msingi ya mafunzo itasaidia washiriki kupata ujuzi mpya na ufahamu wa muhimu katika kufanya kazi zao. Mafunzo pia yanatoa nafasi kwa ajili ya uratibu, kukuza mitandao na ushirikiano baina ya wadau wa kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu.

### 1.2 Madhumuni ya Mwongozo

Mwongozo huu umeandaliwa ili kuzipatia asasi za kiraia nyenzo rejea na kutumika kama msaada wa kufundishia na kuwasaidia kuelewa maana ya usafirishaji haramu wa binadamu na kufahamu vipengele vya sheria ya usafirishaji haramu wa binadamu namba 6 ya mwaka 2008. Pia unalenga kutoa mwongozo kuhusu kanuni za msingi za kumtambua muathirika na kumpa ulinzi, pamoja na mikakati ya kuzuia na utetezi ikilenga kuipa nguvu mikakati ya kitaifa ya kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu nchini Tanzania.

### 1.3 Muundo wa mwongozo na kuwasilisha yaliyomo

Kimuundo, mwongozo huu umegawanywa katika sura sita pamoja na sura ya utangulizi. Sura ya kwanza inatoa historia ya kutengenezwa kwa mwongozo huu, inaelezea muundo na utangulizi. Sura ya pili inatoa mwongozo wa njia za kufundishia na inajumuisha matendo yaliyoandaliwa ili kuweka mazingira kwa ajili ya kuwezesha vipindi viende vizuri katika sura zilizobakia. Sura ya tatu inaelezea maana ya usafirishaji haramu wa binadamu. Katika sura hii tofauti kati ya usafirishaji haramu wa binadamu na magendo ya binadamu zinaangaliwa. Washiriki wataelezwa vipengele na hatua za usafirishaji haramu wa binadamu. Sura ya nne inahusu utambuzi wa muathirika. Inajadili kanuni za msingi zinazohusika na viashiria vikuu vinavyotumika kumtambua muathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu. Sura ya tano inajikita katika kutoa msaada wa moja kwa moja kwa waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu na kutoa mwongozo kuhusu kufanya tathmini ya hatari na rufaa. Sura ya sita inatoa muhtasari kuhusu ushirikiano kati ya asasi za kiraia na vyombo vya kutekeleza sheria.

Kila sura inaanza kwa kuorodhesha malengo mahususi ya kujifunza katika sura hiyo pamoja na matarajio ya matokeo, rasilimali zinazohitajika, muda unaotarajiwa kutumika, na marejeo muhimu yaliyotumika kukusanya nyenzo za kufundishia. Kila aya inaanza na utangulizi unaotoa taswira ya yaliyomo katika sura hiyo. Kuna mazoezi mbalimbali na visa mkasa katika kila moduli/sura, vinavyolenga kuhamasisha majadiliano ya pamoja kati ya washiriki katika masomo maalum katika kila sura. Mwongozo huu umetengenezwa kwa ajili ya matumizi ya washiriki ishirini. Wawezeshaji wanashauriwa kurekebisha muda unaotarajiwa na ukubwa wa vikundi kazi kama washiriki ni wengi zaidi.

# SURA YA PILI

## Mbinu za mafunzo

### 2.1 Utangulizi

Sura hii inalenga kutoa mwongozo wa njia za mafunzo, na inajumuisha shughuli ambazo zimetengenezwa ili kuweka mazingira mazuri kwa ajili ya uwezeshaji rahisi wa vipindi katika sura zilizobaki.

**Malengo:**

- Kuweka mazingira ya uaminifu, heshima na ushirikiano;
- Kufahamiana na kuelezea matarajio;
- Kuweka taratibu zitakazoongoza mafunzo.

**Matokeo yatarajiwayo:**

- Mazingira mazuri ya mafunzo;
- Uhusiano wa wazi na kweli kati ya washiriki na wawezeshaji;
- Taratibu zitakazozingatiwa wakati wa mafunzo.

**Rasilimali:** Bango kitita, kalamu za wino mzito, kalamu na madaftari.

**Muda uliopangwa:** Muda unaokadiriwa kwa ujumla ni dakika hamsini.

**Marejeo muhimu:** Moduli za mafunzo ya kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu za Shirika la Kimataifa –linaloshughulikia maswala ya wahamaji za mwaka 2006.

### 2.2 Changamoto za utofauti.

Usafirishaji haramu wa binadamuni tatizo gumu ambalo linahitaji ushirikiano miongoni mwa wadau mbalimbali katika ngazi ya mtaa, kitaifa, kikanda na kimataifa. Mwongozo huu wa mafunzo umetegenezwa kwa ajili ya matumizi ya asasi za kiraia nchini Tanzania zinazojumuisha taasisi mbalimbali na zenye historia tofauti zinazojihusisha na kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu.

> **KUMBUKA**
>
> Ni juu ya mwezeshaji kuchukua maarifa ya msingi yaliyomo katika mwongozo huu na kuyafanya yawe muhimu na ya manufaa kwa washiriki wa mafunzo.

Mashirika haya yanaweza kuwa na viwango tofauti vya maarifa na uzoefu wa somo hili.

Wawezeshaji watahitaji kutoa nafasi kwa ajili ya majadiliano kuhusu masuala na mbinu katika nyanja hii ya usafirishaji haramu wa binadamu.

Tofauti za maoni lazima zizingatiwe na kuheshimiwa bila kuhusisha mijadala yenye utata au kuzuia utambuzi wa masuala muhimu. Mafunzo yatilie mkazo maarifa ya msingi ambayo yatawawezesha washiriki mbalimbali kushiriki katika majadiliano ili mitazamo, nafasi na kanuni viweze kujadiliwa kwa undani zaidi.

Katika majadiliano yanayohusisha watu tofauti ni muhimu kutofautisha kwa usahihi ukiri na makubaliano, jambo la uhakika au kweli na lile la kusadikika au dhana, na maswali tofauti na maelezo.

Ili kukabiliana na changamoto zinazotokana na utofauti, wawezeshaji wanatakiwa kuzingatia lengo lao la uwezeshaji, kufuata taratibu za ufundishaji wa watu wazima, na kujitahidi kutumia lugha zisizo za kiufundi ili kutoa msingi wa ufahamu utakaoweza kutumika na watu mbalimbali ili kuboresha uwezo wao wa kushiriki katika shughuli za kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu.

> **DOKEZO**
>
> Elezea masuala mbalimbali bila kujaribu -kuyatolea majibu, fungua mjadala bila kujaribu kudhibiti matokeo, na sikiliza ili kuelewa na kuthibitisha utakachokisikia

#### 2.2.1 Kanuni za ufundishaji watu wazima

Watu wazima wanahitaji kufanikisha malengo yao ya mafunzo kwa njia ya moja kwa moja. Pale ambapo tofauti za mtu mmoja mmoja zinapoheshimiwa, washiriki wa mafunzo wanaweza kuunganisha uzoefu wao binafsi na nyenzo zilizopo na kujifunza kwa namna nzuri inayoendena na mahitaji yao. Wawezeshaji wanatakiwa kuangalia mchakato pamoja na mada wakati wa mafunzo. Mafunzo yenye ufanisi huzingatia uwiano kati ya uwasilishaji wa mada na ushirikishwaji wa washiriki ambao unaunganisha mada pamoja na mahitaji ya washiriki. Uwiano huu ukipatikana kikundi hujifunza kutoka kwa wajumbe wake pamoja na nyenzo zilizopo, na hatimaye jamii inayojifunza hujengeka.

Wawezeshaji wanaweza kukisaidia kikundi kuwa jamii inayojifunza kwa:

- Kutumia sehemu ya kwanza ya kila kipindi kwa ajili ya utambulisho, kupitia mpango mzima wa mafunzo na kujibu maswali yoyote kuhusiana na jinsi kipindi kitakavyoendeshwa. Hii ihusishe "maelekezo ya jumla kuhusu mafunzo" (kwa mfano, maelezo kuhusu ratiba, vitendea kazi, mapumziko na huduma za msaada);

- Kutumia lugha nyepesi, maelezo mbalimbali na uzoefu wa washiriki ili kusaidia uelewa wao kuwa rahisi zaidi bila kudhani kuna kiwango sawa cha uelewa baina ya washiriki wa mafunzo;

- Kutoa fursa za mara kwa mara kwa washiriki wa mafunzo ili kupima ufahamu wao, kuuliza maswali, kutoa maoni, na kutumia maudhui ya mafunzo kulingana na mazingira na matarajio yao. Mbinu hii inafanya nyenzo za mafunzo kuwa muhimu na inaonyesha heshima kwa mahitaji ya kila mtu na uzoefu wake;

- Kuendelea kulenga madhumuni ya mafunzo bila kutoka nje ya mada ili kuhakikisha majadiliano yanabaki katika njia sahihi. Wakati huo huo, majibu yote yazingatiwe na yawekwe katika namna ambayo inaonyesha yanaheshimiwa;

- Kuwasilisha mada ngumu na kwa kina katika mantiki sahihi ambayo inaongozwa na dhamira mbalimbali. Mambo ya kuzingatia ni kuwawezesha wawezeshaji kuzingatia taarifa muhimu wakati wa kutoa mafunzo.

- Kushiriki kama mmoja wa washiriki wa mafunzo lakini ukiwa na jukumu la uwezeshaji. Mawasiliano yako na washiriki wa mafunzo yanatakiwa yawe kama mawasiliano baina ya watu wenye dhamira moja ya kutaka kujifunza kuhusu kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu. Uzoefu wa kila mtu ukaribishwe, na unaweza kujenga mazingira mazuri kwa kushiriki kwenye majadiliano na pia kutumika kama mwezeshaji mkuu wa mafunzo.

Mazoea haya yanasisitiza mawasiliano kwa wakati wote wa kipindi na yanajumuisha ufafanuzi wa namna ya kuheshimiana na wakati huo huo yakizingatia maslahi ya kila mshiriki.

### 2.2.2 Uwezeshaji wa mafunzo

**Ubunifu** ni sehemu muhimu ya uwezeshaji mzuri na mafunzo. Miongozo ifuatayo inalenga kutoa mapendekezo na siyo maelekezo, na hivyo basi wakufunzi wanahamasishwa kujenga uwasilishaji ambao utafanikisha malengo ya mwongozo huu kwa ufanisi wenye uwiano kati ya mchakato mzima wa mafunzo na yaliyomo kwenye mwongozo. Wawezeshaji pia watambue mtindo binafsi wa uwezeshaji na jinsi unavyoendana na mazingira yaliyopo. Uwasilishaji wowote si lazima tu uwe kweli kwa maudhui na malengo ya mafunzo bali pia ni lazima uwe wa kimaadili, ukizingatia heshima na wenye mvuto kwa watu wanaojifunza kwa njia mbalimbali. Lengo liwe ni kutengeneza mazingira ambayo majadiliano huru na ya wazi yanategemewa na yana uhalisia. Ifuatayo ni miongozo michache itakayosaidia mafunzo yenye maadili kwa vitendo:

- **Tumia mbinu sahihi za kuuliza maswali** Usiulize swali ambalo linapendekeza jibu. "Kusoma mawazo" au kukisia nini mkufunzi anataka kusikia, hulifanya jibu kuwa sahihi kwa sababu zisizo sahihi, na haitoi nafasi kwa watu kujenga mawazo huru;

- **Epuka kuuliza maswali yenye majibu ya wazi** - Kwa mfano, muulize kila mtu atoe maoni yake kuhusu ni kwa namna gani suala fulani linamuathiri kulingana na mazingira yake, badala ya kuuliza kundi zima "Ni nani anaathiriwa na suala hili? au "mnafikiria nini juu ya suala hili?";

- **Nukuu majibu yanayohitaji ufafanuzi wa baadaye na uyazingatie** - Usipuuze maoni kwasababu hayatatutui mahitaji au matarajio yako. Hii itakusaidia kuyaongoza mawasiliano kwa urahisi zaidi bila kutumia mabavu au kutojali hisia za wengine;

- **Omba mrejesho katika njia ambayo itamruhusu kila mtu kushiriki** – Tumia watu wawili wawili, makundi madogo na mtu mmoja kwa wakati kama njia ya majadiliano ili kutoa fursa za ushiriki kwa umakini na bila upendeleo;

- **Epuka ushiriki shurutishi** - Usikilizaji unaweza kuwa ni njia muhimu ya kushiriki katika mafunzo. Inaweza kusaidia kwa kuonyesha kwamba jibu la "peleka kwa mtu mwingine" linakubalika pale ambapo mtu anahitaji muda wa kufikiri, anapendelea kusikiliza au hana kitu cha kuchangia kwa wakati ule. Weka wazi tangu mwanzo kwamba jibu hili ni sahihi;

- **Toa muda wa kufikiri wakati wa mazoezi** – Panga muda wa kufikiri wakati wa mazoezi kabla ya kuchukua majibu. Hii itaepusha hali flani ya ushindani ambapo "kuwa wa kwanza" inabadilisha matokeo ya malengo ya mafunzo;

- **Wasiliana na washiriki** - Uliza maswali maalumu na ya moja kwa moja ili kupima ni namna gani mafunzo yanaweza kukidhi mahitaji ya washiriki. Hii ni muhimu kwa vipindi kuanzia kwenye maswali wakati wa mazoezi ("je mnahitaji muda wa ziada?") hadi wakati wa kuwasiliana na kikundi kuhusu mazoezi yaliyopangwa na matokeo ("je kuna kitu chochote zaidi ambacho mnategemea kukifanikisha katika siku mbili hizi za mafunzo?)

**Kupanga matarajio**

**Mwezeshaji:** Huu utakuwa ni muda mzuri wa kuwapa washiriki maelezo ya madhumuni ya mafunzo. Majadiliano yako yanategemea kama unafanya mafunzo ya wakufunzi au ni ya ngazi ya ujuzi fulani. Hakikisha kwamba kila mtu anaelewa madhumuni ya mafunzo na matokeo yanayotarajiwa. Mapendekezo ya mazoezi yafuatayo yametengenezwa ili kumsaidia mwezeshaji na washiriki kuweka msingi mzuri wa majadiliano na kujenga mazingira mazuri ya majadiliano wakati wote wa mafunzo. Inashauriwa kuwa muwezeshaji achague moja au zaidi ya mazoezi yafuatayo ili kuyatumia mwanzo wa mafunzo.

**Zoezi 2a: Kufahamiana**

**Lengo:** Kuwatambulisha washiriki na wawezeshaji na kutengeneza mazingira mazuri ya mawasiliano

**Muda uliopangwa:** Dakika 25

**Mwezeshaji:**

- Wakaribishe washiriki wakae ikiwezekana katika umbo la 'U' ambapo wanaweza kuonana; mshukuru kila mmoja kwa kushiriki mafunzo; jitambulishe pamoja na wenzako na elezea jukumu la kila mmoja kwenye mafunzo hayo.

- Onyesha urafiki na uungwana.

- Omba washiriki wajitambulishe wenyewe; tambua mahali wanapotoka na mashirika yao (kama yapo).

- Wakati wa utambulisho, waombe washiriki kuelezea safari yao kubwa ya kwanza wakiwa mbali na nyumbani enzi za utoto wao na ni mambo gani ambayo wataendelea kuyakumbuka katika safari hiyo.

- Hakikisha kila mtu anapata fursa ya kutoa maoni yake.

- Baada ya kila mtu kujitambulisha, waulize washiriki wangejisikiaje kama mambo yangeenda tofauti katika safari yao hiyo muhimu ya kwanza. Elezea kwamba, wakati wa mafunzo kutakuwa na majadiliano ya kina kuhusu watu ambao safari zao ziliishia pabaya sana. Ainisha kwamba waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu mara nyingi huondoka majumbani mwao wakiwa na matumaini makubwa ya maisha bora bila kujua matumaini hayo hayatatimia.

- Malizia kipindi hicho kwa kuwashukuru na kuuliza kama wana maswali yoyote mpaka hapo.

**Zoezi 2c: Kupanga matarajio**

**Lengo:** kutambua malengo ya mafunzo ya washiriki na kuona kama mafunzo yatatekeleza malengo hayo. Pale ambapo hayatekelezi, mwezeshaji anaweza kufikiria kuweka vipindi katika mfumo wa ujumla wa ufundishaji katika mwongozo huu.

**Muda uliopangwa:** Dakika 12

Washiriki wanatarajiwa kuelezea kile wanachotarajia kupata kutoka kwenye mafunzo.

**Mwezeshaji:**

- Waulize washiriki matarajio yao ni nini kutokana na mafunzo. Ni kitu gani wanatarajia kuondoka nacho mwisho wa mafunzo?
- Nukuu majibu kwenye bango kitita.
- Nukuu pointi muhimu na epuka kurudia.
- Hakikisha kila mtu anapata nafasi ya kuchangia.
- Nukuu maamuzi yaliyokubalika na washiriki wote.
- Hitimisha kwa kusema kuwa orodha itapitiwa mwisho wa mafunzo ili kuona kama matarajio yamefikiwa na bandika majibu kwenye ukuta ambapo kila mmoja anaweza kuona.

# SURA YA TATU

## UELEWA WA USAFIRISHAJI HARAMU WA BINADAMU

### 3.1 Utangulizi wa Sura

Sura hii inajikita kwenye maana ya usafirishaji haramu wa binadamu na inaangalia asili na kiwango cha usafirishaji haramu katika ngazi za kimataifa na ndani ya Tanzania. Sura hii inatoa mtazamo wa mfumo mzima wa sheria za kimataifa na kitaifa zinazohusiana na usafirishaji haramu wa binadamu, na inaangalia mambo yanayofanana na kutofautiana kati ya usafirishaji haramu wa binadamu na magendo ya binadamu.

Washiriki pia wataelimishwa kuhusu vipengele au sifa husika na hatua mbalimbali za kosa la usafirishaji haramu wa binadamu.

**Malengo:**

- Kupata ufafanuzi kuhusu 'usafirishaji haramu wa binadamu';
- Kuelewa asili na kiwango cha usafirishaji haramu katika ngazi za kimataifa na ndani ya Tanzania;
- Kuorodhesha vifungu vya Itifaki ya Umoja wa Mataifa ya Usafirishaji Haramu wa Binadamu na Sheria ya Tanzania ya kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu;
- Kutambua matendo, njia na aina za unyonyaji zinazounda kosa la usafirishaji haramu wa binadamu;
- Kufafanua mambo yanayotofautiana na yanayofanana kati ya magendo ya binadamu na usafirishaji haramu wa binadamu;
- Kuelewa usafirishaji haramu wa watoto kama kesi maalum;
- Kutambua majukumu ya watoa huduma katika kukabiliana na usafirishaji haramu wa binadamu.

**Matokeo yanayotarajiwa:**

Mwisho wa kipindi washiriki wataweza:

- Kutambua hatua muhimu za usafirishaji haramu wa binadamu;
- Kuelewa asili na kiwango cha usafirishaji haramu katika ngazi za kimataifa na ndani ya Tanzania;
- Kupata uelewa wa itifaki ya Umoja wa Mataifa ya Usafirishaji Haramu wa Binadamu na Sheria ya Tanzania ya kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu;
- Kuelewa mambo yanayofanana na kutofautiana kati ya magendo ya binadamu na usafirishaji haramu wa binadamu;
- Kuelewa kwanini usafirishaji haramu wa watoto ni kesi maalumu;
- Kutambua majukumu/wajibu wa watoa huduma katika kukabiliana na usafirishaji haramu wa binadamu kwa ufanisi.

**Nyenzo za kufundishia:** Makala iliyorekodiwa 'Soul Trade', kama inapatikana, kesi na maswali katika mwongozo huu, bango kitita, na kalamu za wino mzito.

**Muda:** Masaa matano.

**Marejeo muhimu:**

**Itifaki ya Palermo, Sheria ya Tanzania, Ripoti ya marekani ya mwaka 2013 na machapisho ya IOM[1]**

- Protocol to Prevent, Suppress and Punish Trafficking in Persons, Especially Women and Children, Supplementing the United Nations Convention against Transnational Organized Crime, United Nations, 2000;
- The Anti-Trafficking in Persons Act No. 6 of 2008;
- United States Department of State 2013 Trafficking in Persons Report;
- The IOM Counter Trafficking Handbook for Law Enforcement Officers in Southern Africa, 2005;
- The IOM Counter Trafficking Training Modules Victim Identification & Interviewing Techniques, 2006;
- The IOM Handbook on Direct Assistance for Victims of Trafficking, 2007.

1 Marejeo haya hayana tafsiri rasmi kwa lugha ya Kiswahili.

## 3.2 Maana ya Usafirishaji Haramu wa Binadamu

**Zoezi 3a: Kueleza maana ya Usafirishaji Haramu wa Binadamu**

**Lengo:** Kuwawezesha washiriki kueleza maana ya usafirishaji haramu wa binadamu kwa usahihi.

**Muda:** Dakika 90

**Muwezeshaji:**

- Anza kipindi hiki kwa kuwauliza washiriki wanaelewa nini kuhusu istilahi ya "Usafirishaji haramu wa binadamu".

  Andika majibu kwa ufupi kwenye bango kitita. Wanaweza kutoa mifano ya kesi wanazozijua.

- Kama filamu iliyorekodiwa ya "Soul trade" ipo, inaweza kutumika kama nyenzo muhimu ya kuanzisha mjadala. Kama haipo waombe washiriki wasome hadithi ya Neema iliyotajwa hapo chini.
- Baada ya kuangalia makala/kusoma hadithi, waulize washiriki kama maoni yao yamebadilika baada ya kusoma hadithi / kuangalia makala.
- Andika majibu kwenye bango kitita. Jaribu kuongoza majadiliano ili kupata pointi zilizofupishwa katika makundi matatu tofauti ya kitendo, namna na kusudi au lengo. Maswali yatakayokusaidia kuongoza majadiliano ni pamoja na:
- Wasafirishaji haramu wa binadamu hufanya nini?
- Wasafirishaji haramu wa binadamu wanategemea kutimiza au kufikia lengo gani?
- Wanakusudia kufanya nini na waathirika wao?
- Wanafanya nini ili kufanikisha lengo lao?
- Wanawezaje kufanikiwa kuwadhibiti waathirika wao?
- Warejeshe washiriki kwenye maana ya usafirishaji haramu wa binadamu sehemu ya 2 ya Sheria ya Tanzania ya kupambana na Usafirishaji Haramu wa Binadamu. Uliza kama makala/kesi ya Neema inaendana na maana iliyotolewa kwenye Sheria. Tumia sehemu ya fasihi ya mwongozo kufuatilia majadaliano na eleza maana ya misamiati/istilahi iliyotumika kufafanua usafirishaji haramu wa binadamu, kama ilivyo kwenye sheria.

**KISA MKASA 3A: "Kuuzwa kwa Neema"**[2]

**(Angalia zoezi 3a)**

*Hii ni hadithi ya kweli ya Neema ambaye alikuwa msichana maskini wa kitanzania kutoka mkoani Kigoma ambaye alijitahidi sana kupambana ili aweze kuwa na maisha vizuri. Alichokifanya ni kuitikia wito wa tangazo kwenye gazeti lililosomeka "Wasichana na wanawake chini ya umri wa miaka 35. Kazi zinazolipa vizuri nje ya nchi". Alipiga simu na baadae aliweza kukutanana na kijana mmoja wa kiume ambaye alimuahidi mshahara wa dola za kimarekani elfu moja kwa mwezi kwa ajili ya kuwatunza wazee huko Italia.*[3] *"Nilikutana naye mwishoni mwa mwezi wa sita mwaka 2000, na mwishoni mwa mwezi wa saba niliuzwa kwenye baa iliyoko nchini Nairobi.......na nilifikiria ni kweli kuwa naenda Italia".*[4] *Katika mlolongo wa matukio uliohusisha kupatiwa nyaraka za kughushi, safari ndefu kwa njia ya barabara na kupelekwa maeneo mengi toka upande mmoja hadi mwingine ikiwemo Burundi, Rwanda na Uganda na mwishowe kutembea gizani ili kuvuka sehemu ya mpaka, akiwa pamoja na kundi la wanawake wadogo ambao alisafiri nao, hatimaye walifika nchini Kenya.*[5]

*Baada ya kufika, Neema na wenzake wakiwa baa kwa kifupi waliarifiwa kuwa kila mtu anadaiwa shilingi elfu hamsini, fedha za Kenya kama gharama za usafiri na wangeruhusiwa kuondoka endapo tu kila mtu atalipa deni hilo kwa mmiliki wa baa.*[6] *Neema alipata vipigo kadhaa vya mara kwa mara baada ya kukataa matakwa ya mmiliki wa baa, na hivyo basi Neema aliuzwa kwa mmiliki mwingine wa baa mjini Nairobi.*[7] *Kazi yake kubwa ilikuwa ni usafi wakati wa mchana, kucheza muziki jioni na wakati wote kuwa tayari kukodishwa kwa ajili ya wateja wakati wa usiku.*[8] *Mmiliki wa baa alimsajili kwenye kituo cha polisi kama mhudumu wa baa na angeanza kumlipa kiasi kidogo cha fedha mara tu atakapo kuwa amemaliza kulipia fedha zake alizomlipia wakati wa kumleta.*[9] *Neema alilazimika kujinunulia chakula chake mwenyewe pale baa ambapo ilikuwa ni vigumu kumudu. Lakini aliweza kutunza kiasi cha fedha alizopata kutoka kwa wateja wake waliomkodisha usiku.*[10] *Mwishoni mwa mwaka aliweza kufikisha karibu kiasi cha shilingi elfu ishirini na tano fedha za Kenya.*[11]

*Kufikia hapo, mmiliki wa baa alimtaarifu kuwa ameahidiwa fedha nzuri endapo atamuuza kwa mmiliki mwingine hivyo basi akampa fursa ya kuchagua kati ya kumlipa kiasi cha fedha alizohaidiwa na kuendelea kubaki naye au amuuze kwa mmiliki mwingine.*[12] *Akiogopa kukutana na sehemu mbaya zaidi, Neema aliamua kumlipa mmiliki wake kiasi chote cha fedha alichokuwanacho.*[13] *Mwaka mwingine ulipita kabla ya Neema kutoroka na kutafuta hifadhi Polisi.*[14] *Kipindi hicho, jicho lake moja lilikuwa tayari limepoteza nguvu ya kuona kutokana na kulegea kwa misuli ya mboni yake iliyosababishwa na vipigo vya mara kwa mara kichwani kutoka kwa bosi wake.*[15] *Kwa msaada wa Shirika la Kimataifa linaloshughulikia maswala ya wahamaji, Neema aliweza kurudi nyumbani.*

*Hana kazi na anatakiwa kumlea mwanae wa kiume na anapokea kiasi cha fedha kwa mwezi ambacho ni sawa na dola thelathini za Kimarekani kama msaada wa serikali kwa wasiojiweza.*[16]

2 Kisa mkasa hiki kinatoka kwenye chapisho lisilo na tafsiri ya lugha ya Kiswahili linaloitwa 'Waugh Selling Olga: Stories of Human Trafficking and Resistance (2006) p16 angalizo: mabadiliko yamefanyika kuhusiana na miji na majina'.

3 Ukurasa 16

4 Ukurasa 17

5 Ukurasa 18-20

6 Ukurasa 20

7 Ukurasa 21

8 Ukurasa 21

9 Ukurasa 21

10 Ukurasa 21

11 Ukurasa 22

12 Ukurasa 23

13 Ukurasa 23

14 Ukurasa 24

15 Ukurasa 25

16 Ukurasa 25

### 3.3 Usafirishaji Haramu wa Binadamu: Mtazamo wa Dunia

Uhamaji ni moja ya mambo yanayoitambulisha dunia katika karne ya ishirini na moja, kwa sababu watu wengi zaidi wanahama kuliko nyakati nyingine zozote katika historia ya binadamu. Kuna zaidi ya watu milioni mia moja na tisini na mbili waishio nje ya nchi walikozaliwa, ambayo ni karibia asilimia tatu ya watu wote ulimwenguni.[17] Katika hilo, pia kanda ya Afrika ya Mashariki haijaachwa nyuma. Watu wanahama kwa lengo la kutafuta fursa nzuri za ajira na elimu. Uhamaji huu unaweza kuwa wa ndani ya nchi au wa kuvuka mipaka ya nchi. Mara nyingi hufuata mifumo iliyoundwa kwa vizazi vingi. Katika Afrika mashariki mfumo wa uhamaji wa ndani na nje umebadilika sana kwa zaidi ya miongo mitatu iliyopita na kuna uwezekano wa kuendelea kubadilika kwa wakati ujao. Wahamiaji hufanya kazi katika sekta mbalimbali ikiwa ni pamoja na uzalishaji, biashara isiyo rasmi, kilimo, ujenzi na kazi za ndani.[18] Ingawa mtazamo uliopo ni kuwa uhamaji una faida kote, katika nchi ambayo mtu anatoka na anakoelekea, uhamaji usipodhibitiwa unaweza kuhusisha madhara kijamii, kifedha na kisiasa kwa watu, jamii na serikali na pia kujumuisha uhamiaji usio rasmi, magendo ya binadamu na usafirishaji haramu wa binadamu.[19]

#### 3.3.1 Taarifa na takwimu katika ngazi za kimataifa

Usafirishaji haramu wa binadamu ni biashara kubwa inayohusisha magenge yanayofanya uhalifu wa kupangwa wenye faida kubwa inayoweza kufikia fedha za kimarekani bilioni 32 kwa mwaka.[20]

Na hii inafanya usafirishaji haramu wa binadamu kuwa biashara ya uhalifu yenye faida kubwa ambayo ni ya tatu kimataifa, ikitanguliwa na biashara ya madawa ya kulevya na biashara holela ya uuzaji silaha.

Shirika la Kazi Duniani (ILO) linakadiria kuwa kuna watu zaidi ya milioni kumi na mbili na laki tatu duniani wanaoishi kwa namna moja ama nyingine ya utumwa.[21] Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) linakadiria kuwa zaidi ya watoto milioni moja wanasafirishwa kiharamu kila mwaka.[22] Nukuu ya makadirio inayorudiwa mara nyingi kutoka ripoti ya Kitengo cha wamarekani kinachotoa taarifa kila mwaka kuhusu hali na utekelezaji wa sera za kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu katika nchi mbalimbali duniani inaweka namba ya watu wanaosafirishwa kila mwaka ni kati ya laki sita na laki nane.[23] Kutokana na takwimu za Shirika la Kazi Duniani (ILO), kwa sasa inaaminika kwa kiasi kikubwa kwamba, kimataifa, waathirika wengi wa usafirishaji haramu wa binadamu husafirishwa kwa lengo la kufanyishwa kazi kwa nguvu au kwa kulazimishwa.[24] Hata hivyo vyombo vya habari na wanataaluma wamekuwa wakijikita zaidi kwenye usafirishaji haramu wa binadamu kwa lengo la kufanyishwa shughuli za ngono ambayo inahusisha sehemu kubwa ya usafirishaji haramu wa binadamu kwa ujumla.[25]

Jambo hili lilianza kupewa kipaumbele na umma baada ya ripoti za wasichana wa Ulaya ya Mashiriki waliokuwa wanasafirishwa Magharibi kwa lengo la ukahaba kufuatia kuvunjika kwa Muungano wa Soviet kutolewa.[26] Ripoti hizi zililenga ongezeko kubwa la soko la biashara ya ngono yenye sifa ya ukatili. Jinsi wakati ulivyoendelea kwenda mbele, labda kutokana na mabadiliko ya vipaumbele vya vyombo vya habari, watu wengi walichukulia usafirishaji haramu wa

17 Kuhusu uhamiaji, http://www.iom.int/jahia/jahia/about-migration/lan/en

18 Chapisho la shirika la kimataifa la linaloshughulikia masuala ya uhamiaji, IOM, Sonke Gender Justice Network, An Action Oriented Training Manual on Gender, Migration and HIV (2009) 22

19 http://www.iom.int

20 Chapisho la ILO, "Belser Forced Labour and Human Trafficking: Estimating the Profits-ILO Working Paper 42(2005) uk 17

21 Uk 4

22 Chapisho la UNCEF, UNICEF, the State of the World's Children: Excluded and Invisible (2006) uk 50

23 Repoti ya wamarekani "US Department of State Office to Monitor and Combat Trafficking in Persons, Trafficking in Persons Report (2005) http://www.state.gov/g/tip/rls/tiprpt/2005/46606.htm

24 Rejea chapisho ripoti ya ILO rejeo na.20

25 Repoti ya wamarekani "US Department of State Office to Monitor and Combat Trafficking in Persons, Trafficking in Persons Report: Major Forms of Trafficking in Persons (2009) http://www.state.gov/g/tip/rls/tiprpt/2009/123126.htm

26 Chapisho linaloitwa kwa lugha ya kiingereza Okolski "Illegality of International Population Movements in Polland" 2000 (38) International Migration p 55, 77-80

binadamu kama tatizo la kusini mashariki mwa Asia.[27] Ilichukua miaka mingi kwa dunia kutambua kwamba karibia sehemu zote za dunia zimeathirika na tatizo hili, na katika usafirishaji, nchi inaweza kuwa ya mwanzo, kati, mwisho au mchanganyiko wa zote kwa pamoja. Uthibitisho wa wazi kwamba Usafirishaji haramu wa binadamu umekuwa tatizo la duniani kote unapatikana kwenye ripoti ya kitengo cha wamarekani kinachotoa taarifa kila mwaka kuhusu hali na utekelezaji wa sera za kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu katika nchi mbalimbali duniani.

**Taarifa na takwimu za Usafirishaji Haramu wa Binadamu duniani: (Ripoti ya marekani ya Usafirishaji Haramu wa Binadamu ya mwaka 2011)**

- 3619 (237)* - Hukumu za usafirishaji haramu wa binadamu zilizofanikiwa mwaka 2010
- 6,017 (607)* - Mashtaka ya usafirishaji haramu wa binadamu yaliyofanikiwa mwaka 2010
- 33,113 – Waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu waliotambuliwa
- 17 – Sheria/Kanuni mpya au zilizofanyiwa marekebisho mwaka 2010

**Taarifa na takwimu za Usafirishaji Haramu wa Binadamu duniani: (Ripoti ya Marekani ya Usafirishaji Haramu wa Binadamu ya mwaka 2010)**

- Milioni 12.3 – Watu wazima na watoto walioko kwenye kazi za kulazimishwa na kifungo na wamehusishwa na unyonyaji wa kingono
- 4,200 – Mashtaka ya usafirishaji haramu wa binadamu yaliyofanikiwa mwaka 2009
- 50,000 - Waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu waliotambuliwa
- 0.4% - waathirika waliotambuliwa kama uwiano wa jumla wa makadirio waathirika wote.
- 1.8 kwa kila wakazi 1,000 – Kuenea kwa waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu (makadirio ulimwenguni/duniani)

*Namba zilizo kwenye mabano ni zile za mashtaka na hukumu ya usafirishaji kwa lengo la kufanyishwa kazi

27 Chapisho kwa lugha ya kiingereza linaloitwa Skeldon "Trafficking: A perspective from Asia" 2000 (38) International Migration p 7, 8

### 3.3.2 Itifaki ya Umoja wa Mataifa ya Kuzuia, Kupambana na Kuadhibu Usafirishaji Haramu wa Binadamu, hasa kwa Wanawake na Watoto ('Itifaki ya Palermo')[28]

Usafirishaji haramu wa binadamu umefafanuliwa na sheria ya kimataifa kwenye Itifaki ya Umoja wa Mataifa ya Kuzuia, Kupambana na Kuadhibu Usafirishaji Haramu wa Binadamu, hasa kwa Wanawake na Watoto ('Itifaki ya Palermo'). Itifaki hii ni Nyongeza ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kupinga Uhalifu wa Kimataifa wa Kupangwa (UNTOC), 2000. Ibara ya 3 ya itifaki imetafsiri usafirishaji haramu wa binadamu kama:

*"Usafirishaji haramu wa binadamu utakua na maana ya usaili, usafirishaji, uhamishaji, uhifadhi au upokeaji watu, kwa njia ya vitisho au matumizi ya nguvu au aina nyingine ya matumizi ya nguvu, utekaji nyara, udanganyifu na matumizi mabaya ya madaraka au cheo, mazingira magumu au kutoa au kupokea malipo au faida ili kupata ridhaa ya mtu na udhibiti, kwa lengo la unyonyaji".*

Unyonyaji utajumuisha, unyonyaji katika ukahaba au aina nyingine za unyanyoji kingono, kufanyishwa kazi kinguvu, utumwa, au matendo yanayofanana na utumwa au kuondolewa viungo vya mwili.

Nchi inapokua mwanachama wa mkataba wa Umoja wa Mataifa dhidi ya Uhalifu wa Kimataifa wa Kupangwa na Itifaki ya Palermo (hapa itajulikana kama Itifaki), ina wajibu wa kurekebisha sheria za makosa ya jinai ili ziendane na mikataba hii. Maneno yanaweza kutofautiana ila matendo yote ya usafirishaji haramu wa binadamu yanatakiwa kuwa ni miongoni mwa makosa ya jinai.

Ibara ya 5 ya Itifaki ya Palermo inazitaka nchi wanachama watengeneze sheria ya kufanya usafirishaji haramu wa binadamu kuwa kosa la jinai kama ilivyofafanuliwa kwenye ibara ya 3 hapo juu. Zaidi ya kufanya usafirishaji haramu wa binadamu kuwa kosa la jinai, itifaki inahitaji yafuatayo kujumuishwa katika makosa ya jinai:

- Kujaribu kutenda kosa la usafirishaji haramu wa binadamu;
- Kushiriki kama msaidizi wa kutenda kosa hili;
- Kuwapanga au kuwaelekeza wengine kutenda kosa la usafirishaji haramu wa binadamu.

28 Itifaki ya Palermo ambayo haina tafsiri kwa lugha ya Kiswahili "The United Nations Protocol to Prevent, Suppress and Punish Trafficking in Persons, especially Women and Children)

Kulingana na maana iliyotolewa katika ibara ya 3(a) ya Itifaki, usafirishaji haramu wa binadamu una vipengele vikuu vitatu: kitendo (nini kilifanyika), namna (kwa namna gani kilifanyika) na Lengo (mara zote ni unyonyaji).

**Kitendo:** Kitendo cha usafirishaji haramu wa binadamu kinamaanisha hatua zinazotumiwa na wasafirishaji (kwa mfano kitu kinachofanyika) kumuingiza na kumuendeleza muathirika katika tukio la usafirishaji. Matendo haya kama yalivyoainishwa katika Itifaki yakisimama peke yake sio jinai bali mpaka yambatane na mambo makuu mawili. 1) Dalili kwamba kitendo kilifanyika bila ridhaa au ridhaa kamili haikupatikana na 2) Muelekeo kwamba nia ya kitendo ni unyonyaji.

**Namna:** Namna (kwa mfano jinsi) iliyotumika kumsafirisha mtu, inamaanisha namna ambayo msafirishaji anamuingiza au kumuendeleza mtu katika usafirishaji haramu wa binadamu. Njia zinazotumiwa na wasafirishaji zinajumuisha uongo, udanganyifu na matumizi mabaya ya nafasi aliyonayo mtu au nafasi ya udhaifu wa mtu mwingine na inaweza kutokea kwa au bila kutumia nguvu. Matumizi mabaya ya nafasi aliyonayo mtu au nafasi ya udhaifu wa mtu mwingine kama ilivyoainishwa katika ibara ya 3 ya Itifaki inaeleweka kumaanisha hali yoyote ambayo mtu anayehusishwa hana njia nyingine zaidi ya kukubali kuhusishwa na unyonyaji. Hii ni kukubali kwamba wasafirishwaji wengi huwa kwenye mazingira ya udhaifu dhidi ya wale wanaowasafirisha, mtu mwenye mamlaka, mzazi au mlezi.

**Lengo (unyonyaji):** Sababu kuu ya usafirishaji haramu wa binadamu ni unyonyaji. Maana ya usafirishaji haramu wa binadamu katika Itifaki ya Palermo inajumuisha aina zifuatazo za unyonyaji: umalaya, unyonyaji wa kingono, kufanyishwa kazi kwa nguvu, utumwa na matendo ya kufanana au kuondolewa viungo. Kulingana na Itifaki, unyonyaji unajumuisha aina za unyonyaji unaotokea hata kidogo. Hii inamaanishwa kwamba, orodha iliyotolewa katika Ibara ya 3 si kamili. Kila nchi inaweza kuongeza njia nyingine za unyonyaji katika sheria za ndani ya nchi zao, kulingana na uzoefu wa aina mbalimbali za usafirishaji haramu wa binadamu.

**Unyonyaji kwa ajili ya umalaya na unyonyaji kingono** haujaelezewa katika Itifaki au mahali pengine katika sheria ya kimataifa. Ziliachwa kwa makusudi ili kuruhusu nchi kuridhia Itifaki ya Palermo bila kuzingatia kwamba umalaya ni kosa la jinai au la katika sheria za nchi zao.

**Mambo makuu matatu katika usafirishaji haramu wa binadamu**

| KITENDO | + | NJIA/NAMNA | + | LENGO |
|---|---|---|---|---|
| **(Kinachofanyika)** | | **(Kinafanyikaje)** | | **(Kwanini kinafanyika)** |
| **Kitendo cha:** | | **Kwa njia ya:** | | **Kwa lengo la Unyonyaji, ikiwa ni pamoja na** |
| Kusaili | | Vitisho Au | | Unyonyaji katika ukahaba au |
| Au | | | | Unyonyaji mwingine wa kingono |
| | | Matumizi ya nguvu au aina nyingine ya matumizi ya nguvu | | Au |
| Kusafirisha | | Au | | |
| Au | | | | Kufanyishwa kazi kwa nguvu na huduma nyingine |
| | | Utekaji nyara | | Au |
| Kuhamisha | | Au | | |
| Au | | | | Utumwa/na matendo yanayofanana na utumwa |
| | | Udanganyifu | | |
| Kuhifadhi | | Au | | Au |
| Au | | | | Utumwa |
| | | Matumizi mabaya ya madaraka au cheo, | | |
| Kupokea mtu | | Nafasi ya mtu ya mazingira magumu | | Au |
| | | Au | | Kuondoa viungo vya mwili |
| | | Kutoa au kupokea malipo au faida ili kupata ridhaa ya mtu | | |

**Ridhaa kama utetezi:** Usafirishaji haramu wa binadamu hauwezi kuhusisha ridhaa. Kwa kuongezea, kuwepo kwa ridhaa ya muathirika katika hatua moja ya usafirishaji haramu wa binadamu hakuwezi kuchukuliwa kama ni ridhaa katika hatua zote za usafirishaji haramu huo. Hii ina maana, kama mtu aliridhia kufanya kazi ughaibuni ama kuingia kwenye nchi nyingine kinyume cha sheria, lakini hakuridhia kufanyiwa vitendo vya unyonyaji, basi kosa litakuwa limetendeka. Kwa watoto, ridhaa haina umuhimu kwa sababu mtoto hana uwezo wa kukubali kuingia katika makubaliano yatakayompelekea kuingia katika usafirishaji haramu wa binadamu, hata kama wazazi wake wametoa ridhaa hiyo.

**Mazingira maalum ya watoto:** Itifaki ya Kupambana na Usafirishaji Haramu wa Binadamu inatambua mazingira maalum yanayowakabili watoto hivyo ibara ndogo ya C inaondoa haja ya kuwa na njia ili usafirishaji haramu wa mtoto utimie. Ibara ya 3(c) imetafasiri usafirishaji haramu wa mtoto kama "Usaili, usafirishaji, uhamishaji, uhifadhi au upokeaji wa mtoto kwa lengo la unyonyaji". Kwa maana nyingine, kwa watoto si lazima kuwa na matumizi ya nguvu au udanganyifu ili usafirishaji haramu utokee. Kwa kesi inayohusu mtoto, si tu kwamba ridhaa itakatakaliwa kama ushahidi bali hata njia zilizotajwa hapa. (Angalia sehemu ya 3.7 ya kitabu hiki kwa maelezo zaidi).

### 3.3.3 Taarifa/Ripoti ya Marekani ya Usafirishaji Haramu wa Binadamu

Ofisi ya kufuatilia na kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu kutoka kitengo kinachohusika na maswala ya nchi-Marekani, hutoa taarifa ya kila mwaka ya usafirishaji haramu wa binadamu ambayo inafuatilia juhudi za nchi mbalimbali za kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu kulingana na viwango vilivyowekwa kwenye Sheria ya Marekani ya kuwalinda waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu ya mwaka 2000, kama ilivyorekebishwa.

Hatahivyo, viwango vilivyoko kwenye sheria hiyo kwa kiasi kikubwa vinaendana na mfumo wa kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu ulioko kwenye Itifaki ya Palermo. Zote zinafafanua usafirishaji haramu wa binadamu kama mkusanyiko wa vitendo, njia na lengo. Zote zinaelezea matumizi ya nguvu, udanganyifu au aina nyingine ya matumizi ya nguvu kwa lengo la kupata huduma ya mtu mwingine. Na zote zinakubaliana kwamba si lazima uhamisho ufanyike, sura ya uhalifu wenye unyonyaji wa hali ya juu unalitambulisha kosa hili. Taarifa ya kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu inaiweka kila nchi katika mojawapo ya viwango vitatu, kama sheria ya marekani ya kuwalinda waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu inavyoelekeza.

Uwekwaji wa nchi katika mojawapo ya viwango hivi vitatu unategemea jitihada za serikali katika kufikia vigezo viliyowekwa kwenye viwango vya sheria ya kuwalinda waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu kama ilivyoainishwa kwenye dhana iliyojikita katika mambo makuu matatu: Kufungua mashtaka, Ulinzi na Uzuiaji. Nchi ambazo serikali zake zinazingatia vigezo vilivyoainishwa kwenye sheria ya Marekani ya kuwalinda waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu zinawekwa katika nafasi ya kwanza (Tier 1)[29]. Ingawa nafasi ya kwanza ni ya juu kabisa, haina maana kwamba nchi hizo hazina tatizo la usafirishaji haramu wa binadamu. Bali, nafasi ya kwanza inaonyesha kuwa nchi imekubali uwepo wa usafirishaji haramu wa binadamu, na imefanya jitihada katika kupambana na tatizo hilo, na inatimiza vigezo vya matakwa yaliyoainishwa kwenye sheria ya Marekani ya kuwalinda waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu. Kila mwaka, serikali zinatakiwa kuonyesha jitihada madhubuti katika kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu ili kuendelea kubaki kwenye nafasi ya kwanza. Hakika nafasi ya kwanza inaonyesha jukumu kubwa badala ya ahueni. Nafasi ya pili ni kwa zile nchi ambazo hazijatimiza vigezo vya chini vya sheria, lakini zinaonekana kufanya jitihada za kutosha katika kutimiza vigezo hivyo. Nafasi ya pili chini ya uangalizi ni kwa ajili ya nchi zilizoko nafasi ya pili ambazo zimetathminiwa kutoonyesha jitihada za kutosha katika kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu uliokithiri kwa mwaka uliopita; au nchi zimeainisha "jitihada hizo" ambazo zitapewa kipaumbile cha utekelezwaji katika mwaka unaofuata; ama idadi ya waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu uliokithiri ni kubwa au inaendelea kuongezeka zaidi. Nafasi ya tatu ni kwa ajili ya nchi ambazo zimetathminiwa kutokidhi vigezo vya chini vilivyowekwa na hazionyeshi jitihada zozote za kufikia vigezo hivyo. Kwa mujibu wa, sheria ya Marekani ya kuwalinda waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu, serikali za nchi zilizoko kwenye nafasi ya 3 zinaweza kuwekewa vikwazo fulani, ambapo serikali ya Marekani inaweza kuzuia au kuondoa baadhi ya misaada ya kimataifa ambayo si ya kibinadamu au kibiashara. Kulingana na sheria ya Marekani ya kuwalinda waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu, Serikali ambazo zitawekewa vikwazo pia zitakumbana na upinzani wa Marekani kuhusu misaada (isipokuwa misaada ya kibinadamu, ya kibiashara na ya maendeleo fulani) kutoka taasisi za kimataifa kama mfuko wa kimataifa wa fedha (IMF) na benki ya dunia (World Bank). Hakuna upangaji wa nafasi (Tier) ulio wa kudumu. Kila nchi inaweza kufanya vizuri zaidi ikiwemo Marekani. Lazima nchi zote ziendelee kudumisha na kuongeza juhudi katika kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu.

## 3.4 Usafirishaji Haramu wa Binadamu Tanzania

### 3.4.1 Maelezo kutoka katika Taarifa ya Usafirishaji Haramu wa Binadamu ya mwaka 2013-Tanzania[30]

(Angalizo: Taarifa hii hutolewa kila mwaka. Wawezeshaji na washiriki wanashauriwa kurejea katika ripoti ya karibuni wakati wa mafunzo.)

**Maelezo ya jumla:** Tanzania ni nchi ya mwanzo, ya kati na ya mwisho kwa wanaume, wanawake, na watoto wanaoingizwa katika kazi za kulazimishwa na usafirishwaji kwa ajili ya ngono. Tukio la usafirishaji wa ndani ni kubwa kuliko lile la usafirishaji wa kimataifa, na mara nyingi huwezeshwa na wanafamilia, marafiki au watu wa kati ambao huahidi kutoa msaada wa elimu au kutafuta ajira zenye faida kubwa katika maeneo ya mijini.

Unyonyaji wa wasichana wadogo kwa kupitia katika kazi za ndani unaendelea kuwa tatizo kubwa la usafirishaji Tanzania, ingawa matukio ya usafirishaji

29 Taarifa ya wamarekani "US TIP Report 2010: Tier Placements"

30 Taarifa ya wamarekani "US Department of State Office to Monitor and Combat Trafficking in Persons Report: Tanzania (2013)"

haramu wa watoto kwa ajili ya biashara ya ngono yameongeza katika mipaka ya Kenya na Tanzania.

Wasichana wananyonywa kupitia usafirishaji haramu wa binadamu kwa lengo la ngono katika maeneo ya utalii ndani ya nchi. Wavulana wanahusishwa na kufanyishwa kazi kwa nguvu hasa katika mashamba, lakini pia kwenye migodi, katika sekta ya biashara isiyo rasmi, biashara ya ngono na inawezekana katika boti ndogo za uvuvi.

Idadi ndogo ya watanzania ambao ni watoto na watu wazima wanasafirishwa mara nyingi na watanzania wengine kwenda kufanya kazi za ndani kama watumwa, aina nyingine ya kazi za kulazimishwa, na biashara ya ngono katika nchi zingine ikiwa ni pamoja na Msumbiji, Ethiopia, Afrika Kusini, Uganda, Yemen, Oman, Falme za Kiarabu, Saudi Arabia, Uingereza, Marekani, Ufaransa na katika nchi nyingine za Afrika, Mashariki ya Kati na nchi za Ulaya.

Waathirika waliosafirishwa kutoka nchi nyingine kwa kawaida watoto kutoka Burundi na Kenya, ikiwa ni pamoja na Bangladesh, Nepal, Yemen na India, wanalazimishwa kufanya kazi Tanzania katika sekta ya kilimo, madini na sekta za huduma za ndani; baadhi pia wanahusishwa na bishara ya ngono.

Raia wa nchi jirani wanaweza kwa hiari kuhamia Tanzania kabla ya kusafirishwa kwenda Afrika Kusini, Ulaya na Mashariki ya Kati kwa ajili ya kazi za ndani na biashara ya ngono. Baadhi ya watoto wafanyakazi wa ndani hupata chumba na malazi, ila wengine hunyimwa chakula, hupigwa na hunyimwa kulala, au hufanyishwa kazi kupita kipimo kiasi cha kuchoka - matendo yanayoashiria ufanyishwaji kazi kwa nguvu.

Serikali ya Tanzania haijatimiza kikamilifu wala kuzingatia kwa viwango vya chini vya kutokomeza usafirishaji haramu wa binadamu; hata hivyo inafanya jitihada kubwa ya kufanya hivyo. Serikali imehukumu watuhumiwa wanne ambao ni wasafirishaji wa kimataifa kwa lengo la kazi na inaendelea kutoa rufaa kwa waathirika waliotambuliwa ambao ni watoto katika mashirika yasiyo ya kiserikali kwa ajili kupata huduma. Katika kesi moja ya mafanikio, serikali iliwapa fidia ya kifedha waathirika wanne ambao ni watu wazima, kutokana na faini waliyopewa wahalifu. Hata hivyo, ilishindwa kuwaadhibu wahalifu ipasavyo kwa sababu haikutoa hukumu inayolingana na uzito wa makosa yaliyotendeka.

### 3.4.2 Sheria ya Kupambana na Usafirishaji Haramu wa Binadamu[31]

Tanzania iliridhia Itifaki ya Umoja wa Mataifa ya Kuzuia, Kupambana na Kuadhibu Usafirishaji Haramu wa Binadamu, hasa kwa Wanawake na Watoto (Nyongeza ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kupinga Uhalifu wa Kimataifa wa Kupangwa) mnamo mwaka, 2000, na kwa kufanya hivyo iliazimia kuchukua hatua madhubuti za kuzuia na kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu. Kwa hiyo, mwaka 2008 Tanzania ilipitisha sheria ya kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu (sheria No. 6 ya mwaka 2008). Sheria hii imeanza kutumika, mashtaka yamefunguliwa na hukumu zimetolewa[32].

Kifungu cha 4 cha sheria hii kinatafsiri usafirishaji haramu wa binadamu kama (ilivyofupishwa);

(**Kitendo**) "kusaili, kusafirisha, kuhamisha, kuhifadhi, kupokea mtu kwa…

(**Njia**) za vitisho au kutumia nguvu, udanganyifu au ulaghai, kwa…

(**Lengo** la unyonyaji): Sheria inatafsiri unyonyaji kuhusiana na usafirishaji haramu wa binadamu kujumuisha:[33]

- Ukahaba/umayala na aina zingine za unyonyaji kingono;
- Kufanyishwa kazi au kutoa huduma kwa nguvu;
- Utumwa na matendo yanayofanana na utumwa;
- Kuondoa viungo vya mwili.

**Mazingira ambayo hayawezi kutumika kama utetezi:**

Sheria ya Kupambana Usafirishaji Haramu wa Binadamu imeorodhesha masuala ambayo hayawezi kutumika kama utetezi katika kesi za usafirishaji haramu wa binadamu. Kifungu cha 4(3) na (4) cha Sheria kinatamka:

- "Pale ambapo muathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu ni mtoto, ridhaa ya mtoto, mzazi au mlezi haiwezi kutumika kama utetezi wa mashitaka chini ya sheria hii bila kujali kuwa kuna ushahidi wa matumizi mabaya ya madaraka, udanganyifu, ulaghai au uwepo wa mazingira hatarishi ya mtoto umetumika vibaya" na
- "Ridhaa ya muathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu haitasaidia katika utetezi pale ambapo vitisho, matumizi ya nguvu, udanganyifu, ulaghai, ukatili au vitisho kwa lengo la kuondoa au kuuza viungo vya binadamu vilitumika".

31 Sheria hii haina tafsiri kwa lugha ya Kiswahili "The Anti-Trafficking in Persons Act, 2008"

32 Taarifa ya wamarekani "US Department of State Trafficking in Persons Report 2013"

33 Angalia Kifungu cha 2

**Adhabu kama zilivyoainishwa katika Sheria ya Kupambana na Usafirishaji Haramu wa Binadamu**

| Kifungu | Kosa | Adhabu (TZS) |
|---|---|---|
| Kifungu cha 4 | Vitendo vya usafirishaji haramu wa binadamu | Faini isiyopungua shilingi milioni 5 na isiyozidi milioni 100 au kifungo cha miaka 2 hadi 10 au vyote kwa pamoja kifungo na faini |
| Kifungu cha 5 | Vitendo vinavyochochea au kuwezesha usafirishaji haramu wa binadamu. | Faini isiyopungua shilingi milioni 2 na isiyozidi shilingi milioni 50, au kifungo cha mwaka 1 hadi 7 au vyote kwa pamoja kifungo na faini |
| Kifungu cha 6 | Usafirishaji haramu wa binadamu uliokithiri | Faini isiyopungua shilingi milioni 5, na isiyozidi shilingi milioni 150 au kifungo cha miaka miaka 10 hadi 20 au vyote kwa pamoja kifungo na faini |
| Kifungu cha 7 | Usafirishaji haramu wa binadamu kwa kumtumia mtu wa kati | Faini isiyopungua shilingi milioni 4 na isiyozidi shilingi millioni 150 au kifungo cha miaka 7 hadi 15 au vyote kwa pamoja kifungo na faini |
| Kifungu cha 8 | Matumizi ya wasafirishwaji kwa ajili ya ukahaba | Faini isiyopungua shilingi millioni 1 na isiyozidi shillingi millioni 30, au kifungo cha mwaka 1 hadi 7 au vyote kwa pamoja kifungo na faini. |

**Zoezi 3b: Kuelewa Hatua za Usafirishaji Haramu wa Binadamu**

**Lengo:** Kuwasaidia washiriki kutambua mbinu (njia) za Usaili, Usafirishaji, na Udhibiti zinazotumiwa na wasafirishaji kulingana na sheria ya kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu.

**Muda:** Dakika 75

**Mwezeshaji:**

- Waombe washiriki wajigawe kwenye makundi ya watu wanne au watano.
- Kila kundi lichague mwenyekiti na mtoa taarifa (msemaji).
- Kwa kila kundi, wape maelezo (na maswali yanayoendana).
- Msemaji atawasilisha majibu (matokeo) kwa niaba ya kundi.
- Toa dakika 25 za majadiliano kwenye kundi.
- Toa dakika 8-10 za mrejesho kwa kila kundi.

Tumia majadiliano kwa kila maelezo ili kuwezesha majadiliano ya jumla kwa maswala yafuatayo:

- Maelezo namba 1 – Usafirishaji wa nje dhidi ya usafirishaji wa ndani, njia za kusafirisha, nyaraka zinazotumika kwenye safari, kwanini wasafirishaji wanawahamisha waathirika mbali na mazingira waliyoyazoea.
- Maelezo namba 2 – Njia zinazotumika na wasafirishaji katika kusaili waathirika, maswala ya ridhaa, aina mbalimbali za usaili (kwa mfano, mtindo na muundo).
- Maelezo namba 3 – Aina za unyonyaji, sehemu unyonyaji unapotokea.
- Maelezo namba 4 –Mahitaji na utoaji wa kazi na huduma yanayohusiana na usafirishaji haramu wa binadamu, unyonyaji kwa wanaume na wavulana.
- Maelezo namba 5 – Njia za udhibiti zinazotumiwa na wasafirishaji.
- Hitimisha kwa kuelezea mbinu (njia) kuu zinazohusika katika mchakato mzima wa usafirishaji haramu wa binadamu.

### 3.5 Usaili na Uhamasishaji

**Njia ya mawasiliano inayotumika kwenye usaili:**

Usaili unaweza kufanyika katika njia mbalimbali. Wasafirishaji wengine hutumia matangazo kupitia magazeti, au machapisho mengine ya kuwavutia waathirika, wengine hutegemea njia ya mazungumzo, mitandao shirikishi ya kijamii, intaneti na mawasiliano binafsi. Kimuundo, yanaweza kuanzishwa kama mashirika ya usafiri na ajira, ofisi za mawakala wa kazi au mawakala wa sekta ya burudani. Usaili unaweza pia kuendeshwa kwa kupitia mitandao ya watu binafsi au mtu binafsi anayefanya kazi kwa kujitegemea mwenyewe.

Wanafamilia wa muathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu kama vile wazazi, ndugu wa kuzaliwa, jamaa, marafiki wa kiume au wa kike na wanandoa, wanaweza pia kushiriki kwenye usaili.

Kwa mazingira ya usafirishaji haramu wa binadamu wa kimataifa au wa kuvuka mipaka ya nchi, usafirishaji huo huanzia katika nchi moja (au mahali) pa mwanzo na kuishia kwenye nchi nyingine (au mahali) pa mwisho. Kama muathirika atapita na kutumia muda kadhaa kwenye nchi ya tatu (au mahali), kwa kawaida itajulikana kama nchi ya kati. Waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu hunyonywa pindi wanapofika kwenye nchi ya mwisho. Hatahivyo, mtu hapaswi kupuuza ukweli kwamba unyonyaji wa waathirika wengi huanzia mahali pa kati, kabla hata ya kufika nchi ya mwisho.

**Njia za usafiri na nyaraka zitumikazo:**

Usafirishaji haramu wa binadamu wa kuvuka mipaka ya nchi unaweza kuwa kwa njia ya nchi kavu, anga au bahari. Isidhaniwe kwamba, nyaraka zote zinazotumika na wasafirishaji ni za kughushi. Pale ambapo nyaraka kama viza, hati za kusafiria za muda au pasipoti zinatumika zinaweza kuwa za kweli au za kughushi. Waathirika wengi husafiri kwa kutumia pasipoti halali na viza za kazi, masomo au utalii ambazo ni halisi. Mara nyingi wakati wa safari wasafirishaji huongozana na waathirika na huzuia nyaraka zao za kusafiria. Utaratibu huu huwezesha wasafirishaji waendelee kuwadhibiti waathirika na pia hufanikiwa kuwashawishi maafisa wa uhamiaji kuamini safari zao kutokana na maelezo yao wanayoyatoa kukubalika, ambayo huficha ukweli na pale inaposhindikana hulazimika kutoa hongo kwa maafisa hao ambao wanaweza kuharibu utaratibu mzima uliopangwa. Kwa ufupi, waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu wa kuvuka mipaka ya nchi wanaweza kusafirishwa kwa halali, kwa kufuata matakwa yote ya sheria za uhamiaji au kusafirishwa kinyume cha sheria, kwa kutumia nyaraka za kughushi na pia kwa njia ya magendo ya binadamu.

Hata hivyo, usafirishaji haramu wa binadamu unaweza kutokea bila hata ya kuvuka mipaka ya nchi. Hii inajulikana kama usafirishaji haramu wa binadamu wa ndani ya nchi. Usafirishaji haramu wa binadamu wa ndani unaweza kutokea bila hata muathirika kuhamishwa kabisa. Kwa mfano, pale ambapo muathirika husailiwa au huhifadhiwa kwa lengo la unyonyaji bila hata kuhamishwa kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine.

**Kwanini mara nyingi wasafirishaji huwahamisha waathirika:**

Kwenye usafirishaji haramu wa binadamu wa kuvuka mipaka ya nchi (na usafirishaji haramu wa binadamu wa ndani unaohusisha uhamisho), kumhamisha muathirika mbali na sehemu yake ya asili kuna manufaa makubwa kwa msafirishaji. Kimsingi, hii inakusudia kumtenganisha muathirika na mazingira aliyoyazoea ambayo yangeweza kuzuia lengo la unyanyasaji na unyonyaji lisitimie. Itakuwa vigumu kwa waathirika kutafuta msaada kama hawajui jiografia, lugha, utamaduni na mpangilio wa mazingira hayo mapya, na hii husaidia waendelee kunyonywa. Uhamisho endelevu pia husaidia kumkanganya muathirika na humwia vigumu kuanza kutafuta njia ya kurudi alikotoka (sehemu ya asili).

#### 3.5.1 Mbinu za udhibiti (rejea sehemu ya pili, kifungu cha 4 cha Sheria)

Ili kuweza kupata hukumu katika kesi za usafirishaji haramu wa binadamu, waendesha mashitaka watahitaji kuhakikisha kuwa kosa limetendeka kwa kupitia moja ya njia zilizoorodheshwa katika sehemu ya II, kifungu cha 4 cha sheria mfano: vitisho, nguvu, udanganyifu na matumizi mabaya ya madaraka. Kuna uwezekano wa kujumuisha njia zilizotumiwa na wasafirishaji ambazo zote zina tabia moja kuu ya kufanana kwa mfano, zote zinaashiria kutokuwepo kwa ridhaa huru kwa upande wa muathirika. Kwahiyo, ridhaa ya muathirika huwa inaharibiwa kisheria kwa sababu imepatikana kupitia mojawapo ya njia hizi. Njia zinazotumika na wasafirishaji dhidi ya wasafirishwaji zinaweza kuwekwa katika makundi mawili ambayo mara nyingine huingiliana: udanganyifu na matumizi ya nguvu.

**Udanganyifu:** Kwa suala la udanganyifu, kutakuwa na haja ya kutofautisha kati ya udanganyifu kamili na ule wa kiasi. Pale ambapo msafirishaji anatoa ahadi ya kumtafutia kazi za ndani muathirika na hatimaye kumsababishia kuingia kwenye ukahaba, udanganyifu huu ni kamili. Hatahivyo, kwa kesi zingine, msafirishaji anaweza kuelezea ukweli kuhusu baadhi ya mipango lakini si yote. Kesi kama hiyo itakuwa pale ambapo muathirika kwa ufahamu wake mwenyewe anakubali kuhusishwa kwenye ukahaba lakini haelezwi ukweli

kuhusu mazingira ya unyanyasaji na unyonyaji atakayokutana nayo. Kwahiyo, ile ridhaa dhahiri ya muathirika inaharibiwa.

**Matumizi ya nguvu:**

Njia za matumizi ya nguvu zinajumuisha matumizi ya nguvu yenyewe, vitisho, kuteka, matumizi mabaya ya madaraka na mazingira hatarishi. Katika mazingira haya, ridhaa ya muathirika haipo kabisa. Waandishi wa Itifaki wanaonekana kuelewa kwamba wasafirishaji wataona ni rahisi kuhalalisha matendo yao kwa kudai kwamba muathirika ameridhia tendo hilo. Njia hii ya kuepuka hukumu inafungwa kwa ibara ya 3(b), inayotupilia mbali utetezi wa ridhaa ya muathirika pale ambapo msafirishaji ametumia njia yoyote kati ya njia zilizoorodheshwa kwenye aya iliyotangulia.

Iwe kwa kurubuniwa au kulazimishwa, mara muathirika anaposailiwa, usafirishaji haramu unajumuisha uvumilivu wa muathirika kuendelea kuwa katika unyonyaji. Mtu anaweza kushangaa kwa nini waathirika wanaopata mateso sana wakiwa kwenye mikono ya wasafirishaji wanashindwa kutoroka au kutafuta msaada. Mara nyingi, hii ni kwa sababu wasafirishaji wanawadhibiti. Inaeleweka waathirika wengi hupinga na hujaribu kuepuka masharti wanayowekewa na wasafirishaji. Ukinzani mara nyingi unazimishwa na ukatili na vitisho kuanzia mwanzo. Baada ya hapo msafirishaji hutumia njia nyingi ili kuhakikisha kuwa anamdhibiti muathirika na anaendelea kubaki katika unyonyaji. Baadhi ya njia kuu za matumizi ya nguvu na udhibiti zinazotumika zinajumuisha:

**Kutengwa:** Kwa kawaida muathirika hutengwa kutoka kwenye mazingira aliyoyazoea na misaada husika mara tu anapoondoka kwenye nchi yake au eneo lake la asili. Huwekwa kwenye mazingira ambayo hafahamu lugha, tamaduni au jiografia na hulazimika kutegemea matakwa ya msafirishaji ili kuendelea kuishi. Pamoja na hayo, wasafirishaji pia huwafungia waathirika kwenye vyumba binafsi mara tu baada ya kufika eneo la mwisho na huhakikisha muathirika hana mawasiliano na mtu yeyote. Mara nyingi sharti hili huambatana na kunyimwa chakula, upatikanaji wa aina yeyote ya mawasiliano na ulimwengu wa nje au mtu mwingine yeyote ambaye anaweza kuwa kwenye mazingira hayo. Lengo ni kupata uhakika kuwa muathirika atafuata matakwa yote kwa kuwa hana msaada wowote. Kutengwa kunaweza kuendelea hata baada ya muathirika kufuata matakwa yote ya msafirishaji ili kuhakikisha kwamba hakuna mbinu za kutoroka zinazotengenezwa au msaada wowote unapatikana.

**Matumizi ya nguvu (kifungu cha 4 (1)(g)(i)** Ingawa mara nyingi mchakato mzima wa usafirishaji haramu wa binadamu unakuwa umejaa ukatili, matendo fulani ya matumizi ya nguvu yanastahili kutiliwa mkazo/kupewa kipaumbele. Unyanyasaji wa kimwili, kihisia, kimaneno na kingono kwa muathirika mpya aliosailiwa kwa kawaida hufanywa ili kupeleka ujumbe kwamba muathirika huyo yuko chini ya mikono ya msafirishaji. Kwenye kesi nyingi za usafirishaji haramu wa binadamu kwa lengo la unyonyaji wa kingono, muathirika hubakwa mara kadhaa na mwanaume / wanaume na hupigwa vibaya mpaka akubali kushiriki kwenye biashara ya ngono. Wakati wa hatua ya unyonyaji, vipigo hutolewa kwa mwathirika kama njia ya adhabu pale ambapo 'anakiuka sheria' au anaonyesha tabia isiyokubalika kama kushindwa kumridhisha mteja.

**Kushikiliwa kwa nyaraka (kifungu cha 5(2)(f):** Mara nyingi hii hutokea kwa kesi za usafirishaji haramu wa binadamu wa kuvuka mipaka ya nchi. Nyaraka za kusafiria na nyaraka zingine za utambuzi haswa pasipoti ni ushahidi rasmi wa kumtambulisha muathirika. Mara nyingi pasipoti hushikiliwa na wasafirishaji wakati wa hatua ya kati/kupita (transit) na hutolewa tu pale ambapo inahitajika wakati wa kuvuka mipaka ya kimataifa. Mara nyingi waathirika hushawishiwa kukabidhi hati zao za kusafiria ili kuhifadhiwa au kutunziwa wakati wa safari na hata baada ya kufika. Pale ambapo hati za kusafiria zinashikiliwa na msafirishaji, hutumika kama njia ya kumfanya muathirika asitoroke. Sio kwamba tu muathirika atapoteza utambulisho wake lakini pia atakuwa kwenye hatari ya kukamatwa na kufukuzwa na uhamiaji kama atakutwa hana nyaraka. Kwenye kesi nyingi, wasafirishaji hutoa ujumbe huu kwa waathirika ili kuwaonya wasifanye mawasiliano na maafisa au kutafuta njia ya kutoka kwenye kifungo/ unyonyaji.

**Madawa ya kulevya:** Waathirika hupewa madawa ya kulevya na wasafirishaji ili kuhakikisha kwamba hawakimbii/hawatoroki. Ili kuendelea kupata madawa ya kulevya na kuhakikisha kwamba hawayakosi, inawalazimu waathirika waendelee kufanya kazi kwa bidii na kuwasilisha mapato yao ili kupatiwa madawa hayo.

**Vitisho:** Hutolewa kwa aina mbalimbali ya matukio. Unyanyasaji wa kimwili, kijinsia, kihisia na matumizi ya matusi kwa mwathirika hutumika kama njia ya kutuma ujumbe kwa waathirika wengine kwamba hayo yatawapata kama hawatafuata maagizo/masharti yaliyowekwa. Baadhi ya wasafirishaji wanatumia mfumo wa 'kugawa na kutawala' na wanahamasisha waathirika wengine walifahamu hilo, na hivyo inakuwa vigumu sana kwa waathirika kuaminiana na inapelekea wao kuona kwamba msafirishaji ni

'rafiki' pekee wa kuaminika. Kwa upande mwingine, wasafirishaji hutoa vitisho na wakati mwingine hudhuru ndugu wa karibu wa familia na wapendwa wa waathirika. Ni muhimu kutambua kwamba, kwenye kesi nyingi muathirika huwa anamjua msafirishaji (k.m. mpenzi wa kiume) na wakati kwa wasafirishaji wengine, muathirika anatakiwa kutoa maelezo kuhusu familia yake, aidha kwenye hatua ya usaili au mara tu baada ya kufika katika eneo la mwisho, wakati akiwa katika hali ya kuchanganyikiwa. Sehemu ya maelezo hayo hutumika kwa urahisi hapo baadae dhidi ya muathirika ili kumkatisha tamaa kama ana mpango wowote wa kutoroka au anaonyesha upinzani wa kufuata maelekezo.

**Kuweka Rehani (kifungu cha 4 (1)):** Hii ni njia pekee ya udhibiti ambayo siyo rahisi kuelezea bila ya kurudi nyuma kwenye mchakato mzima wa usafirishaji haramu wa binadamu. Kwa kawaida waathirika walengwa hurubuniwa kwa ahadi za kupatiwa kazi zenye ujira mkubwa mara nyingi zikiambatana na maelezo kuwa kuna gharama za kulipia. Hizi ni pamoja na gharama za usafiri, malazi na chakula cha njiani kuelekea eneo la mwisho. Wakati mwingine msafirishaji au wakala wake atahitaji kupewa ujira wa kazi aliyoifanya, na hayo yote hufanya maelezo ya wasafirishaji kuonekana ya kuaminika zaidi. Waathirika wengi wanaweza kufanikiwa kupata fedha kupitia mauzo ya mali zao au mikopo, lakini mara nyingi huwa hazitoshi. Msafirishaji huchukua nafasi hii kumueleza mlengwa kwamba atalipia gharama zote lakini zitarudishwa hapo baadae kupitia mapato ya kazi. Ni ahadi isiokatalika ambayo inaweza kuwekwa kwa maandishi, na huu ndio mwanzo wa mahusiano ya mdai-mdaiwa. Wengine hawaelewi kwamba hii si kawaida mpaka pale wanapofika kwenye eneo lao la mwisho na kuambiwa kwamba msafirishaji ameingia gharama za kuwasafirisha ambazo mara nyingi zinakuwa zimeongezwa na watatakiwa kufanya kazi chini ya masharti yaliyowekwa ili kupata uhuru wao. Mara nyingi deni hilo hushindikana kulipwa maana msafirishaji hutafuta sababu za kuendelea kuongeza deni hilo. Hii hutokea pale ambapo muathirika hupewa faini kwa utovu wa nidhamu, uchelewaji au kutohudhuria kazi iwe kwa sababu ya ugonjwa au sababu nyingine. Waathirika wengine wanatakiwa kuwalipa wasafirishaji gharama za chakula, malazi, mavazi na mapambo. Lengo ni kuendelea kumuweka muathirika katika mzunguko wa deni la kudumu mpaka pale atakapokuwa hana 'manufaa' au atauzwa kwa msafirishaji mwingine ambaye atarudia mchakato ule ule wa unyonyaji.

**Uchawi:** Aina hii ya udhibiti inaripotiwa kuhusishwa na mitandao ya usafirishaji haramu wa binadamu ya Afrika Magharibi, hasa Nigeria. Taarifa za mwanzo zinatoa pendekezo kwamba uchawi ama mazingaombwe ya watu weusi yalitumika kuwaogopesha na kuendelea kuwadhibiti waathirika. Mganga wa jadi huchukua vitu binafsi kutoka kwa mwanamke aliyesailiwa kama vile kucha, vifungu vya nywele au matone ya damu ya hedhi. Tambiko hufanyika ambapo mahusiano kati ya msafirishaji na muathirika huimarishwa. Msafirishaji huandaa safari kwa makubaliano ya kiasi fulani cha malipo (kwa kawaida kiasi kikubwa cha fedha) na msafirishwaji hukubali kuheshimu makubaliano na kulipa deni. Nguvu ya uchawi hutumika kuwaadhibu wale wote ambao wataenda kinyume na makubaliano. Upatikanaji wa vitu binafsi wakati wa kuvamia madanguro katika baadhi ya sehemu za Ulaya inatoa kichocheo cha kuamini kwamba muathirika hulazimishwa kufanyiwa ibada za matambiko na msafirishaji ambapo baadae vile vitu binafsi hutolewa na kuonyeshwa kwa waathirika kwa njia za vitisho. Muathirika hutishiwa kwamba pale atakapotoroka kwa mnyonyaji, basi vitu hivyo vitatumika kumtafuta na kumsababishia madhara kupitia njia za uchawi. Hatahivyo, taarifa za hivi karibuni zinaonyesha kwamba matambiko hayo ni sherehe za baraka ambapo mganga hutakiwa kuomba mema kwa ajili ya safari hiyo. Inasemekana sherehe zenye madhumuni sawa na hayo hufanyika pia kwenye makanisa pale ambapo msafiri ni mkristo. Kwa upande mwingine, haileti tofauti yeyote (kwa maana wasafirishaji huharibu mpango mzima na kuutumia kwa lengo la udhibiti), hii ina changamoto kwa waganga wa jadi ambao wanaweza kuwajibika kwa kuhusishwa na kosa la usafirishaji haramu wa binadamu.

### 3.5.2 Aina za Unyonyaji

Aina za unyonyaji zilizoainishwa kwenye sheria zinaweza kugawanywa kwenye makundi matatu na zinaweza kuwa na mwingiliano: Unyonyaji wa kingono, Unyonyaji wa kufanyishwa kazi na kuondolewa viungo vya mwili. (Angalia ufafanuzi wa unyonyaji kwenye sehemu ya 1, kifungu cha 3, cha sheria).

**Unyonyaji wa kingono:** Unyonyaji wa kingono unaweza kuhusisha umalaya wa kulazimisha au ndoa za kulazimisha, matumizi ya machapisho ya ngono au maonyesho ya matendo mengine ya ngono kama kucheza mziki kwa kutia ashki. Aina hii ya unyonyaji hutokea kwenye mitaa, madanguro, baa, nyumba binafsi, mabafu ya mvuke na sehemu za kukanda viungo. Mambo hayo mawili ya mwisho yanaonekana kufanana na madanguro maana pia hutoa huduma za kingono. Unyonyaji wa kingono kwa wanawake umetangazwa na kufanyiwa utafiti sana katika suala zima la usafirishaji haramu wa binadamu, kiasi kwamba wakati fulani iliaminika ni aina pekee ya usafirishaji haramu wa binadamu. Utafiti zaidi umeonyesha sio tu uwepo wa aina nyingine za unyonyaji lakini pia imedhihirisha ukweli kwamba wanaume na wavulana husafirishwa kwa lengo la unyonyaji wa kingono. (Angalia sehemu ya 1, kifungu cha 3, cha sheria kwa ajili ya ufafanuzi wa 'unyonyaji wa kingono').

**Unyonyaji wa kufanyishwa kazi:** Kinyume na unyonyaji wa kingono, inaonekana kuwa wanaume na wavulana wako kwenye hatari zaidi ya kukabiliwa na unyonyaji kwa lengo la kufanyishwa kazi. Aina hii ya unyonyaji inaweza kutokea kwenye viwanda, mashamba, migodi, uvuvi na kazi za ujenzi. Kuna taarifa kuwa wavulana husafirishwa kwa lengo la kushiriki mashindano ya ngamia haswa kwenye nchi za Mashariki ya Kati. Mara nyingi wasichana husafirishwa kwa lengo la kufanyishwa kazi za ndani. Pia kuna taarifa kwamba vijana wadogo husafirishwa kwa lengo la kushirikishwa kama ombaomba wa mitaani na kwenye shughuli za uhalifu kama wabebaji wa madawa ya kulevya na waporaji wa mitaani. (Angalia ufafanuzi wa unyonyaji katika sehemu ya 1, kifungu cha 3, cha sheria).

**Kuondolewa kwa viungo vya mwili:** Usafirishaji haramu wa binadamu kwa lengo la kuondolewa viungo vya mwili umeelezewa kwenye Itifaki. Uingizwaji wa aina hii ya unyonyaji kwenye Itifaki ya Palermo una nia ya kujumuisha mambo fulani ambapo mtu hunyonywa kwa lengo la msafirishaji kujipatia faida kwenye 'soko la viungo' na pia pale ambapo mtu anasafirishwa kwa lengo la kuondolewa viungo na/au sehemu ya mwili kwa ajili ya maswala ya ushirikina/uchawi na dawa za kienyeji.

Uondolewaji wa viungo vya mwili ni nyongeza ya kipekee iliyoko kwenye vipengele vya Itifaki. Nyongeza hii iliwekwa sababu ya ongezeko la mashaka/wasiwasi juu ya baadhi ya wataalamu wa afya ambao walijipatia soko lenye faida kubwa kwa ajili ya upandikizaji wa viungo vya binadamu mnamo miaka ya 1990. Kumekuwa na majadiliano mengi iwapo istilahi ya 'viungo' ihusishe sehemu za mwili kama damu, vidole na ngozi. Kama inavyotarajiwa, kwa kawaida usafirishaji haramu wa binadamu kwa lengo la kuondolewa viungo vya mwili hufanyika katika sehemu za afya ambazo baada ya kufanya utambuzi wa uongo huwalevya wagonjwa na kuwaondolea viungo kwa ajili ya kuviuza. Taarifa nyingi kuhusu suala hili hulitaja kama 'kuiba figo'. (*Angalia Sehemu ya 1, Kifungu cha 3, cha Sheria, 'ufafanuzi wa unyonyaji'*).

### 3.5.3 Aina nyingine za unyonyaji

*Usafirishaji haramu wa binadamu kwa lengo la machapisho ya picha za ngono:* Wanawake, wanaume na watoto wanaweza kusafirishwa kwa ajili ya machapisho ya picha za ngono. Hii imejumuishwa kwenye sheria chini ya ufafanuzi wa "*unyonyaji wa kingono*: ukimaanisha ushirikishwaji wa mtu katika umalaya au utengenezaji wa machapisho ya ngono kunakotokana na vitisho, udanganyifu, matumizi ya nguvu, kutekwa nyara au matumizi mabaya ya mazingira magumu aliyonayo muathirika". Ingawa haijaonyeshwa wazi kwenye Itifaki, ufafanuzi wa unyonyaji pia unahusisha aina nyingine za 'unyonyaji wa kingono', kama machapisho ya ngono. Zaidi ya hayo, pia imeainishwa kwenye masuala ya watoto ndani ya Ibara ya 2(c) ya Itifaki ya nyongeza ya mkataba wa haki za watoto kuhusu uuzaji wa watoto, ukahaba wa watoto na machapisho ya picha za ngono za watoto. Ibara ya 2(c) inafafanua machapisho ya picha za ngono ya mtoto yanahusisha ''uonyeshaji wowote wa ukweli au kuigiza wa mtoto katika shughuli/vitendo vya ngono au uonyeshaji wa sehemu za siri za mtoto kwa lengo la maswala ya ngono." (*Angalia sehemu ya 1, kifungu cha 3 cha sheria kwa ajili ya ufafanuzi wa 'unyonyaji wa kingono'*).

**Ndoa za kulazimishwa/Ndoa za utotoni:** Usafirishaji haramu wa binadamu unaweza kuwepo kwa lengo la ndoa za kulazimishwa (na pia ndoa kwa lengo la kusafirishwa). Kumekuwa na kesi nyingi za wanawake na wasichana ambao wamesafirishwa ndani na nje ya nchi kwa lengo la ndoa. Ndoa ambazo zinaweza kuwa na lengo la unyonyaji ni kama vile ndoa za utotoni, ndoa za kulazimishwa, ndoa za kupangwa, ndoa za muda, ndoa kupitia mitandao ('mail order bride phenomenon') na ndoa kwa ajili ya kuzaa mtoto.

Kwenye kesi zingine, ndoa zinatumika kuwezesha/ kufanikisha usafirishaji haramu wa binadamu (Kwa mfano kujipatia nyaraka za kusafiria) au kuficha kosa la usafirishaji haramu wa binadamu (kwa mfano, pale ambapo waathirika wanalazimishwa kuolewa na wasafirishaji). Mara nyingi unyonyaji unakamilika kuwa 'ndoa za kitumwa', kama ilivyofafanuliwa kwenye mkataba wa nyongeza wa kukomesha utumwa, biashara ya utumwa na matendo yanayofanana na utumwa, ambao unaelezea kwamba unyonyaji unakamilika pale ambapo matendo yafuatayo yanatendeka:

- Mwanamke hana haki ya kukataa, anapewa ahadi au anatolewa kwa ajili ya kuolewa kwa makubaliano ya malipo ya fedha au aina nyingine ya malipo kwa wazazi, walezi, familia au mtu yeyote au kikundi; au
- Mume wa mwanamke, familia yake, au ukoo wake, wana haki ya kumhamisha mke kwenda kwa mtu mwingine kutokana na malipo/ thamani waliyopokea; au
- Mwanamke aliyefiwa na mume wake anawajibika kurithiwa na mtu mwingine.

Sekta ya kutafuta mke kwa njia ya mtandao 'mail order bride' inahusishwa na usafirishaji haramu wa binadamu ambapo mashirika ya kimataifa yanayojishughulisha na 'kuunganisha watu' yanafanyakazi kwa ajili ya kusaili waathirika, ambao hutolewa kama mabibi harusi, lakini huuzwa kwa siri kwenye unyonyaji wa kingono, ndoa za kulazimishwa (mara nyingine inahusisha umalaya wa kulazimishwa), au kushikiliwa kwenye utumwa wa kazi za nyumbani. Sekta hii haiwachunguzi wateja wa kiume na hamna njia rasmi ya kujua kama wateja hao wameshaoa na hawana historia ya uhalifu.

**Utumwa au matendo yanayofanana na utumwa:**

Je ni kwa namna gani utumwa wa kisasa unatofautiana na utumwa wa kale? Itifaki ya Palermo ilitokana na vyombo vya kisheria vya

mwanzo dhidi ya utumwa. Dhana kama ufanyishwaji kazi kwa nguvu, utumwa na matendo yanayofanana na utumwa yamefafanuliwa kwenye baadhi ya mikataba iliyopo ambapo pale inapotumika kwa mataifa husika, lazima itoe muongozo. (Angalia sehemu ya 1, kifungu cha 3 cha sheria kwa ufafanuzi wa ufanyishwaji kazi kwa nguvu na utumwa).

## 3.6 Usafirishaji Haramu wa Binadamu dhidi ya Magendo ya Binadamu

Tatizo mojawapo linalowakabili watoa huduma wa asasi za kiraia kwenye kesi zinazoweza kuwa za usafirishaji haramu wa binadamu ni jinsi ya kutambua kama wanashughulikia 'uhamiaji usio rasmi au usafirishaji haramu wa binadamu'; hatahivyo, ni lazima watoa huduma waweze kutofautisha mambo hayo mawili. Ingawa kuna mambo mengi yanayofanana katika aina hizi mbili za uhalifu, uhalifu wao ni wa tofauti. Sehemu hii inaelezea tofauti kati ya usafirishaji haramu wa binadamu na magendo ya binadamu.

**KISA MKASA 3b: Mashinji (Rejea zoezi 3c)**

*Mashinji ni mvuvi mwenye miaka 20 anayeishi kijiji cha Igombe mkoa wa Mwanza nchini Tanzania. Hivi karibuni alipata mawazo ya kuondoka nchini Tanzania na kwenda kutafuta maisha nchi za Magharibi. Ingawa ana uwezo wa kumudu maisha yake kutokana na samaki anaovua na kuuza, amegundua kwamba kuna watu wachache wa rika lake waliobaki kijijini kwake. Kwa kweli, watoto wadogo na wazee wamebaki kijijini na karibia wote wanaishi kwa kutumia fedha kutoka nje kutoka kwa wazazi au watoto wanaofanya kazi Marekani au Canada.*

*Pale Mashinji anapoomba ushauri kutoka kwa wazazi wake iwapo ajaribu kwenda ughaibuni, anagundua ingawa wazazi wake watasikitika kuondoka kwake lakini kwa upande mwingine wataona fahari ya kuwa na mtoto anayeishi Marekani. Kupitia msaada kutoka kwa baba yake, Mashinji anamhusisha 'wakala' ambaye anakubali kumsaidia kufanikisha safari yake ya Marekani kwa gharama ya dola za kimarekani 3,700. Wiki moja baadae, Mashinji anajikuta katikati ya bahari ya hindi akiwa amepanda meli ya mizigo ya Burundi ikiwa na wahamiaji wasio rasmi wa kitanzania kama 24 hivi ambao nao wanamatumaini ya kufika Marekani. Hali ndani ya chombo hicho ni ya baridi na isiyofaa. Wahamiaji hao wasio rasmi wamefungiwa kwenye behewa la kusafirishia bidhaa na wanalindwa wakati wote na warundi wenye silaha ambao hawaongei kiswahili. Wanaruhusiwa kutoka mara moja kwa wiki na kwenda kwenye kijumba cha sitahani (deck) kwa ajili ya usafi, lakini karibia kila mtu ana ugonjwa wa macho shauri ya mazingira machafu. Mashinji anaogopa na ana mawazo ya kutoroka lakini baada ya wiki kadhaa, meli inatia nanga kwenye ufukwe wa Msumbiji na wahamiaji wasio rasmi wanaambiwa watapelekwa Johannesburg ambapo watapewa hati za kusafiria ambazo zitawawezesha kupanda ndege kwenda Marekani ya Kusini na hatimaye kutoka hapo kwenda Marekani.*

*Hatahivyo, wakati wakiwa wanasubiri kwenye ghala huko Maputo, wahamiaji hao na mawakala wanashangazwa na uvamizi wa polisi, na wakiwa katika hali ya kuchanganyikiwa, Mashinji anatoroka. Anaendelea na safari mwenyewe kuelekea Magharibi mpaka pale anapokutana na dereva wa magari makubwa ya mizigo ambaye kwa ukarimu wake anamsaidia kuvuka mpaka kuelekea Swaziland huku akiwa amejificha kwenye gari. Anapofika Swaziland, police wanamkamata Mashinji na dereva kwa kosa la kuingia nchini kinyume na sheria.*

**KISA MKASA 3b: Penda (Rejea zoezi 3c)**

*Penda ni msichana wa miaka ishirini kutoka jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Bado hajaolewa, na ana watoto wawili wadogo ambao anawahudumia kupitia uuzaji wa mbogamboga. Siku moja, rafiki yake Marjani, alimueleza kuwa anaweza kumtafutia kazi ya kulea watoto huko Afrika ya Kusini, ambapo angeweza kupata kipato mara kumi ya kile anachokipata kwa mwezi. Marjani pia alimuahidi kufanya mipango yote ya safari, na kulipia safari nzima kama Penda angekubali kumrudishia gharama hizo pale atakapoanza kazi huko Afrika ya Kusini. Baada ya kuona kwamba kipato hicho kitakuwa na faida kwa familia yake, Penda anawaacha watoto wake chini ya uangalizi wa mama yake na kuanza safari yake kwa basi huku akisindikizwa na Marjani. Penda hana pasipoti ya kusafiria, lakini Marjani anamhakikishia kuwa haitaji kuwa nayo kwasababu ana marafiki kwenye mpaka. Wanavuka mpaka na kuingia Malawi bila tatizo, kama Marjani alivyosema. Ni wakati huu tu Penda atavuka mpaka kuelekekea Afrika ya Kusini huku akijua hilo.*

*Baada ya kusafiri kwa siku nzima, Marjani anamuacha Penda chini ya uangalizi wa dereva wa magari makubwa ambaye alimueleza Penda watasafiri pamoja kuelekea Afrika ya Kusini. Penda anashangaa kumuona yule dereva anampa Marjani noti za hela zilizokunjwa sababu alitegemea Marjani ndiye angemlipa yule dereva gharama za usafiri wake. Haulizi maswali yeyote kuhusu muamala huo, sababu alidhani ni hela za biashara isiyokuwa na uhusiano na safari yake.*

*Dereva anaonyesha hali ya kirafiki lakini anamuomba Penda akae nyuma ya gari ambalo limefunikwa ili kuepuka matatizo ambayo wanaweza kukumbana nayo mpakani. Kuna giza, joto kali, na kwa ujumla hali halisi nyuma ya gari sio nzuri lakini Penda anakubali sababu hana pasi ya kusafiria na anategemea ushauri na ukarimu wake. Hatahivyo, usiku ule baada ya safari ya siku nzima, yule dreva anasimamisha gari sehemu ya kificho, anafungua nyuma ya gari, na kumbaka Penda. Anasukumwa aingie kule nyuma ya gari na mlango unafungwa tena.*

*Ni safari ndefu na kukaa kwa Penda nyuma ya gari kunafikia mwisho baada ya gari kusimama uwanjani karibu na mto. Pale yule dreva wa gari kubwa anakutana na watu wanne ambao wanampatia kiasi kikubwa cha fedha. Penda anachukuliwa mpaka ng'ambo ya mto na wale watu wanne na anaambiwa yuko Afrika ya Kusini. Baada ya kusubiri kwa masaa machache chini ya mti, gari linafika na Penda anaamriwa aingie kukaa kwenye viti vya nyuma vya gari. Anawakuta wanawake wengine watano tayari wamekaa huko nyuma lakini hamna hata mmoja anayeongea. Wote wanaonekana kama wamepigwa. Penda anaogopa, haamini tena kama atapatiwa kazi aliyoahidiwa, na anapojaribu kukataa kuingia ndani ya lile gari anatishiwa na bunduki.*

*Penda pamoja na wale wanawake wengine wanapelekwa kwenye nyumba binafsi sehemu ya mjini. Katika kipindi cha wiki kadhaa, wale watu wanne wanawanyanyasa kijinsia na kimwili na hawaruhusiwi kuondoka kwenye majengo yale. Penda anaambiwa kama atatoroka, polisi watamkamata na kumuweka jela kwa kosa la kuwepo Afrika Kusini bila pasipoti, na kwamba hataweza kuwaona watoto tena. Anaambiwa tena, kama atajaribu kutoroka, watoto wake watatafutwa, wakamatwe na kuuzwa. Hatimaye, wanaume wengine wanaanza kuja kwenye nyumba ile, na Penda analazimishwa kufanya nao mapenzi na malipo yanaenda kwa wale wasafirishaji wanne. Baadae Penda anauzwa kwenye danguro ambapo analazimishwa shughuli za umalaya. Mmiliki wa danguro anachukua kipato chake.*

*Siku moja, polisi wanavamia danguro na kumkuta Penda hana nyaraka za kumuwezesha yeye kuwepo Afrika Kusini na anarudishwa kwao.*

**Magendo ya Binadamu:** Itifaki ya pili ya nyongeza ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa dhidi ya Uhalifu wa Kimataifa wa Kupangwa, ni Itifaki dhidi ya Magendo ya Binadamu kwa njia ya nchi kavu, bahari na anga (hapa inatambulika kama itifaki ya dhidi ya Magendo ya Binadamu).

Itifaki hii dhidi ya magendo ya binadamu ni muhimu kwa mtazamo wa uhamaji na usafirishaji haramu wa binadamu; inajikita katika kupambana na magendo ya binadamu, utoaji wa hati za kusafiria au vitambulisho bandia, kupata, kusaidia kupata au kumiliki hizo hati bandia au matendo yanayosaidia na kujinufaisha kutokana na uhamaji usio rasmi.

Kulingana na Itifaki ya Magendo ya Binadamu, "Magendo ya Binadamu" inamaanisha:

*"Ni kitendo cha kumsadia mtu ambaye si raia au mkazi wa kudumu kuingia nchi nyingine bila kufuata taratibu za sheria za nchi husika kwa lengo la kujinufaisha moja kwa moja au vinginevyo kifedha au faida nyingine" na Kuingia kinyume cha sheria inamaanisha "kuvuka mipaka ya nchi bila kufuata taratibu muhimu za uhamiaji za nchi unayoingia".*



**Magendo ya Binadamu Chini ya Sheria ya Tanzania:** Rejea kwenye maana katika sehemu ya kwanza ya sheria. Zingatia kwamba tafsiri ya neno magendo ya binadamu inapotosha kwa sababu imejumuishwa kwenye maana ya "unyonyaji". Sheria ya Uhamiaji haitafsiri maana ya magendo ya binadamu.

Kuna baadhi ya mambo yanayofanana kati ya magendo ya binadamu na usafirishaji haramu wa binadamu unaohusisha kuvuka mipaka ya nchi. Hivyo ni muhimu sana kufafanua mambo yanayofanana na muhimu zaidi tofauti kati ya makosa haya ya jinai.

Ingawa matendo yote yanaweza kuhusisha mtandao wa makosa ya jinai (uhalifu), na usafirishaji wa watu katika mipaka, usafirishaji haramu wa binadamu unahusisha muendelezo wa unyonyaji kwa muathirika. Kwa kesi za magendo ya binadamu, mara baada ya mhamaji kupitishwa kimagendo kwenye nchi ya mwisho na kulipa ada inayotakiwa, uhusiano wake na mfanya magendo ya binadamu unaisha na mhamaji anakua huru na wala hatakua katika mazingira ya kinyonyaji.

Kwa tukio la usafirishaji haramu wa binadamu unaohusisha uvukaji wa mipaka ya nchi, uhusiano wa msafirishwaji na msafirishaji hauishii baada ya kuvuka mpaka bali msafirishwaji huendelea kuwa katika mazingira ya kinyonyaji.

Hivyo magendo ya binadamu ni kosa dhidi ya nchi, wakati usafirishaji haramu wa binadamu ni kosa dhidi ya mtu na wakati wote unajumuisha ukiukwaji wa uhuru wa mtu. Hata hivyo ikumbukwe kwamba magendo ya binadamu mara nyingine huweza kuwa mwanzo wa unyonyaji, hivyo ni vyema kuwa makini unapopeleleza kesi za uhamiaji usio rasmi.

Zipo tofauti nyingi za muhimu kati ya usafirishaji haramu wa binadamu na magendo ya binadamu. Hizi zinajumuisha:

- **Ridhaa (Makubaliano):** Magendo ya binadamu mara nyingi yanafanyika katika mazingira ya hatari na magumu, yanahusisha wahamaji walioridhia (au waliokubali) kupitishwa kimagendo. Kwa upande mwingine waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu hawatoi ridhaa kusafirishwa, huwa wanatekwa na wasafirishaji au wanakubali kusafiri pamoja au bila msafirishaji kwa sababu tu wamedanganywa kwa kupewa ahadi za uongo za kazi na fursa ambazo hazipo katika nchi ya mwisho.

- **Unyonyaji:** Mara baada ya mhamaji kuingizwa kimagendo kwenye nchi ya mwisho na kulipa ada inayotakiwa, uhusiano wake na mfanya magendo unakwisha na mhamaji anaufurahia uhuru wake na haendelei kuwa katika mazingira ya kinyonyaji. Tofauti na mhamaji aliyevushwa kimagendo, msafirishwaji analazimika kuendeleza uhusiano wake na msafirishaji hata baada ya kufika nchi ya mwisho. Katika uhusiano huu anadhibitiwa na kufanyiwa vitendo vya unyonyaji na anayemsafirisha na anaweza pia kuuzwa kwa wasafirishaji wengine watakaoendelea kumfanyia vitendo vya unyonyaji.

- **Jinsi Fedha zinavyopatikana:** Wasafirishaji wanajipatia fedha kwa kuwanyonya watu (mara nyingi kwa njia ya umalaya au kufanyisha kazi kwa nguvu) katika nchi ya mwisho, ambapo wafanya magendo ya binadamu wanajipatia fedha kwa kuwatoza ada wahamaji kama mbadala wa kuwasaidia wavuke mipaka ya nchi kwa njia isiyo rasmi.

- **Kuvuka mipaka:** Usafirishaji haramu wa binadamu waweza tokea ndani ya nchi (usafirishaji wa ndani) au nje ya mipaka ya nchi (usafirishaji wa kimataifa). Kwa maneno mengine mtu anaweza akasafirishwa ndani ya nchi au kwenda nje ya nchi (wakati mwingine kupitia nchi jirani) kwa lengo la unyonyaji. Usafirishaji wa ndani unaweza kutokea bila muathirika kusafirishwa. Hata hivyo mtu hawezi kusafirishwa kimagendo ndani ya nchi moja; magendo ya binadamu wakati wote yanahusisha kuvuka mipaka ya nchi kimataifa bila kufuata utaratibu wa sheria. Kwa kuongezea wasafirishwaji wanaweza kuvuka mipaka ya

nchi kwa njia rasmi ama njia zisizo rasmi. **Kesi zinazoingiliana:** Baada ya kuvushwa kwenye mipaka ya nchi kimagendo wahamaji wasio rasmi baadae wanaweza kudanganywa au kulazimishwa kuingia kwenye mazingira ya kinyonyaji na kuwafanya wawe waathirika wa usafirishwaji haramu wa binadamu. Mara nyingi ni vigumu kwa maafisa wanaotekeleza sheria na wasaidizi wa waathirika kugundua kama mazingira hayo ni ya kesi ya magendo ya binadamu au usafirishaji haramu wa binadamu, na wahamaji wenyewe wanaweza wasijue hatari iliyo mbele yao.

- Zaidi ya hayo, waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu hukutana na mamlaka husika si kama waathirika lakini kama watuhumiwa, kwasababu hulazimishwa kushiriki katika matukio mbalimbali ya uhalifu (kubeba madawa ya kulevya, kazi isiyo halali au ukahaba).
- Mwanzoni mamlaka zinaweza kupata shida kutofautisha wahamiaji wasio rasmi ambao wamevushwa kimagendo na waathirika ambao wamesafirishwa. Kulingana na mamlaka na mazingira, ulinzi na huduma ya misaada kwa waathirika vinaweza kupatikana.
- Nchini Tanzania, utambuzi, ulinzi na msaada kwa waathirika unaongozwa na vifungu vya sehemu ya III na IV ya sheria ya kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu ambayo inatoa huduma mbalimbali kwa watu ambao wametambuliwa kuwa ni waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu.

**KISA MKASA 3e:**

**Yolande (Rejea Zoezi 3c, muendelezo)**

*Yolande, ni mwanamke mwenye miaka 31 anayetoka Jamuhuri ya Muungano Tanzania. Ni muuza matunda wa jijini Dar-es-salaam na siku moja kijana aliyejitambuisha kwa jina la George toka nchi jirani alimfuata. George alimweleza habari ya kutaka kumsaidia na kumpatia kazi kwenye duka la nguo nchini Afrika Kusini. Yolande alionyesha kukataa lakini George aliendelea kumshawishi na baada ya siku kadhaa Yolande alikubali kwenda na George Afrika Kusini. George alimuahidi kufanya matayarisho ya kila kitu; na Jumamosi moja walivuka mpaka wakiwa na gari binafsi na kuingia Malawi. Wakiwa Lilongwe, George alichukua chumba cha hoteli na alikaa na Yolande kwa siku kadhaa. Katika kipindi hicho walifanya mapenzi.*

*Baada ya kama wiki moja pale hotelini, George alimwambia Yolande kwamba ana jambo la kibiashara anahitaji kulishughulikia na angeondoka kwa siku kadhaa, lakini angerudi kuja kumchukua na kumpeleka Afrika Kusini. Masaa machache baada ya George kuondoka, mwanaume mmoja alibisha hodi kwenye mlango wa chumba cha Yolande na akamwambia kuwa yeye ni rafiki wa George na alimwambia atakaa kwenye kile chumba mpaka George arudi. Kwasababu George ndiye aliyepangisha kile chumba, Yolande hakuwa na sababu ya kukataa na sababu pia chumba kilikuwa na vitanda viwili basi hilo lilimfanya awe na amani. Usiku huo yule mwanaume alimwomba Yolande wafanye mapenzi na alipokataa, alimbaka. Siku iliyofuata, mwanaume mwingine tena alikuja na kumbaka. Ndani ya siku tano mfululizo, Yolande alikuwa amebakwa na wanaume tofauti wasiopungua kumi. Wale wanaume walikuwa hawajuani vizuri na Yolande alishindwa kutoroka sababu kila wakati kulikuwa na mtu kule chumbani.*

*Siku ya sita, meneja wa ile hoteli aligonga kwenye mlango wa kile chumba, na kumwambia mwanaume aliyekuwa na Yolande kuwa George alilipia kile chumba kwa siku tatu tu na kama wangetaka kupangisha tena kile chumba walitakiwa walipe malipo ya awali kwa ajili ya wiki nzima. Yule mwanaume aliondoka mara baada ya mazungumzo na kumwacha Yolande akiwa peke yake kwa mara ya kwanza. Mara ya kwanza alidhani ya kuwa ameenda mapokezi kulipia bili lakini baada ya masaa matatu kupita bila ya yule mwanaume kurudi ndipo Yolande nae akaamua kuondoka. Yolande hakumwona George tena na baadae aligundua kuwa George alikuwa amewapangishia vyumba wanawake wengine wanne kwenye ile ile hoteli. Hao wanawake walipatwa na matatizo kama ya kwake.*

**KISA MKASA 3f:**

**Mariam (Rejea Zeoezi 3c muendelezo)**

*Mariam ni msichana mzuri wa kitanzania mwenye umri wa miaka 16 aliyekatisha masomo yake akiwa darasa la saba. Ana kipaji maalum cha ususi wa nywele na wasichana wengi wa kijijini huenda kusuka kwake mitindo mbalimbali ya nywele. Kwasababu ya uzuri wake, wavulana wengi wa kijijini waliwaomba wazazi wake waruhusiwe kumuoa Mariam. Wazazi wa Mariam hawakukubaliana na hilo sababu walitaka mwanaume kutoka mjini amuoe binti yao.*

*Shangazi yake Mariam anakaa Dar es salaam na anamiliki saluni ya kutengeneza nywele. Mara nyingi anasafiri kwenda Kyela kumsalimia dada yake (mama yake Mariam). Mariam anashauriwa aende mjini Dar es salaam akafanye kazi kwenye saluni ya shangazi yake kwa malipo ya shilingi 300,000 kwa mwezi. Familia yake ilifurahi sana sababu Mariam atakaa kwa shangazi yake na atafanikiwa kuweka akiba ya fedha atakazopata na kuzituma nyumbani kwa mama yake.*

*Wazazi wa Mariam wanawashirikisha majirani habari hizo njema. Shangazi yake anaahidi pia atamuandikisha Mariam kwenye masomo ya jioni ili aweze kumalizia kidato cha nne. Shauri ya furaha, Mariam alikosa usingizi siku ile. Aliendelea kutafakari maisha mazuri katika jiji la Dar- es- salaam na nafasi ya kuendelea na masomo yake. Alimuomba Mungu mara kadhaa ambariki shangazi yake kwa ukarimu wake. Mariam na shangazi yake waliondoka asubuhi na mapema kuelekea Dar-es-salaam. Njiani shangazi alimuusia Mariam jinsi ya kuishi kwa kujiheshimu jijini Dar es salaam. Pia alimuambia kwamba, kama atajiheshimu, atamuunganisha na watu maarufu na ataishi maisha mazuri.*

*Mariam na shangazi yake waliwasili jioni jijini Dar-es-salaam na walielekea Mikocheni ambako shangazi yake aliishi. Nyumba ilikuwa na vyumba vitatu na pembezoni kulikuwa na saluni pamoja na chumba kingine kilitumika kama baa. Siku iliyofuata Mariam alionyeshwa sehemu ambapo angefanyia kazi. Siku ya kwanza ilikuwa nzuri kwa Mariam. Siku chache baadae, Mariam akiwa amemaliza kazi na anataka kuelekea nyumbani, mmoja wa wateja wa baa aligundua uzuri wa Mariam na akamueleza shangazi yake kwamba angempatia mshahara wake wote kama angemruhusu awe na mahusiano ya kimapenzi na Mariam. Shangazi yake Mariam alifurahi sana na akamwita aje kusaidia shughuli za baa. Baadae shangazi yake alimwambia aanze kuwahudumia wageni waliokuwa wamekaa na yule mtu. Mariam alikumbushwa na shangazi yake yale mazungumzo ya kwenye gari kuwa awe mwangalifu na watu anaojichanganya nao. Mariam alimwambia shangazi yake kuwa asingeweza kufanya kile ambacho wateja walimtaka akifanye, na hili lilimkasirisha sana shangazi yake. Mariam aliambiwa kwamba maadam anaishi kwenye nyumba ya shangazi yake, basi ni lazima alale na mtu yeyote atakayeambiwa alale naye la sivyo angeadhibiwa. Mariam alinyimwa chakula kila mara alipokataa kuwahudumia wateja wa shangazi yake na aliacha kumlipia ada ya shule. Afya ya Mariam ilianza kuporomoka na alinyimwa huduma za afya. Alitaka kurudi nyumbani lakini hakuwa na fedha sababu shangazi yake alikuwa anamtunzia fedha zote alizozipata.*

**KISA MKASA 3g:**

**Nora (Rejea Zoezi 3c muendelezo)**

*Nora ni msichana mwenye umri wa miaka 24 anayejishughulisha na ukahaba jijini Arusha nchini Tanzania. Biashara ilishuka sana na Nora alidhani ya kwamba ni sababu umri umesogea na wasichana wadogo walioko kwenye biashara ya ukahaba walikuwa wanamwibia wateja wake. Alisikia fununu kwamba wanawake wengi makahaba wa kitanzania wanapata kipato kikubwa nje ya nchi, na wakala anapomueleza kuhusu kufanya kazi Afrika Kusini, anakubali mara moja.*

*Wakala anatoa msaada mkubwa kwa Nora. Anamlipia Nora nauli ya ndege ya kwenda Johannesburg kiasi cha dola za kimarekani 700 na anatayarisha mtu wa kumpokea uwanja wa ndege atakapofika. Pale ambapo Nora anamueleza kuwa hajui kuongea lugha ya Kiingereza, wakala anamuhakikishia kuwa wanawake wengi wa kitanzania wanafika Afrika Kusini wakiwa hawajui kuongea lugha ya Kiingereza, lakini hujifunza haraka, na wanaishia kuolewa na wanaume matajiri. Nora anaridhika na majibu anayopewa. Anatambua kwamba hawezi kuwa kahaba milele, na atatafuta njia ya kutengeneza maisha yake ya baadae. Anakubali kumrudishia wakala zile dola 700 za kimarekani kwa ajili ya juhudi zake na gharama alizotumia na anamhakikishia kuwa atamrudishia fedha hizo katika kipindi cha mwezi mmoja.*

*Nora anasafiri kuelekea Uwanja wa Kimataifa wa Johannesburg na hakupata tatizo lolote sababu hahitaji visa yeyote kuingia Afrika Kusini. Nora hakujua kwamba anaruhusiwa kukaa nchini kwa muda wa miezi mitatu tu na anashangaa atawezaje kupata fedha za kuweza kumlipa yule wakala ndani ya kipindi cha miezi mitatu. Kama ilivyopangwa na wakala wa Tanzania, mwanaume aitwaye Charles alimsubiri Nora uwanja wa ndege. Charles ni raia wa Afrika Kusini na haongei kiswahili lakini aliweza kumtambua Nora, na akampeleka kwenye nyumba binafsi iliyopo eneo la kitajiri jijini Johannesburg ambapo anapumzika baada ya safari ndefu.*

*Siku iliyofuata kwenye majira ya saa nne asubuhi, Charles alimsindikiza Nora kwenye danguro ambapo alianza kufanya kazi ili aweze kulipia deni lake. Kazi hiyo ilikuwa kama Nora alivyotegemea. Alifanya kazi kwa masaa mengi, mara nyingi kuanzia saa 4 asubuhi na alimaliza saa 11 au 12 asubuhi ya siku inayofuata, na mara nyingine ilibidi asafiri na wanawake wenzie kwenda kwenye miji mikubwa kwa ajili ya ukahaba.*

*Pindi muda wake wa kuishi Afrika Kusini ulipokaribia kuisha, na akiwa bado hajamaliza kulipia deni lake la mwanzo, Nora anaamua kuendelea kufanya kazi Afrika Kusini bila visa kwani alikuwa hajapata hela yoyote ya kujikimu yeye mwenyewe. Ili kuondoa usumbufu na polisi, Charles na mmiliki wa danguro wanafanya utaratibu wa kumuozesha Nora kwa mmoja wa wateja wake wa Afrika Kusini ili kumuwezesha kuendelea kubaki nchini. Yule mteja anakubali, na anamlipa Charles kiasi cha dola 7000 za kimarekani. Mteja huyo ni tajiri sana na Nora anafurahi kuolewa naye, huku akiamini kuwa ataweza kuacha kazi ya ukahaba. Hatahivyo, baada ya harusi, Nora anagundua kwamba bado anatakiwa kuendelea na biashara ya ukahaba ili kuweza kulipa kulipa deni la dola 7,000 za kimarekani ambazo mteja/mume wake alimlipa Charles.*

*Kwa shingo upande, Nora anakubali mpango huo mpya kwani alikuwa kapanga masaa ya kufanya kazi zake na alikuwa anaweza kupata muda wa kupumzika pale anapotaka. Mume wake alimtunza vizuri, na alikuwa na uhuru wa kwenda atakako. Pia, alikuwa na akaunti yake mwenyewe ya benki ambayo alitunza hela zake japokuwa ilibidi amlipe mume wake kiasi fulani cha hela kila mwezi. Pindi deni la dola 7000 za kimarekani litakapomalizika, Nora ataacha kuwa kahaba na ataendelea kuishi Afrika Kusini.*

**Zoezi 3d – Kuelewa usafirishaji haramu wa watoto**

**Lengo:** Kuwezesha washiriki kubaini tofauti kati ya kesi za usafirishaji haramu wa watu wazima na watoto

**Muda:** Dakika 50

**Muwezeshaji:**

- Gawanya washiriki kwenye makundi ya watu kati ya wanne au watano.
- Kila kundi lichague mwenyekiti na msemaji.
- Waombe washiriki wasome kesi ya Andrew na kujibu maswali yatakayofuata hapo chini.
- Toa dakika 25 za majadiliano.

**Maswali yanayohusu kesi ya Andrew:**

- Je, kesi hii ni ya usafirishaji haramu wa binadamu kama inavyofafanuliwa kwenye Sehemu I ya Sheria? Elezea jibu lako
- Kisheria ni nani awajibishwe kwa suala la Andrew? Zingatia kila mshtakiwa na ujadili ni kipengele gani kitatumika kwenye sehemu I ya sheria.
- Je umri wa Andrew unaathiri vipi jibu lako?

**Mwezeshaji:** Atahitimisha mjadala kwa kuonyesha ukosefu wa "njia" kwenye ufafanuzi wa itifaki ya Palermo kuhusu usafirishaji haramu wa watoto na kuoanisha na suala la ridhaa. Hakikisha kwamba kuna uelewa wa maana ya mtoto na uhusiano uliopo wa ukosefu wa uwezo wa kutoa ridhaa.

## 3.7. Watoto kama kundi maalum

**KISA MKASA 3h:**

**Andrew (Rejea Zoezi 3d)**

*Andrew ni mvulana mwenye miaka 12 kutoka kijiji kimoja nchini Tanzania. Mama yake, Sophia, ni mjane mwenye watoto 6 wa kuwatunza na sababu ya ukame katika kijiji hicho, utafutaji wa chakula cha kuwalisha watoto wake wote inakuwa ni tatizo kubwa sana kwake. Andrew akiwa kama kijana mkubwa kwenye familia hiyo, anajiona ana wajibu kwa wadogo zake na angependa kumsaidia mama yake kuwatunza wadogo zake. Kabla ukame haujaanza, mara nyingi Andrew hujishughulisha na vibarua anavyofanya kwa jirani zake lakini kwa sasa hamna aliye na hela ya kumlipa.*

*Siku moja, Sofia alikutana na mwanaume aitwaye Joshua ambaye alikuwa anatafuta vijana wakakamavu wakufanya kazi kwenye mashamba huko Kenya. Sofia alipomwambia Joshua kuwa ana kijana mwenye umri wa miaka 12 ambaye anatafuta kazi, Joshua aliahidi kumpatia Sofia kiasi cha shilingi 170,000/= kama ujira wa kazi atakayofanya Andrew, huku akiahidi kuwa atakula na kulala mahali atakapokuwa anafanyia kazi. Kwa Sofia, kiasi hicho cha fedha kilikuwa kinatosha kusaidia kuwalisha watoto wake wengine na kuwa na matumaini kwamba mtu mwingine angesaidia kumlisha Andrew, na hivyo kuwa na matumbo machache yakulisha. Sofia alikubaliana na mapatano haya.*

*Ingawa Andrew alisikitika sana kuiacha familia yake, alifurahi kwa kuwa angeweza kuisaidia familia yake kwa njia hii na hivyo yeye pamoja na Joshua na vijana wengine wanne walianza safari yao ya siku kadhaa. Mara nyingi walitembea pembezoni mwa barabara na wakati mwingine walidandia nyuma ya magari makubwa. Andrew hakuwa na kumbukumbu kama walivuka mpaka wowote, hatimaye baadae yeye pamoja na wenzake walifika eneo la shamba ambalo halikuathiriwa na ukame. Joshua aliwaongoza kando kando ya mashamba tofauti makubwa na huku akijadiliana na kupatana bei na watu aliowakuta huko. Baada ya kupokea kiasi cha shilingi milioni 1, alimuacha Andrew na mwanaume aitwaye Godfrey.*

*Godfrey aliwasimamia wafanyakazi wengi na wengine walikuwa vijana wenye umri sawa na Andrew. Alihakikisha wote wanafanya kazi kwa bidii huko mashambani huku wakianza kazi kabla jua halijachomoza na kumaliza baada ya jua kuzama. Hawakupewa malipo yeyote kwa kazi waliokuwa wakiifanya na walikuwa wakipewa chakula mara mbili kwa siku tu, asubuhi na jioni. Usiku, vijana wote walilala kwenye chumba chenye sakafu ngumu na chafu kisichokuwa na godoro wala mkeka, ingawa kila mmoja alipewa blanketi jepesi la sufi. Mara nyingi Andrew alihisi njaa na baridi na aliugua mara kwa mara.*

*Baada ya miezi mingi kupita, Andrew alichoshwa na ile hali aliokuwa anaishi na alianza kukumbuka nyumbani. Hakujua ni jinsi gani angeweza kurudi nyumbani kwenye familia yake, lakini baadae aliamua kuondoka kule shambani pasipo kumueleza mtu yeyote malengo yake ya kufanya hivyo. Muda mfupi baada ya kuondoka shambani, usiku mmoja alikamatwa na polisi.*

### 3.7.1 Maelezo ya usafirishaji haramu wa watoto

Itifaki ya Palermo inafafanua maana ya mtoto kuwa ni mtu yeyote mwenye umri chini ya miaka kumi na nane; sheria ya Tanzania ya kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu inabeba maana sawasawa na hiyo (*Angalia Sehemu I, kifungu cha 3 cha sheria, 'maana ya mtoto'*).

Ingawa vyombo mbalimbali vya kimataifa vinaamuru uwajibikaji wa nchi husika kupinga usafirishaji haramu wa watoto, Itifaki ni chombo pekee kinachofafanua maana ya mtoto. Mifano mingine maarufu ni mkataba wa umoja wa mataifa wa haki za watoto na mkataba wa Afrika wa haki na ustawi wa watoto ambayo ina vipengele vya usafirishaji haramu.

### 3.7.2 Kazi za watoto, ajira za watoto na usafirishaji haramu wa watoto

**Kazi za watoto:** zinahusisha kazi nyepesi ambazo sio hatarishi na ambazo haziingiliani na ukuaji wa watoto.

**Ajira za watoto:** zinahusisha kazi za hatari ambazo huweka haki ya mtoto ya kuishi, ulinzi na ukuaji wake kwa ujumla katika hali hatarishi.

**Usafirishaji haramu wa watoto:** Ni kitendo cha kusaili, kusafirisha, kuhamisha, kuhifadhi au kupokea mtu yeyote chini ya miaka 18 kwa lengo la unyonyaji.

### 3.7.3 Usafirishaji haramu wa watoto (aina za unyonyaji wa watoto)

Usafirishaji wa watoto wakati mwingine ni vigumu kutambulika, kwa kiasi fulani huwa ni uhalifu uliojificha na unatofautiana kulingana na mazingira. Baadhi ya aina za usafirishaji wa watoto ambazo zinasadikika kufanyika Tanzania ni pamoja na:

**Unyonyaji wa kufanyishwa kazi kwa nguvu:** Watoto wanaweza kusafirishwa kwa lengo la kufanyishwa kazi. Kwa kawaida hufanyishwa kazi kwa nguvu, kulingana na aina ya ajira au kazi bila ujira ambazo zinakiuka haki za watoto. Baadhi ya sekta ambazo watoto waliosafirishwa wanaweza kupatikana ni pamoja na: kilimo, uvuvi, kazi za majumbani na migodini;

**Unyonyaji wa kingono:** Watoto waathirika wa usafirishaji haramu kwa lengo la unyonyaji wa kingono, mara nyingi huwa wanapata maumivu yaliyokithiri ya kimwili, ukatili na unyanyasaji wa kijinsia na kisaikolojia kutoka kwa wasafirishaji na wateja. Watoto walionyonywa kingono pia wapo katika hali hatarishi ya kupata UKIMWI na magonjwa mengine yakuambukiza ya zinaa. Ingawa usafirishaji haramu kwa lengo la unyonyaji wa kingono unawaathiri sana wanawake, usafirishwaji wa wavulana wadogo kwa lengo la ukahaba unaendelea kukithiri na haupaswi kufumbiwa macho;

**Ndoa za kulazimishwa/Ndoa za utotoni:** Aina hii ya usafirishaji haramu wa binadamu inatokea zaidi kwa wasichana. Inaweza kutokea kwa sababu za kiuchumi zaidi (kwa familia maskini) au kutokana na ndoa zinazoamuliwa na familia kati ya wanandoa watarajiwa kulingana na tamaduni za makabila fulani. Katika baadhi ya maeneo, kumekuwa na ongezeko la uhitaji wa wasichana wadogo ambao ni bikira haswa kwenye sehemu ambazo kasi ya maambukizi ya UKIMWI ni kubwa.

# SURA YA 4

## UTAMBUZI WA WAATHIRIKA

### 4.1 Utangulizi wa Sura

Sura hii inaelezea kanuni za utambuzi na mahojiano kwa waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu na pia njia za kuhakikisha wanalindwa ipasavyo. Waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu wana mahitaji makubwa ya afya ya kimwili na kisaikolojia ambayo yanahitaji kushughulikiwa kwa haraka. Dhumuni la msingi la utambuzi wa muathirika ni kuhakikisha kwamba hatua stahiki zinachukuliwa ili kumsaidia. Hata hivyo utambuzi wa muathirika unaweza kusaidia pia upelelezi madhubuti na kuwafungulia mashtaka wasafirishaji.

**Malengo:**

- Kutambua umuhimu wa utambuzi wa waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu na kanuni za msingi zinazotumika kuwasaidia waathirika hao;
- Kutambua viashiria vikuu vinavyotumika kuwatambua waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu;
- Kuelewa mchakato mzima wa mahojiano na waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu.

**Matokeo yatarajiwayo:**

Washiriki watapata ujuzi wa kutambua waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu na mwisho wa moduli hii:

- Wataelewa umuhimu wa kuwatambua waathirika kwa usahihi;
- Watatambua kanuni za msingi na hatua zinazotumika katika utambuzi na ulinzi wa muathirika;
- Wataweza kutambua viashiria vya msingi vinavyotumika katika kuwatambua waathirika;
- Watapata uelewa kuhusu mchakato mzima na mbinu zinazotumika kuwahoji waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu;
- Watafahamu zaidi vipengele vya Sehemu ya III na IV vya Sheria ya Kupambana na Usafirishaji Haramu wa Binadamu (Na. 6 ya mwaka 2008) kama vilivyo muhimu kwa utambuzi na usaidizi kwa waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu.

**Vitendea kazi:** Kesi na maswali kwenye kitabu hiki, bango kitita, kalamu ya wino mzito, Sehemu III na IV ya sheria ya kupambana na ushafirishaji haramu wa binadamu Na. 6 ya mwaka 2008

**Muda:** Masaa 5 na dakika 30

**Marejeo muhimu:**

Machapisho ya IOM na Umoja wa Mataifa

- The Anti-Trafficking in Persons Act No. 6 of 2008;
- The IOM Counter Trafficking Handbook for Law Enforcement Officers in Southern Africa, 2005;
- The IOM Counter Trafficking Training Modules Victim Identification & Interviewing Techniques, 2006;
- The IOM Handbook on Direct Assistance for Victims of Trafficking, 2007.
- Anti-Trafficking Training for Frontline Law Enforcement Officers Training Guide ICMPD, 2006;
- The United Nations Global initiative to Fight Human Trafficking, UN-GIFT B.P.:006, The Vienna Forum to Fight Human Trafficking, 13-15 February 2008, Austria Center Vienna, Background Paper, 006 Workshop: Criminal Justice Responses to Human Trafficking, 2008.

## 4.2 Umuhimu wa Utambuzi wa Waathirika

Usafirishaji haramu wa binadamu unahusisha ukiukwaji wa haki na utu wa binadamu. Kuwatambua waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu ni muhimu ili kuhakikisha wanapata ulinzi na msaada. Kama muathirika asipotambuliwa, anaweza kuchukuliwa kama mhamiaji asiye rasmi au akaachwa bila kupatiwa mahitaji, ulinzi au msaada stahiki ili aweze kurudi katika hali yake ya awali. Hii inaweza kuleta madhara kwa muathirika na uchunguzi wa kesi ya ushafirishaji haramu wa binadamu. Bila ulinzi na msaada, waathirika wanaweza kushindwa kujiamini na kukosa ulinzi ili waweze kushirikiana na maafisa watekelezaji wa sheria katika uchunguzi wao wa jinai.  Bila ya ushahidi na ushuhuda kutoka kwa wasafirishwaji, ni vigumu kuwafungulia mashtaka wasafirishaji.

**Msaada kwa waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu unaweza kuwa ni njia madhubuti ya kupambana na uhalifu wa kupangwa***

Watu wanaosafirishwa nje ya mipaka wanawekwa katika mazingira ya kupata taarifa za kina kwasababu huhamishwa kutoka nchi ya mwanzo kwenda nchi ya mwisho, hii inajumuisha: majina, anuani na namba za simu za watu wanojihusisha na usafirishaji haramu, magari na njia za mawasiliano zinazotumika na anuani za nyumba za makazi salama au makazi mengine ambapo unyonyaji unaendelea; na majina, maelezo ya baadhi ya waathirika na maeneo ambayo waathirika wengine bado wananyonywa. Pia wanaweza kufahamu njia za upatikanaji wa fedha haramu na sehemu ambazo vitu vingine vinapatikana. Kwahiyo, mkakati ambao unawafukuza mara moja wasafirishaji unaonekana ni sawa na kutupa vyote kwa pamoja, madawa ya kulevya na ushahidi wa polisi.

Wakati mwathirika anaweza kukubali kutoa taarifa kwa polisi ili kuepuka kufukuzwa, anaweza asiwe mwepesi kutoa taarifa ambazo zitahatarisha utambulisho wake au eneo lake kama hajashawishika na uwezo wa serikali kumlinda. Shirika la kimataifa linaloshughulikia maswala ya wahamaji (IOM) linashauri kwamba wasafirishwaji haramu wapewe msaada wa kiafya na ushauri wa kisaikolojia, pamoja na mazingira salama ili kuwasaidia waweze kurudi katika hali yao ya awali.

Wale wanaoweza kuepukana na sonona watakuwa katika nafasi nzuri ya kutoa taarifa kuhusu mitandao ya uhalifu wa kupangwa na kupata nafasi nzuri ya kupona.

Wakati inaonekana ni vizuri waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu wahamasishwe kushirikiana na uchunguzi wa polisi kuhusiana na matendo ya mitandao ya uhalifu wa kupangwa, na kwamba utoaji wa makazi ya muda ni nyenzo za kuhamasisha ushirikiano, wasafirishwaji hawataweza kuendelea kujisikia wanatishwa au kuumia kutokana na yale waliyoyapitia. Mabadiliko yoyote ya ukazi wa muda kwa ajili ya uchunguzi ni lazima yaendane na hatua za ziada kama vile msaada wa malazi, afya na ushauri wa kisaikolojia.

Kwa msaada huo, waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu hawatakuwa tu na nafasi ya kupona kwa kipindi kirefu bali wataweza kutoa taarifa za kiintelijensia kwa ajili ya uchunguzi na kufungua mashtaka.

*Inatoka kwenye chapisho la IOM (IOM Counter-Trafficking Handbook for Law Enforcement Officers in Southern Africa, Chapter 4 (2006)).

**Zoezi namba 4a: Misingi ya Utambulisho wa Muathirika**

**Lengo:** Kubaini faida za kuwatambua waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu na kanuni elekezi katika kuwasaidia waathirika hao.

**Muda**: Dakika 45

**Mwezeshaji:**

Anza kipindi hiki kwa kuwaomba washiriki watoe mawazo yao ni kwanini wanafikiri ni muhimu kuwatambua waathirika?

Unaweza kuuliza maswali yafuatayo kuongoza majadiliano:

Je ni faida gani zinazotokana na utambuzi wa mwathirika kwa:

- Waathirika?
- Maafisa wa kutekeleza sheria?
- Juhudi za kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu kwa ujumla?

Pale ambapo faida zimeainishwa, uliza maswali yafuatayo:

- Kwa kuwa na faida hizi, je ni jinsi gani watoa huduma wawahudumie waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu?
- Ni kanuni zipi zitumike kutuongoza katika kuwahudumia waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu?
- Hitimisha kipindi kwa kuelezea kwa ufupi kanuni elekezi za msingi katika kuwahudumia waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu.

## 4.3 Kanuni elekezi katika kuwahudumia waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu

Kanuni elekezi ya msingi katika kuwahudumia waathirika ni "usiwadhuru". Kwa kuongezea katika kanuni hii, watoa huduma wanatakiwa kutambua mitazamo ifuatayo wakati wakichangamana na waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu.

**Mtazamo wa haki za binadamu:** Usafirishaji haramu wa binadamu ni ukiukwaji uliokithiri wa haki za binadamu, ambao unazuia na kuharibu utu wa msafirishwaji haramu. Kwahiyo, ni muhimu mifumo ya kutoa huduma izingatie haki za binadamu. Wale ambao wanachangamana na waathirika wanatakiwa wawe na huruma na waelewe mahitaji yao kulingana na mtazamo wa waathirika. Maamuzi kuhusu muathirika yanatakiwa yatoke kwa na yazingatie 'maslahi ya muathirika'. Waathirika wana haki ya kulindwa, kuombwa ushauri na kupewa taarifa kuhusu hatua zote zinazochukuliwa kwa niaba yao.

**Waathirika wa Uhalifu**

Ikumbukwe kwamba waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu ni **waathirika wa uhalifu**; na si wahalifu.

**Mtazamo unaozingatia Uathirika:** Hatua zozote zitakazochukuliwa na mashirika yanayotoa msaada ni lazima zihakikishe kwamba muathirika ni mtu wa muhimu. Hii inahitaji muathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu:

- Asichukuliwe kama mhalifu;
- Asipewe uathirika kwa mara nyingine;
- Asipewe alama ya aibu
- Asikamatwe;
- Asinyanyapaliwe;
- Apewe msaada wote kama haki yake.

**Mtazamo wenye sura mbalimbali:** Ufahamu wa kina kuhusu usafirishaji haramu wa binadamu unahitaji kueleweka katika mchakato mzima. Kosa la usafirishaji haramu wa binadamu linaeleweka vizuri kama mjumuisho wa makosa ya jinai yaliyounganika kwa pamoja badala ya kosa moja, ni mchakato wa makosa ya jinai badala ya tukio moja la jinai ambalo linaweza kuhusisha wahalifu wengi.

Kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu kunahitaji juhudi za pamoja za vyombo mbalimbali ambavyo vimepewa dhamana ya kufanya shughuli mbalimbali, vikiwemo vyombo kama polisi, vyombo vinavyotoa huduma za kijamii, waendesha mashtaka, washauri, mashirika yasiyo ya kiserikali, n.k wote ambao wanafanya kazi mbalimbali katika mchakato mzima wa kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu.

Nchini Tanzania, wizara ya afya na ustawi wa jamii (idara ya ustawi wa jamii) na Kamati ya kitaifa ya kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu na Sekretarieti yake (chini ya wizara ya mambo ya ndani), ni vyombo vikuu vya serikali ambavyo vimepewa jukumu kubwa la kupambana na usafirishaji haramu

wa binadamu. Majukumu hayo yanaruhusu uratibu wa wadau mbalimbali ili kuhakikisha mahitaji mbalimbali ya waathirika, ikiwa ni pamoja na makazi, ushauri nasaha wa kisaikolojia, huduma ya matibabu ya kimwili na msaada wa kisheria vinafikiwa.

Wizara ya afya na ustawi wa jamii chini ya idara ya ustawi wa jamii Tanzania ina jukumu kubwa katika masuala ya kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu:

- Inatoa huduma na msaada kwa waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu kwa kushirikiana na wadau;
- Inatoa huduma za msingi na kuhakikisha kwamba haki za binadamu za waathirika zinazingatiwa, kwa kushirikiana na wadau;

Aidha, chini ya sheria ya kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu, namba 6 ya mwaka 2008, serikali:

- Ikishauriwa na kikundi kazi, itaanzisha au kuteua vituo vya ulinzi na msaada kwa waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu.

*Kamati ya kitaifa ya kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu* ina majukumu yafuatayo;

- Kuratibu shughuli za idara za serikali na vyombo vya kutekeleza sheria vilivyopewa dhamana ya kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu.
- Kutoa mapendekezo kwa ajili ya kutengeneza mpango kazi wa kitaifa wa kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu;
- Kumshauri waziri kuhusu masuala ya kisera yanayohusiana na usafirishaji haramu wa binadamu;
- Kutoa ushauri kuhusiana na uchunguzi na kufungua mashtaka ya jinai kuhusu usafirishaji haramu wa binadamu;
- Kupendekeza na kukuza mikakati ya kuzuia na kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu;
- Kushirikiana na vyombo vya serikali na mashirika yasiyokuwa ya kiserikali ili kusaidia kuwarejesha katika hali zao za awali na kuwaunganisha na familia zao waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu;
- Kujiweka sambamba na viwango vya maendeleo katika kuzuia na kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu kimataifa na kikanda;
- Kuandaa miongozo kwa ajili ya kutoa fedha kwenye mfuko; na
- Kushughulikia masuala yoyote yanayohusiana na usafirishaji haramu wa binadamu.

## 4.4 Mambo maalum ya kuzingatia

**Jinsia;** Ingawa muathirika anaweza kuwa mtu yeyote, utafiti unaonyesha kuwa idadi kubwa ya waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu, hasa wale wanaosafirishwa kwa lengo la unyoyaji wa kingono, ni wanawake. Mwitikio duni kwa waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu unaofanywa na vyombo mbalimbali unaongeza ubaguzi na unyanyasaji wa kijinsia ambao upo tayari kwenye jamii. Hivyo, kuzingatia jinsia ni jambo linalohitajika katika kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu. Hatua na taratibu zinazochukuliwa na wadau mbalimbali zizingatie haki za jinsia.

**Haki za watoto:** Utafiti umeonyesha kwamba kuna hitaji kubwa la watoto kwa ajili ya unyonyaji. Watoto wakiwa katika kundi hatarishi zaidi wamekuwa wakinyanyaswa wakati na baada ya kusafirishwa, hivyo mwitikio usio sahihi katika kuwasaidia unawaongezea madhara zaidi ambayo wamekwisha yapata. Kwahiyo, mwitikio katika kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu unatakiwa uzingatie haki za watoto.

Kanuni zifuatazo zizingatiwe wakati wa kutoa msaada kwa watoto:

- Maamuzi yanayochukuliwa yanatakiwa yazingatie maslahi bora ya mtoto;
- Mtoto apewe nafasi ya kutoa mawazo yake katika maswala yote;
- Mlezi atatakiwa kuteuliwa kutoa maamuzi kwa ajili ya ustawi wa mtoto. Sheria ya kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu inaelekeza msaada utolewe kwa ajili ya muathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu ambaye ni mtoto mara baada ya kubainika kwamba muathirika anaweza kuwa ni mtoto na mpaka pale utambuzi, kuunganishwa na familia na kupona kabisa kwa mtoto kukithibitika (angalia sehemu ya IV, kifungu cha 19 cha sheria);

- Mkataba wa haki za mtoto unasema kwamba "Nchi wanachama wachukue hatua zote za kisheria, kiuongozi, kijamii na kielimu ili kumlinda mtoto na namna zote za ukatili kimwili au kiakili, kuumizwa au kunyanyaswa au kuhudumiwa kwa uzembe, uonevu au unyonyaji, wakati akiwa katika uangalizi wa wazazi, walezi kisheria au mtu yeyote ambaye anamhudumia mtoto";
- Jitihada zifanywe katika kutambua mahali ambapo mtoto anatoka na familia yake, hata hivyo izingatiwe kwamba mlezi wa mtoto kisheria anaweza kuwa ameshiriki katika mchakato wa usafirishaji;
- Haki za mtoto muathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu zimezingatiwa kwa makini kuhusiana na kumrudisha mtoto (sehemu ya IV, kifungu cha 22 cha sheria).

**Mwongozo wa Kusaidia Watoto Waathirika wa Usafirishaji Haramu wa Binadamu**

Miongozo ya msingi ifuatayo izingatiwe wakati wa kushughulikia mahitaji ya watoto waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu:

- Pale ambapo umri wa muathirika haujulikani na kuna sababu za kuaminika kwamba muathirika ni mtoto, watoa huduma wamhudumie wakiamini kuwa ni mtoto. Wakati wakisuburi uhakiki wa umri, muathirika anatakiwa ahudumiwe kulingana na viwango maalumu vya ulinzi wa mtoto muathirika.

**Hasa:**

- Baada ya utambuzi wa mtoto muathirika, au pale ambapo inasadikika kuwa muathirika ni mtoto, watoa huduma wanatakiwa kwa haraka waandae uhamisho wa mtoto muathirika kwenda sehemu salama au makazi salama;
- Tathmini ya umri ifanywe kulingana na vigezo vya kitaifa, lakini katika hali ya umakini;
- Baada ya utambuzi wa mtoto muathirika, huduma za malezi zitafutwe ili kumchagua mlezi;
- Wakati huo huo, faragha na usiri wa masuala ya mtoto vizingatiwe;
- Watoto waathirika wanastahili kupata uangalizi na ulinzi wa haraka ikiwa ni pamoja na usalama, chakula na malazi katika mahali salama, kupata huduma ya afya, msaada wa saikolojia ya jamii, msaada wa kisheria;
- Watoto waathirika ambao hawana utaifa/ ukazi wa nchi waliyokutwa, kwa kanuni ya ujumla wanastahili kurudishwa katika nchi zao za asili;
- Watoto waathirika hawatarudishwa kwenye nchi zao za asili kama, baada ya tathmini ya hatari na usalama, kuna sababu za kuaminika kwamba usalama wa watoto au wa familia zao uko hatarini.

**Tamaduni, dini na lugha:** Waathirika wote wa usafirishaji haramu wa binadamu lazima wapewe heshima sawa, bila kujali tamaduni, jamii au dini zao. Waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu wanaweza kutoka sehemu mbalimbali za nchi au mkoa, au sehemu yoyote duniani. Ni muhimu kufahamu muingiliano wa tamaduni na tofauti za dini wakati wa kushughulikia mahitaji ya waathirika. Moja ya changamoto kubwa katika kutoa msaada kwa waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu ni tofauti ya lugha. Waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu wanaweza wasiweze kuongea lugha inayojulikana katika nchi ambayo inawasaidia; kadhalika, mara nyingi wasafirishaji huhakikisha kuwa hii inatokea kama mbinu mojawapo ya kuwadhibiti waathirika. Kwa kufahamu hili, taarifa muhimu, fomu za kuridhia na huduma zitolewe kwa muathirika katika lugha ambayo anaielewa. Mara nyingi hii inahitaji huduma za mtafsiri. Kama ilivyo kwa watoa huduma wote, ni muhimu kwa mtafsiri yoyote ambaye anawasiliana na muathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu awe anaaminika na apewe mkataba wa kuzingatia usiri. Hii inaweza kufanya kazi vizuri kwa kupitia miundo rasmi kama vile balozi na mahakama, ambazo mara nyingi hutumia huduma za kutafsiri ambazo zimethibitishwa. Kama mtoa huduma unatakiwa umhakikishie muathirika kuwa anaweza kukuamini kwa kuwa uaminifu wao umevunjwa mara kwa mara katika mchakato wa usafirishwaji. Uhakika huo pia wapewe watafsiri. Watafsiri wanatakiwa waelewe kwamba hawako pale kujibu kwa ajili ya waathirika bali ni kutafsiri moja kwa moja.

**Uhalifu wa Kupangwa:** Usafirishaji haramu mara nyingi ni uhalifu wa kupangwa unaovuka mipaka ya nchi na taifa.

Ni uhalifu wa kupangwa wenye vipengele vingi kwa sababu:

- Unahusisha uhalifu wa aina mbalimbali kama kununua, kuuza, unyanyasaji wa kijinsia na unyonyaji, kufungiwa, na utekaji;
- Maeneo ya matukio ya uhalifu yanaanzia kutoka eneo la asili kuelekea eneo la kati na mpaka eneo la mwisho;
- Unahusisha unyanyasaji wa mara kwa mara toka kwa wanyanyasaji mbalimbali, ambao mara nyingi wana mitandao na wamejipanga;
- Ni 'kosa endelevu', ambalo linaanza na usaili na huendelea mpaka pale muathirika atakapookolewa; na,
- Kwa 'biashara' ya uuzaji wa watu, wahalifu wanajipatia 'faida' katika hatua mbalimbali za shughuli zao.

**Uhitaji wa nguvu kazi (ajira ya watu) kwa gharama nafuu:** Usafirishaji haramu wa binadamu kwa uhakika una faida kubwa, sio tu kwa mawakala ambao hufanikisha usafirishaji au uvushaji wa watu nje ya mipaka, lakini pia kwa waajiri ambao huwanyonya wale wanaowafanyisha kazi kwa nguvu katika maeneo ya mwisho. Unyonywaji wa wasafirishwaji haramu mara nyingi hutokea kwenye maeneo matatu kati ya haya; (a) kwenye shughuli za kiuchumi ambazo aidha ni halali au ambazo sio rasmi, (b) kwenye sekta za kiuchumi ambazo zina udhibiti hafifu au ambazo hazina udhibiti na ni vigumu kutekeleza udhibiti pale ambapo viwango vya faida vinakuwa vimeshuka sana, (c) maeneo ambayo ni vigumu kusimamiwa na kanuni za kazi kwa mfano majumba binafsi .Lazima ielewekekuwa uhitaji huo ni wa nguvu kazi yenye gharama nafuu ambayo inaweza kudhibitiwa na waajiri . Mara nyingi waajiri wanajihusisha na uuzaji wa bidhaa au utoaji wa huduma mbalimbali na wako katika nafasi ya uhitaji wa nguvu kazi ya gharama nafuu. Kwa mfano hitaji kubwa la nguvu kazi ya gharama nafuu kwenye mashamba ya cocoa imepelekea usafirishwaji haramu wa watoto na watu wazima kutoka maeneo jirani kuelekea nchini Ivory Coast (hii imekuwa ikitokea tangu katikati ya miaka ya 1990) .

## 4.5 Utambuzi wa Waathirika

**KISA MKASA 4a: Kim** (Rejea Zoezi 4b)

*Nora aliletwa ofisini kwako kupitia asasi isiyokuwa ya kiserikali. Yeye ana miaka 22 na hivi karibuni amekimbia kutoka kwenye moja ya danguro. Asasi hiyo isiyokuwa ya kiserikali imekupa taarifa kwamba Nora hana nyaraka zozote za utambulisho wake. Hatahivyo, walishindwa kuwasiliana naye sababu alikuwa hawezi kuongea lugha yoyote ya eneo lile. Unaweza kuona michubuko kwenye uso wake na anaonekana amechoka.*

**KISA MKASA 4b: Dan** (Rejea Zoezi 4b)

*Pia asasi hiyo imekuletea mtu mwingine ambaye ni Daniel. Daniel anaonekana ni mtu mwenye miaka 35 na anaweza kuwasiliana vizuri. Wakazi wa eneo karibu na mpaka wa mji, walimkuta akiwa hana fahamu na akapelekwa hospitali. Yeye alisema alikuwa anasafiri akiwa ni sehemu ya kundi lililoongozwa na mtu anayejulikana na polisi kwa makosa ya uhalifu aliyoyafanya kipindi cha nyuma. Daniel alikuwa na pasi ya kusafiria lakini hakuwa na visa ya kumruhusu kuingia nchini. Anaonekana mwenye hofu na wasiwasi. Anasema aliporwa na kundi la vijana ambao walichukua hela alizokuwa amebeba.*

### 4.5.1 Maelezo ya Viashiria vya Awali

Viashiria ni maelezo (tendo) au alama zinazoenyesha kwamba kesi fulani inaweza kuwa ya usafirishaji haramu wa binadamu. Vinaweza kuonekana au kujulikana kwa kuwa na uelewa wa matukio ambayo yanahusiana na shughuli za uhalifu, maelezo kutoka kwa muathirika au alama za kudhuru zinazohusiana na usafirishaji haramu. Kuna viashiria vingi vya usafirishaji haramu wa binadamu. Vingine ni vya wazi kama alama zinazoonekana au kuonyeshwa na muathirika. Kwa mfano, muathirika anaweza kueleza wazi kwamba amekuwa wakifanya kazi kinyume na matakwa yake au akaonyesha mashaka/ kutoamini wenye mamlaka husika. Viashiria vingine sio vya wazi na vinaweza visijionyeshe mpaka baadae wakati wa upelelezi. Usafirishaji haramu wa binadamu unatofautiana na vivyo hivyo hata viashiria vinatofautiana. Baadhi ya kesi za usafirishaji haramu ni wazi kutokana na alama ambazo muathirika anazionyesha. Kesi zingine zinaweza kuonyesha hali/ mazingira ambayo yatawafanya watoa huduma kuwa na mashaka au kujiuliza kama kweli muathirika amepitia katika hali ya usafirishaji haramu. Utambuzi wa mwanzo wa viashiria ni muhimu ili kuweza kujua kama muathirika amesafirishwa au kama watoa huduma wanahisi kuna mazingira ya usafirishaji haramu. Kuwepo au kutokuwepo kwa viashiria vya awali/mwanzo haina maana kwamba usafirishaji haramu umethibitishwa au umepuuzwa.

Inatakiwa ifahamike kwamba viashiria ambavyo vimeainishwa hapo chini vinalenga kusaidia mchakato mzima wa kutathmini. Mazingira ya ndani na uzoefu unaweza kuonyesha uhitaji wa viashiria vya ziada au kukubaliana na vile vilivyopo. Watoa huduma wanatakiwa kubadilika kulingana na mazingira na kukabiliana na mazingira hayo ipasavyo. Viashiria vyote vinatakiwa vizingatiwe kwa ujumla sababu hakuna hata kimoja kitakachotoa majibu kikisimama peke yake.

Viashiria vya awali vifuatavyo vinatakiwa vizingatiwe:

**Umri** - Jinsi mtu anavyokuwa na umri mkubwa ndivyo anakuwa na uwezekano mdogo wa kuhusishwa katika biashara ya usafirishaji haramu wa binadamu. Unyonyaji wa kingono bado ni lengo kuu la usafirishaji haramu, na wasafirishaji haramu huwa hawasafirishi waathirika wenye umri wa kati au zaidi sababu hawahitajiki sana na wateja. Msimamo huo huo hutumika kwa upande wa unyonyaji kwa lengo la kufanyishwa kazi kwasababu jinsi mtu anavyokuwa na umri mkubwa ndivyo anavyozalisha kidogo akiwa katika mazingira ya kazi ngumu. Kwa upande mwingine, jinsi mtu anavyokuwa na umri mdogo ndipo kunakuwa na uwezekano mkubwa wa kuhusishwa kwenye usafirishaji haramu wa binadamu. Idadi ya watoto wanaohusishwa na uhalifu inaongezeka kila mwaka na watoto wako kwenye kundi hatarishi kwasababu wanaweza kunyonywa kwa njia nyingi: katika sekta ya ngono, masoko haramu ya kazi, kama 'watumwa' wa kufanyishwa kazi za ndani na kupitia viungo vyao vya mwili.

**Jinsia** - Usafirishaji haramu kwa lengo la ngono mara nyingi unawaathiri wanawake na wasichana kwasababu ukahaba unaendelea kuwa aina ya unyonyaji yenye faida kubwa. Usafirishwaji wa wanaume kwa lengo la ukahaba hasa kwa wavulana wadogo, unaanza kuongezeka na hauwezi kufumbiwa macho. Kama mtu ni mwanaume au mwanamke sio kigezo cha kumsafirisha kwa lengo la unyonyaji wa kufanyishwa kazi, utumwa au kuondoa viungo, kwa kuwa jinsia zote zinaonekana kuhusishwa na usafirishaji haramu wa binadamu kwa kiwango sawa.

**Ukabila/Utaifa** - Upatikanaji wa waathirika unategemea sababu mbali mbali zikiwemo, umaskini, ubaguzi na ukosefu wa fursa na ni mara chache muathirika wa kweli kutoka nchi tajiri zilizoendelea. Hata hivyo, inawezekana kwamba baadhi ya makabila madogo yanaweza kuwa katika hali hatarishi/ yakalengwa katika usafirishaji haramu. Sababu zinazosukuma watu kusafirishwa zinaweza kuchangia katika mazingira ya ndani ya nchi na ya kikanda, mfano kutoka kijijini kwenda mjini. Fikra kwamba "mjini kuna maisha mazuri".

**Nyaraka** - Kutokana na mazingira ya kikanda au kijiografia, mara nyingi vitambulisho na hati za kusafiria huchukuliwa kutoka kwa waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu kama njia ya udhibiti toka kwa wasafirishaji na waathirika halisi mara nyingi hawatakuwa na nyaraka hizo, ingawa hayo pia yanaweza kuonekana kwa waomba hifadhi wengi na kwa baadhi ya kesi za magendo ya binadamu.

**Eneo la mwisho** – Eneo la mwisho ambalo muathirika alikutwa kabla ya kuwasiliana na watoa huduma, mara zote litakuwa ni muhimu: danguro, klabu ya usiku, wakala wa kutafutia watu kazi, sehemu za unyonyaji kwa lengo la kufanyishwa kazi kama viwanda, migahawa, au maeneo ya kilimo yatakuwa ni viashiria vya unyonyaji.

**Mazingira** - Mazingira yanayopelekea mtu kupewa rufaa na kwenda sehemu nyingine siku zote yatakuwa ni kiashiria na ni muhimu taarifa nyingi zipatikane kutoka kwa yule aliyetoa rufaa; mazingira kama kuokolewa kutoka kwenye madanguro; utambuzi na uokolewaji na asasi zisizo za kiserikali zitarahisisha mchakato wa uchunguzi.

**Alama/ushahidi wa unyanyasaji** – Alama yoyote inayoonyesha majeraha mwilini inaweza kuwa kiashiria chanya cha usafirishaji haramu wa binadamu; waathirika wananyanyaswa na wasafirishaji na wateja ambapo sio kitu cha kawaida katika kesi za magendo ya binadamu. Kitu cha msingi katika maamuzi yoyote yanayohusiana na hili, ni suala la muendelezo wa unyanyasaji hata baada ya kufika katika eneo lililokusudiwa.

**Tathmini ya taasisi iliyotoa rufaa** – Kwa kesi ambazo muathirika amepelekwa kwa watoa huduma kupitia taasisi za rufaa, kama vile asasi zisizo za kiserikali, maoni ya watoa rufaa wataalamu wanaofanya kazi katika eneo hilo, yatakuwa ya msingi katika hatua za uchunguzi na ni muhimu yaingizwe katika tathmini ya jumla.

### 4.5.2 Uthibitisho wa Viashiria

Kama viashiria vimetambuliwa, hatua inayofuata ni kutafuta kama kuna taarifa nyingine zinazoweza kusaidia uthibitisho wa viashiria. Kwa kutoa uthibitisho wa ziada wa viashiria itasaidia kuonyesha chanzo/asili ya kesi ya usafirishaji haramu na kutoa taarifa ili kufanya maamuzi ya hatua zipi zifuatwe. Hata hivyo, uthibitisho wa viashiria unatofautiana kulingana na kila kesi ukizingatia kwamba kila kesi inahusisha viashiria vya aina yake/tofauti.

Uthibitishaji wa viashiria vya awali unaweza kufanikiwa kwa njia mbalimbali, ikiwemo kuwauliza waathirika maswali ya nyongeza na kupitia nyaraka (kwa mfano nyaraka za kusafiria ambazo zinathibitisha utambulisho, umri, tarehe ya kuingia na kutoka, taariafa za matibabu kama zipo; tiketi za kusafiria). Kufuatia uchunguzi, maamuzi ya hatua inayofuata yanatakiwa yafanyike. Hatua itakayochukuliwa inategemea chanzo na mazingira ya kesi fulani ya usafirishaji haramu wa binadamu na ustawi wa muathirika aliyesafirishwa.

**Zoezi 4b – Viashiria vya Mwanzo/ awali**

**Lengo:** Kutambua viashiria vya mwanzo vinavyotumika katika kuwatambua waathirika ambao wanaweza kuwa wa usafirishwaji haramu wa binadamu.

**Muda:** Dakika 50

**Mwezeshaji:**

- Omba washiriki waelezee mazingira ambayo watoa huduma wanaweza kuwakuta waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu.
- Orodhesha majibu kwenye bango kitita.
- Jadili mambo ambayo yatakuwa yameachwa.
- Eleza kwamba zoezi linalofuata linahusu maswali yafuatayo:
- Tunawezaje kutambua kwamba mtu ni muathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu?
- Ni ishara gani au viashiria vinavyotumika kutambua kama mtu amesafirishwa kwa njia haramu?
- Waombe washiriki waangalie mifano hapo juu na wajibu maswali.
- Toa dakika saba za kusoma.
- Ongoza majadiliano ya mrejesho.
- Orodhesha majibu kwenye bango kitita na kwa kifupi jadili kila kiashiria cha mwanzo. Pia ongezea kwa kuelezea viashiria vya mwanzo ambavyo vinaweza kuwa vimeachwa kwenye majibu ya awali.

**Swali:**

Ni mtu gani kati ya hao wawili ambaye unadhani anaweza kuwa amehusishwa na usafirishaji haramu wa binadamu? Eleza kwanini.

### 4.5.3 Maswali maalumu ya utambuzi[34]

Maswali na maoni yaliyotolewa hapo chini ni maswali bora ya mahojiano - majibu na viashiria vilivyotathminiwa kabla viangaliwe kwa pamoja kabla ya kufikia maamuzi.

1. **Mawasiliano yalianzaje kati ya mtu (msafirishwaji) na yule anayesaili?** Je mawasiliano yalianzishwa na msafirishaji kupitia uhusiano binafsi, familia au mtandao wa marafiki au kupitia matangazo ya kazi au fursa za kazi zilizopendekezwa? Kwa usafirishaji haramu wa binadamu wa kuvuka mipaka ya nchi, mara nyingi mawasiliano ya moja kwa moja hufanyika na muathirika au familia ya muathirika (kama ni watoto). Uhamaji kwa lengo la kazi mara nyingi hutoa fursa za unyonyaji kwa wasafirishaji pale ambapo watu wanahama kwa ajili ya kutafuta kazi. Mara nyingi vyombo vya habari hutumika katika mchakato wa utambuzi kwa waathirika wa unyonyaji wa kingono na uhamaji wa kimataifa, kwa mfano, kwa kuitikia wito wa matangazo ya ajira nje ya nchi.

2. **Ni aina gani ya kazi iliahidiwa na kutarajiwa, aidha kwenye sehemu nyingine ndani ya nchi au katika nchi za kigeni?** Ni ujira upi na mazingira yapi yaliahidiwa katika nchi ya mwisho? Kwa ujumla kesi za usafirishaji haramu zinahusisha kiasi fulani cha ulaghai kwa upande wa msafirishaji. Hii inaweza kuwa ni ulaghai kamili kulingana na aina ya ajira au ulaghai usio kamili pale ambapo muathirika hujua kwamba lengo la safari yake ni kujihusisha na biashara ya ngono au aina fulani ya kazi na akadanganywa kwa mfano kuhusu mazingira ya kazi na kiwango cha malipo.

3. **Je kuna fedha yoyote iliyotolewa awali kwa mtu anayesaili?** Mipangilio ya kifedha ni muhimu, mara nyingi uhalifu wa usafirishaji haramu wa binadamu unafanyika kwa misingi ya aina fulani ya kuweka rehani ambapo muathirika anakuwa na madeni ya msafirishaji ambayo yanatakiwa kulipwa mara baada ya kufika kwenye nchi ya mwisho. Waathirika wengi ni maskini na mara chache sana wana uwezo wa kulipia safari zao, uthibitisho wa hili ni kiashiria tosha cha usafirishaji haramu wa binadamu.

4. **Je mtu alisafirishwa kwa nguvu/lazima kutoka kwenye nchi yake ya asili ili kwenda kunyonywa?** Waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu hutekwa na hiki ni kiashiria kikubwa cha uhalifu wa usafirishaji haramu wa binadamu- Kuondolewa kwa nguvu hutokea mara chache kwenye kesi za magendo ya binadamu.

5. **Nani alilipia gharama za usafiri?** Kwa kuwa waathirika wengi hutoka kwenye mazingira ya umaskini, wasafirishaji mara zote hulipia gharama za usafiri. Hii inapelekea waathirika kuwa na madeni, ambapo hutumika kama njia ya udhibiti na hiki ni kiashiria tosha cha usafirishaji haramu wa binadamu. Kesi za magendo ya binadamu ambazo mfanya magendo hulipia gharama zote humuweka muathirika katika hali inayochangia unyonyaji, na pia huficha ukweli wa kesi ya magendo pale ambapo muathirika huishia kuwekwa rehani afikapo nchi ya mwisho na kuwa muathirika wa unyonyaji, hivyo kuhusisha usafirishaji wa binadamu.

6. **Je kuna mipaka yoyote ilivukwa, kama ndivyo, je ilivukwa kwa siri au wazi? Kama ilivukwa kwa wazi, je nyaraka alizotumia muathirika kuvuka mipaka zilikuwa ni za kwake au za uongo, au visa za uongo zilitumika?** Waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu wanaweza kuvuka mipaka kwa siri au kihalali, kwa njia ya miguu au kwa magari, wakitumia nyaraka halali au za kughushi. Taratibu za usafiri zinategemea mazingira na eneo. Kuvuka kwa kutumia njia za ndani kunaweza kufanikishwa kwa kificho; maeneo ya mbali yanahitaji njia za waziwazi na uonyeshaji wa nyaraka wakati wa kuvuka mipaka. Wasafirishaji haramu hupendelea kuwasafirisha waathirika kwa njia ya wazi kwa kutumia nyaraka zao au kwa nyaraka za utambulisho za kughushi kwasababu wanaweza kuwanyonya vizuri zaidi kwenye nchi za mwisho, kama wakiweza kuwasafirisha bila kificho, kuliko kuwaficha waathirka wasionekane na jamii na kuwa kama waingiaji wa siri. Kwa kuongezea katika kesi za usafirishaji haramu, usaili unakamilika kwa njia ya ulaghai, ni muhimu kwa wasafirishaji kuendelea kudumisha uhalali kwa kutumia nyaraka za waathirika la sivyo itapelekea hatari ya kuhisiwa kuwa wamemdanganya muathirika.

7. **Nani mwenye nyaraka kwa sasa?** Kwa kawaida waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu hawataruhusiwa kubaki na nyaraka zao kwa kuwa wanaweza kuzitumia kutoroka. Kuchukuliwa kwa nyaraka ni njia mmojawapo ya udhibiti inayotumiwa na wasafirishaji kuwadhibiti waathirika. Mwelekeo mpya wa taratibu za usafirishaji zinaruhusu waathirika kuhifadhi nyaraka zao, lakini hutishiwa kwa njia zingine; kwa kigezo au dhana kwamba waathirika kwa sasa wanafanya kazi kwa uhuru/kiuhalali.

34 Rejea chapisho, the IOM (2007) IOM Counter Trafficking Training Modules Victim Identification and Interviewing p43-45

8. **Je muathrika alitumia muda wowote pale alipopita (nchi ya kati) kuelekea nchi ya tatu na kama ndivyo, Je, alijihusisha na shughuli zozote katika nchi hizo? Je, alijihusisha na shughuli ya aina gani?** Waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu wa kuvuka mipaka ya nchi si mara zote husafirishwa moja kwa moja kuelekea nchi ya mwisho. Utaratibu wa safari unaweza kutawanywa kwa kipindi cha muda fulani na waathirika wanaweza kulazimishwa kwenye shughuli za unyonyaji katika maeneo tofauti.

9. **Ni Shughuli gani ambayo muathirika amejihusisha nayo tangu alipowasili katika nchi ya mwisho?** Baada ya kufika nchi ya mwisho, unyonyaji kwa ajili ya kujipatia fedha ni lengo kuu la usafirishaji haramu wa binadamu na shughuli kama ukahaba au kazi zisizo halali ni viashiria dhahiri vya uhalifu. Sifa hizi pia zinatumika katika usafirishaji haramu wa binadamu wa ndani ya nchi.

10. **Ni muda gani baada ya kuwasili katika nchi ya mwisho shughuli hiyo ilianza?** Mwenendo/utaratibu ni kiashiria kikuu katika kesi halisi za usafirishaji haramu wa binadamu, kwa kawaida hatua ya unyonyaji itaanza mara moja au mara baada ya kufika kwasababu msafirishaji anataka kupata faida kutoka kwa muathirika haraka iwezekanavyo. Kama kuna muda mrefu ulipita mara baada ya muathirika kufika na pale unyonyaji ulipoanza, inawezekana kesi hiyo ikachukuliwa kama uhamiaji usio rasmi - ikifuatiwa na uamuzi wa kuhusishwa na kazi za kinyonyaji. Kwa mfano, mwanamke anaweza kuingia katika nchi kama mhamiaji asiye rasmi, aidha kibinafsi au kwa kutoa malipo ya awali kwa mtandao wa magendo ya binadamu na baadaye akaamua kuwa kahaba ili aweze kulipa deni au kwa ajili ya kujipatia fedha.

11. **Je mtu alilazimishwa kujihusisha na shughuli yoyote?** Kama ndivyo, kwa jinsi gani? Mahusiano yoyote ya kutumia nguvu ni muhimu katika uhalifu wa usafirishaji haramu wa binadamu. Kiwango cha nguvu iliotumika ina uhusiano na shughuli ambayo muathirika anategemea kuifanya. Kwenye kutekwa, muathirika hulazimishwa tokea mwanzo na kwa usaili wa ulaghai muathirika analazimishwa kuanzia pale uhalifu unapojulikana. Ulazimishwaji unaweza kuchukua sura mbalimbali; kwa mfano vitisho, matumizi ya ukatili wa kimwili, kingono au kiakili dhidi ya muathirika au ya familia ya muathirika, kutengwa na jamii, kuingiziwa hofu, kunyanyapaliwa au kukataliwa, kutokuamini wenye mamlaka na kunyimwa haki ya maamuzi na utu. Wasafirishaji wanaweza kutengeneza mazingira ya utegemezi wa kimwili kupitia (madawa ya kulevya au pombe/kileo) au kupitia utegemezi wa kisaikolojia au hata kunyimwa chakula na maji.

12. **Ni kiasi gani cha fedha mtu anazipata kupitia shughuli hii?** Kiasi cha fedha ambacho mtu atapata kitatofautiana kulingana na shughuli ambayo muathirika atafanya. Ukahaba unaweza kuleta fedha nyingi zaidi kuliko kazi za kawaida. Mara nyingi muathirika haoni mapato hayo maana huchukuliwa na wasafirishaji, ambao wakati mwingine huweka ahadi za kumlipa muathirika hapo baadae.

13. **Je mtu huyo aliruhusiwa kuhifadhi mapato yake?** Kwa kesi nyingi, wasafirishaji humiliki fedha zote zilizopatikana kutokana na matendo ya unyonyaji na wanaweza kumpatia muathirika kiasi kidogo kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Wahamiaji waliopitishwa kimagendo hujipatia fedha baada ya kuvuka mipaka isivyo halali na mara nyingi humiliki fedha hizo, aidha huzitumia wenyewe au huzipeleka kwa familia zao zilizoko nchi za asili. Kwa kawaida, waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu hawana uhuru huu. Hata hivyo, kwa zile kesi ambazo waathirika wanaonekana kutuma fedha mara kwa mara kwa familia zao nyumbani, bado inaweza kuwa kesi ya usafirishaji haramu wa binadamu kwasababu wasafirishaji wanaweza kuanzisha akaunti za benki zenye jina la mtu kutoka familia ya muathirika ili kuendelea kujipatia faida.

14. **Je wasafirishaji na washiriki wengine walimtaka muathirika alipe deni? Kama ndivyo, ni shilingi ngapi? Na kwa ajili ya nini?** Kuweka rehani ni jambo la kawaida katika usafirishaji haramu wa binadamu. Madeni yanatengenezwa kwa ajili kupatiwa nyaraka, hati za kusafiria, gharama za usafiri, malazi na gharama nyingine. Madeni yote yanachanganywa na matokeo yake ni upatikanaji wa kiasi ambacho hakiwezi kulipwa.

15. **Je mazingira ya kazi yalikuwaje?** Jinsi mazingira ya kazi yanavyokuwa na vizuizi na ukiukwaji wa utu, ndivyo kunakuwa na uwezekano mkubwa kwamba ni kesi ya usafirishaji haramu wa binadamu. Kuendelea kumdhibiti muathirika katika mazingira ya unyonyaji uliopitiliza ni njia mojawapo ya udhibiti inayotumiwa na wasafirishaji.

16. **Ni kiwango gani cha uhuru wa kuchagua na kutembea alikuwa nacho huyo mtu?** Waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu hupewa au kutopewa kabisa uhuru wa kuchagua aina ya kazi wanayofanya au huduma wanaotakiwa kuitoa. Ni kwanini muathirika hakuweza kutoroka mapema? Muendelezo wa unyonyaji unafanikishwa kwa muendelezo wa kutumia nguvu. Kwa lugha rahisi, mazingira ya kazi na unyonyaji yanapelekea mtu yoyote mwenye akili timamu kutaka kuyakimbia/kutoroka pale anapopata fursa hiyo. Sababu inayopelekea waathirika kushindwa kutoroka ni pale ambapo wanazuiwa kufanya hivyo sababu ya njia mbalimbali za kutumia nguvu zinazotumiwa na wasafirishaji kama matumizi ya vitisho kwao au kwa wapendwa wao nyumbani; kutengwa na jamii; hofu ya kutambulika; kunyanyapaliwa sababu ya ukahaba, woga na kupoteza uaminifu na polisi. Uwepo wa sababu zozote kati ya hizi unaonyesha uwezekano kwamba kesi hiyo ni ya usafirishaji haramu wa binadamu.

Katika hatua ya utambuzi, muathirika yoyote aliyetambuliwa anatakiwa kupewa rufaa ya huduma ya ulinzi na msaada ikiwemo makazi salama, matibabu, msaada wa kisaikolojia na kisheria na huduma zingine za ustawi. Kama muathirika ametambuliwa, anatakiwa apewe muda wa kutafakari bila kujali hadhi yake ya uhamiaji. Muda wa kutafakari unamruhusu muathirika kuendelea kukaa katika eneo la mwisho au kati huku akiendelea kupata ahueni kutokana na yale yaliyompata na kutoa maamuzi kama angependa ushirikiano wa uchunguzi/upelelezi kutoka kwa maafisa watekelezaji wa sheria.

**Zoezi namba 4d – Kuwahoji waathirika**

**Lengo:** Kuelewa kanuni zinazotakiwa kufuatwa katika mchakato wa kuwahoji waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu.

**Muda utakaotumika: Dakika 60**

**Mwezeshaji:**

- Waombe washiriki waendelee kubaki katika makundi yao ya mwanzo.

  Kama itahitajika, unaweza kubadilisha washiriki wachache kwenye makundi mengine ili kumpa kila mmoja nafasi ya kufanya kazi na watu wapya.
- Kila kundi linatakiwa lichague mwenyeketi na mwasilishaji.
- Eleza kwamba kesi hii ni muendelezo wa hadithi kutoka zoezi lililopita. Waombe washiriki waangalie maelezo na wajibu maswali yafuatayo.
- Toa dakika ishirini kwa kazi ya kikundi.
- Sikiliza taarifa kutoka katika kila kundi na tumia nafasi hiyo kujadili madhara na usalama kuhusiana na waathirika na wale wanaoweza kuwa waathirika.
- Baada ya hapo, hitimisha kwa kuelezea kanuni za msingi zinazotakiwa kufuatwa na watoa huduma wakati wa kufanya mahojiano kwa kutumia mbinu zinazolenga wahusika.
- Kama muda ukiruhusu, unaweza kuwaambia washiriki waigize jinsi ya kufanya mahojiano. Angalia kiambatanisho cha IV kwa muongozo zaidi.

  **Maswali:**

  Kwa kufanya kazi na wanakikundi wenzako na kulingana na maelezo yaliyotolewa hapa juu, jadili mambo yafuatayo:

1. Ni nani awepo kwenye mahojiano na kwanini?
2. Mahojiano yafanyike wapi? Mpangilio wa ukaaji uweje?
3. Ni ujuzi gani unaotakiwa kwa yule anayehoji?
4. Ni mambo gani utajadiliana na daktari Mosha kabla ya mahojiano?
5. Ni changamoto gani uzitegemee wakati wa mahojiano?

**KISA MKASA 4d**

**Agnes Jonathan Hatua ya II (Rejea zoezi 4d)**

***Jumatano, terehe 20/10/2009 - saa 2:00 asubuhi***

*Unafanya mawasiliano na sehemu ya makazi na kuongea na daktari Grace Mosha ambaye ni mwanasaikolojia aliyeajiriwa na TAGA, asasi isiyo ya kiserikali ambayo inatoa msaada kwa wanawake waliokumbwa na ukatili wa kijinsia. daktari Mosha anakwambia kwamba Agnes ana hali mbaya sana na ana uchovu mwingi sana kwasababu ya kukosa usingizi. Amepewa dawa za usingizi na anatakiwa asisumbuliwe na maafisa hadi hapo baadaye. Daktari Mosha anasema kwa jinsi anavyoona ni kama Agnes anataka kushirikiana nao isipokuwa ana wasiwasi juu ya mama yake kujua alichokuwa anakifanya.*

*Unafanya uchunguzi wa awali kupitia Kitengo cha Upelelezi wa Makosa ya Jinai. Uchunguzi unaonyesha maelezo yafuatayo:*

*Kuna uwezekano mkubwa anuani ikawa ni nambari 035 ya Alykhan, Upanga, Dar es Salaam. Inaaminika kuwa mmiliki ni Bwana Amir Ahmed KHAN, mwenye asili ya Pakistani. Amekuwa akiishi Tanzania kwa miaka minne sasa na inasadikiwa kuwa ni mtu mwenye uwezo mkubwa katika kampuni inayojihusisha na masuala ya ajira iitwayo "Global Opportunities Incorporated" ambayo imesajiliwa na ofisi ziko katika barabara ya Alykhan. Jina la KHAN halionekani popote katika nyaraka za usajili. Mkurugenzi na katibu wa kampuni anayeonekana kwenye nyaraka za usajili ni mwanamke aitwaye Jully Mbuttu wa anwani hiyo hiyo.*

*Tarehe 3 Novemba mwaka 2008, kupitia msamaria mwema ambaye hakutaka kujulikana, idara ya uhamiaji ilipata kibali cha kufanya upekuzi katika eneo hilo na kumkuta KHAN na wanawake wengine watano kwenye nyumba hiyo. Wanawake watatu kati ya hao walikuwa wanatoka Nairobi na wanne alikuwa ni raia wa Tanzania. Wanawake wale watatu wa Kenya walikuwa wamekamatwa na kuwekwa kizuizini na kurejeshwa kwao kama wahamiaji wasio rasmi. Wote watatu walikataa kueleza shughuli wanazofanya au kumuongelea KHAN, aliyekuwa anamiliki eneo hilo. Hakukuwa na ushahidi wa kutosha wa kuweza kuchukua hatua yeyote dhidi yake na haikuwezakana kumkamata kwa wakati ule. Mwanamke wa tano alikuwa anaitwa Dorothy MBOYA ambaye alikuwa na umri mkubwa zaidi ya wale wengine na alionekana kuwa ni msaidizi wa KHAN.*

*KHAN alifahamika kabla na Kitengo cha Uhamiaji na Kitengo cha Upelelzi wa Makosa ya Jinai na alikuwa akihisiwa kuwa ni mmoja wa washiriki wa mitandao ya uhalifu wa kupangwa ambayo ilijihusisha na biashara ya usafirishaji wa wanawake na wasichana kati ya Afrika Mashariki na Pembe ya Afrika na Ulaya. Hadi leo hakuna mtu ambaye amekuwa tayari kutoa ushahidi dhidi yake.*

***Jumatano, tarehe 20 Oktoba 2009 - saa 12:30 jioni***

*Kupitia maombi yake, unaonana na daktari Mosha kwenye ofisi za TAGA katikati ya jiji la Dar es Salaam. Daktari Mosha anakwambia kuwa Agnes bado kalala fofofo na inavyoonekana itamchukua masaa kadhaa hadi kuamka. Anasema kuwa (Daktari Mosha) aliweza kuongea na Agnes kwa muda kidogo wakati wa asubuhi na kwa utaalamu wake inaonekana Agnes alishtushwa sana na jambo lililomkuta.*

*Daktari anaendelea kusema kuwa amemshauri kwamba akiachilia mbali yeye kukubali au kutokubali kushirikiana na polisi, hana budi kumwambia mama yake ukweli juu ya kilichomsibu, ukizingatia kwamba kutokana na kilichomtokea, hakuna ambaye atashindwa kuelewa, na pia hii itasaidia kuondoa nguvu ya Amir Ahmed ambaye anaonekana kama bado yuko juu yake. Daktari alimweleza kuwa kawaida hivi vitu huwa na tabia ya kujulikana hali yoyote ile na kwamba itakuwa vizuri kwa Agnes kuwahi kumwambia mama yake kilichomkuta kabla ya mama yake kusikia kutoka kwa watu wengine. Jambo hili linamwingia Agnes akilini na ameamua kufuata ushauri wa Daktari Mosha.*

*Maandalizi yamefanywa na TAGA na mshirika wake ambaye ni asasi isiyo ya kiserikali asubuhi ya siku iliyofuata jijini Dar es Salaam kuanzisha mawasiliano kwa njia ya simu na mke wa Jonathan ili Agnes amuhakikishie mama yake kwamba yuko salama na pia amweleze kilichomtokea.*

*Daktari Mosha anakwambia kwamba Agnes anataka haki na anataka kutoa ushirikiano kama shahidi dhidi ya Amir Ahmed na wengine. Amejiandaa kutoa maelezo ya ushahidi ila anahofia rafiki zake wa Asmara wakijua alichofanya na bado anamwogopa Amir Ahmed. Daktari Mosha anashauri kuwa itasaidia kama Agnes ataelezwa jinsi mfumo wa makosa ya jinai ulivyo kabla mahojiano hayajaanza.*

*Ilikubaliwa kwamba Agnes atapatikana kwaajili ya mahojiano ya kiushahidi saa 5:00 siku inayofuata, Alhamisi, tarehe 21 Oktoba. Daktari Mosha anasema kwamba anapatikana endapo atahitajika.*

### 4.5.4 Mwongozo wa Mahojiano

Kumhoji muathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu kunahitaji umakini na umaanani, pia muda wa kutosha wa kukusanya maelezo yote ya kesi kutoka kwa muathirika.

Vile vile mahitaji, usalama na ustawi wa muathirika yapewe kipaumbele muda wote. Waathirika wa usafirishaji haramu wako katika hali hatarishi kwahiyo ni vizuri kuwahudumia. Mtu aliyepata mafunzo maalum atakaye mhoji muathirika anatakiwa kutumia tahadhari na njia sahihi.

Kuna miongozo ya msingi mbalimbali inayowezesha mahojiano yenye kuzaa matunda, kuhakikisha kuwa ustawi wa muathirika unapewa kipaumbele na kuwa na dhamira ya kuongeza matokeo yenye maana:

**Endesha mahojiano kwenye mazingira ya faragha:** Ingawa sheria hii ya msingi mara nyingi ni ngumu kufuatwa, kutegemeana na mazingira, inatakiwa kila jitihada ifanyike ili kuepuka usumbufu wakati wa mahojiano.

**Anayehojiwa awe katika hali tulivu:** Hisia na msongo wa mawazo huwa na nafasi kubwa katika mahojiano. Mtu anayehoji atakuwa na wakati mgumu kumtathmini mtu mwenye hofu. Kuanza mahojiano katika hali ya kawaida pasipokuwa na mazungumzo magumu na yakutisha kutachangia utulivu. Kwa kuondoa hisia mbaya na kumtia moyo muathirika, anayehoji anaweza kuendesha zoezi zima pasipo kumfanya mhojiwa kujisikia vibaya.

**Eleza lengo:** Anayehoji anatakiwa kuuliza maswali kwa umakini lengo likiwa ni kupata taarifa muhimu na nyingi kwa kadri itakavyowezekana.

**Mbinu nzuri za kuuliza maswali:** Kujua jinsi ya kuuliza maswali ni muhimu kama ambavyo ni muhimu kujua maswali gani ya kuuliza. Pia kufanya maswali yawe rahisi kueleweka ni muhimu.

**Acha mtu anyehojiwa awe muongeaji mkuu:** Kosa kubwa la anayehoji ni kuongea sana kupita kiasi. Tathmini sahihi juu ya mtu au kupata taarifa muhimu kuhusu uhalifu inategemea kumpa mhojiwa muda wa kutosha kuongea katika hali ya kudhibitiwa. Anayehoji anatakiwa kuendesha mahojiano na sio kuyatawala.

**Kuwa msikilizaji mzuri:** Anayehoji vizuri anatakiwa awe msikilizaji mzuri pia. Wanaohoji wanatakiwa kuwa na nidhamu na kuelekeza mawazo yao juu ya kinachosemwa na jinsi kinavyosemwa. Anayehoji asitarajie kusikia maswali fulani na kuanza kuchambua majibu kabla ya mtu kumaliza au kutazamia jibu litakuwa nini.

**Lugha ya mwili:** Kuhakikishwa kwa lugha ya mwili ni muhimu sana ili kuongeza imani kwa mtu anayehojiwa. Uwe na ufahamu wa mbinu za lugha ya mwili na uzitumie kufuatana na mazingira husika.

**Usipinge majibu yaliyotolewa:** Ni lazima wanaohoji wadhibiti hisia zao binafsi na wasiruhusu hisia hizo ziingilie mahojiano. Wasionyeshe kushtuka au kutoamini ikitokea baadhi ya taarifa zinakinzana. Waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu huenda walikumbana na matukio yasiyoeleweka kibinadamu.

**Usimkwaze/Usimuumize:** Chukulia kila kesi ya anayeweza kuwa msafirishwaji na mazingira yake kana kwamba athari ya kudhurika ilikuwa kubwa, mpaka hapo itakapobainika kuwa tofauti. Usifanye mahojiano yeyote yatakayofanya hali halisi ya mhojiwa kuzorota katika kipindi kifupi au kirefu.

**Mfahamu vizuri muathirika na tathmini athari zinazomzunguka:** Tambua athari zinazohusiana na usafirishaji haramu wa binadamu na kesi mahususi.

**Tayarisha taarifa ya rufaa:** Kuwa tayari kutoa taarifa kuhusu hatua sahihi za kisheria, afya, makazi, msaada wa kijamii na huduma ya ulinzi na kusaidia katika rufaa kama ikibidi.

**Hakikisha unaficha utambulisho wa mhojiwa na kuwe na usiri:** Linda utambulisho wa mhojiwa na hakikisha kuna usiri wakati wote.

**Sikiliza na heshimu tathmini ya hali halisi ya kila mmoja na athari za usalama wao:** Tambua kuwa kila mtu atakuwa na malalamiko au mahitaji tofauti na pia mtazamo wa mhojiwa unaweza kuwa tofauti na jinsi wengine watakavyotathmini.

**Usiendelee kumuumiza muathirika:** Usiulize maswali yatakayochokoza majibu yenye ghadhabu. Uwe tayari kukabiliana na hali ya taharuki ya mhojiwa na kumshauri na kumsaidia katika hali hiyo.

**Uwe tayari kukabiliana na dharura:** Uwe tayari kuchukua hatua pale ambapo msafirishwaji haramu atasema yuko katika hali ya hatari. Wasiliana na vitengo mahsusi vikiwemo vya huduma na misaada pale ambapo mtu ana mahitaji maalum. Kama huna uhakika jinsi ya kutatua tatizo mahsusi au kama utakumbana na matatizo magumu, hatua stahiki ya kuchukua wakati wote ni kuwaita wataalam wa kitengo maalum cha kupambana na usafirishaji haramu au ikiwa mtu huyo atahitaji msaada wa haraka mwelekeze mtu huyo kwenye asasi isiyo ya kiserikali au taasisi ya serikali inayohudumia waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu na vivyo hivyo toa taarifa kwenye kitengo maalumu husika.

Kuna miongozo mahususi zaidi iliyoandaliwa na Shirika la Afya Duniani, ambayo ni muhimu sana kwa wale wanaokutana na waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu kwa mara ya kwanza.

**Mwongozo wa kuwahoji Watoto:**

Miongozo ifuatayo inapendekezwa wakati wa kuwahoji watoto:

- Wafanyakazi pekee waliopata mafunzo ya mahitaji maalum na haki za watoto wanatakiwa kuwahoji wale wanaodhaniwa kuwa ni waathirika. Pale inapofaa na ikiwezekana wale wanaohoji wawe wa jinsia moja na hao watoto;
- Tengeneza mahali pa mahojiano panapo endana na umri, ikiwezekana pawe na vitu vya kuchezea kama mwanasesere, vitabu au michezo mbalimbali;
- Anzisha maongezi kwa kuzungumzia au kufanya vitu ambavyo havina uhusiano na mikasa ya usafirishwaji (jadili mambo ambayo yanajulikana na mtoto);
- Weka mazingira yawe ya kawaida na yasiwe rasmi. Wasiliana na mtoto uso kwa uso;
- Tumia lugha inayofaa na rafiki kwa watoto (tumia maneno ambayo mtoto anayatumia);
- Elezea mambo katika njia ambayo mtoto ataelewa. Maswali yatakayoulizwa yaendane na umri na uwezo wa akili wa mtoto;
- Anza na maswali ya wazi, yanayomruhusu mtoto kujieleza;
- Epuka maswali elekezi (ya moja kwa moja), mfano "Je mtu huyo alikunyanyasa?"
- Usilazimishe na kung'anga'nia kupata taarifa pale ambapo inaonyesha dhahiri kwamba mtoto kaelezea chote anachokijua. Ufahamu kuwa watoto wanaweza kuacha kutoa baadhi ya taarifa au kutoa jibu ambalo wanaamini yule anyehoji angependa kulisikia;
- Mahojiano yafanyike mbele ya mzazi, mlezi au mtaalam wa ustawi wa jamii au mwanasaikolojia;
- Maliza mahojiano katika hali ambayo itamhakikishia yule mtoto kuwa amefanya vizuri na pia aneyehoji anapatikana wakati wote kama atahitajika kuongea naye zaidi.

## 4.6 Usalama na Usiri wa Taarifa

Nakala za karatasi zenye taarifa:

Taratibu nzuri zinazohusiana na machapisho yenye taarifa za siri kuhusu usafirishaji haramu wa binadamu zinajumuisha:

- Kuhifadhi taarifa mahali salama katika kabati linalofunga;
- Pale ambapo taarifa zinatumika, zisiachwe peke yake bila msimamizi;
- Ziteketeze au ziharibu nakala ambazo hazihitajiki tena.

Ni muhimu sana kusimamia au kushughulikia taarifa za siri zinazomhusu muathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu kwa kuzingatia suala zima la usalama. Hali nyeti ya taarifa za usafarishaji haramu na umuhimu wa kushughulikia taarifa hizo kwa uangalifu unasisitizwa. Wakati wote mafaili ya taarifa za usafirishaji haramu wa binadamu, pamoja na maelezo ya waathirika, yashughulikiwe na kuhifadhiwa kwa uangalifu na usiri mkubwa. Sheria ya Tanzania ya kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu, Kifungu cha 9, kifungu kidogo (1) kinaelekeza kuwa maisha binafsi na utambulisho wa waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu utahifadhiwa na kulindwa.

**Taratibu/ Kanuni za Ulinzi wa Taarifa:**

Waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu wanapaswa kufahamishwa vizuri mchakato mzima wa ukusanyaji wa taarifa zinazowahusu na matumizi yake na pia haki zao za kupata taarifa hizo.

Taarifa binafsi zinazohusu waathirika au mchakato wao wa usafirishwaji zitolewe tu pale ambapo muathirika ametoa ruhusa ya maandishi na ridhaa kamili inayoidhinisha kutolewa kwa taarifa binafsi kwa ajili ya shughuli maalum.

Kutokana na ongezeko la mashaka/hatari inayochangiwa na makundi ya uhalifu wa kupangwa ya usafirishaji haramu, ni vizuri kuwa na uangalifu madhubuti katika usimamizi na uteketezaji wa taarifa binafsi za siri.

# SURA YA 5

## MSAADA WA MOJA KWA MOJA KWA WAATHIRIKA

### 5.1 Utangulizi wa Sura

Sheria ya kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu si muhimu tu kwa ajili ya kuwashitaki wasafirishaji, bali pia ni nyenzo muhimu inayoainisha haki za waathirika. Nchini Tanzania, sehemu ya III na IV ya sheria ya kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu inaelezea ulinzi kwa waathirika. Sheria hii inaelekeza kuwa waathirika wote wa usafirishaji haramu wa binadamu wapatiwe huduma za ulinzi, mahali salama pa kulala na mahitaji ya msingi, ushauri nasaha, msaada wa kisheria, huduma za afya, ajira, elimu na pia warejeshwe katika hali zao za awali. (rejea sehemu ya IV, vifungu vya 17-24 vya sheria). Sura hii inahusu utoaji wa msaada wa moja kwa moja kwa waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu kwa kutumia vipengele husika vya sheria na taratibu nzuri za kimataifa zinazotumika.

**Malengo:**

- Kupata uelewa wa jinsi ya kutathmini hatari na mambo yanayohusiana na ulinzi na usalama;
- Kuelewa mambo ya kuzingatia wakati wa kutoa msaada moja kwa moja kwa waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu, pamoja na rufaa na kushughulikia hadhi ya ukaazi wa waathirika.

**Matokeo Yanayotarajiwa: Mwisho wa moduli, washiriki wataweza:**

- Kufahamu mahitaji mbalimbali ya wasafirishwaji na jinsi ya kukidhi mahitaji hayo;
- Kufahamu hatari za kiulinzi na kiusalama zinazoweza kujitokeza wakati wa kutoa msaada wa moja kwa moja kwa waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu na jinsi ya kukabiliana nazo;
- Kutambua hatua za kufuata wakati wa kuandaa mpango wa kuwaunganisha waathirika na familia/jamii zao;
- Kuelewa vipengele vya sehemu ya III na IV ya sheria ya Tanzania ya kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu Na. 6 ya mwaka 2008 kama inavyohusika katika utoaji msaada kwa waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu.

**Nyenzo za kufundishia:** Visa mkasa na maswali katika mwongozo huu, bango kitita, kalamu ya wino mzito, sehemu ya III ya sheria ya kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu Na.6 ya mwaka 2008.

**Muda**: Masaa 5 na dakika 30

**Marejeo muhimu:**

**Machapisho ya IOM na umoja wa mataifa** The Anti-Trafficking in Persons Act No. 6 of 2008, the United Republic of Tanzania, 2008;

- The IOM Counter Trafficking Handbook for Law Enforcement Officers in Southern Africa, 2005;
- The IOM Counter Trafficking Training Modules Victim Identification & Interviewing Techniques, 2006;
- The IOM Handbook on Direct Asisistance for Victims of Trafficking, 2007;
- Anti-Trafficking Training for Frontline Law Enforcement Officers Training Guide ICMPD, 2006;
- The United Nations Global initiative to Fight Human Trafficking, UN-GIFT B.P.:006, The Vienna Forum to Fight Human Trafficking, 13-15 February 2008, Austria Center Vienna, Background Paper, 006 Workshop: Criminal Justice Responses to Human Trafficking, 2008.

**Zoezi 5a: Kutathmini hatari**

**Lengo:** Kufahamu jinsi ya kutathmini hatari na mambo yanayohusiana na ulinzi na usalama.

**Muda:** Dakika 120

**Muwezeshaji:**

Anza kipindi kwa kufungua majadiliano ya jumla na kuuliza maswali yafuatayo:

- Je kuna hatari zozote za kiusalama ambazo watoa huduma wanao wasaidia waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu wanaweza kuzipata? Kama zipo, ni zipi?
- Vipi kuhusu waathirika wanaopokea msaada kutoka kwa watoa huduma?
- Waeleze washiriki kwamba zoezi linalofuata ni jinsi ya kutambua na kukabiliana na hatari hizi.
- Waombe washiriki wabaki katika makundi yao ya awali. Kama itahitajika unaweza kuwabadilisha washiriki wachache katika makundi ili kuruhusu kila mmoja kupata nafasi ya kufanya kazi na watu wapya.
- Kila kundi lichague mwenyekiti na muwasilishaji.
- Eleza kwamba kesi ni muendelezo wa hadithi katika zoezi lililopita. Waambie waangalie maelezo na kujibu maswali yanayofuata.
- Toa dakika sitini kwa kazi ya kikundi.
- Sikiliza ripoti kutoka katika kila kundi na tumia nafasi kujadili maswala ya hatari na kiusalama kuhusiana na waathirika na wanaoweza kuwa waathirika.
- Baada ya hapo, hitimisha kwa kusisitiza umuhimu wa usalama kwa waathirika na watoa huduma wakati wa kutoa msaada wa moja kwa moja kwa waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu.

## 5.2 Kutathmini Hatari

**KISA MKASA 5a: Agnes Jonathan-sehemu ya III**

**(Rejea zoezi 4e)**

**Muhtasari wa ushahidi wa mahojiano uliotolewa na Agnes Joathan kati ya Alhamisi tarehe 21/10/2009 na Jumamosi tarehe 23/10/2009.**

Agnes Jonathan alitoa maelezo yafuatayo kwa undani kama ushahidi:

*Anaishi nyumbani na mama yake ambaye ni mjane na ndugu zake wadogo watatu katika mji mkuu wa Kenya, Nairobi. Baba yake alifariki karibu miaka mitatu iliyopita. Agnes alipata elimu nzuri ya sekondari na mara zote alitamani kupata mafunzo ya kuwa muuguzi, kama alivyokuwa mama yake kabla ya kuwa na watoto. Agnes amemaliza mwaka wa kwanza wa mafunzo ya uuguzi na yuko muhula wa pili wa mwaka wa pili wa mafunzo hayo. Yeye ni mkristo na yuko karibu sana na mama yake. Ni mwanamke anayevutia na japokuwa alikuwa na marafiki wa kiume kipindi cha nyuma, hakuwahi kujihusisha kwa namna yoyote katika mahusiano ya kimapenzi na hata mmoja kati yao.*

*Mama yake anasumbiliwa na matatizo ya macho na ameanza kushindwa kuona vizuri. Daktari anakadiria kwamba asipofanyiwa upasuaji ndani ya miezi kumi na mbili atakuwa kipofu. Familia haina fedha za kulipia upasuaji na Agnes anapata fedha kidogo tu kutoka katika ruzuku ya wanafunzi kwa ajili ya kulipia masomo yake.*

*Katikati ya wiki, karibu na mwisho wa mwezi septemba, Agnes alijadiliana na baadhi ya wanafunzi wenzake kuhusu matatizo ya familia yake katika mesi ya chakula ya hospitali, akionyesha wasiwasi wake kuhusu afya ya mama yake na anaogopa kwamba itabidi aache masomo ili atafute kazi itakayomlipa vizuri ili aweze kulipia upasuaji wa mama yake.*

*Baadaye siku hiyo, wakati anatoka hospitali mwisho wa shifti yake, mwanamke ambaye hajawahi kukutana naye aliyejitambulisha kama Asmarina alimfuata Agnes. Asmarina alikuwa ni mwanamke wa Kielitrea, mwenye wa umri wa kati na amevaa vizuri. Alimwambia kwamba anawakilisha taasisi ndogo ya kuajiri inayoitwa "Global Opportunities Incorporated" na kwamba anaweza kumsaidia. Asmarina alimwambia Agnes kwamba amesikia kuhusu tatizo lake na la kuumwa kwa mama yake kutoka kwa rafiki yake na anatamani kupendekeza suluhu kwa tatizo hili.*

*Asmarina alimwambia Agnes kwamba taasisi yake ni moja ya taasisi zilizopo Afrika mashariki na ulaya na inafanya kazi kwa ushirikiano na taasisi nyingine ya ajira iliyopo uingereza ambayo inaajiri wanafunzi manesi kwa ajili ya kufanya kazi katika hospitali za mji wa Birmingham. Asmarina alimwambia si kwamba angeweza tu kupata mshahara mkubwa ili aweze kutuma fedha nyumbani, bali pia angeweza kuendelea na shule na kuhitimu kuwa nesi na wakati huo huo kutimiza masharti ya mkataba wake.*

*Agnes alimwambia Asmarina kwamba hana uhakika na pendekezo hilo na atahitaji muda wa kulifikiria na kuongea na mama yake. Pia alimuelezea Asmarina kwamba hana fedha za kulipia katika hio taasisi, lakini Asmarina alimhakikishia kwamba fedha za kulipia taasisi na za kusafiria anaweza kuzitoa akifika Birmingham na kwamba masharti na gharama zitaainishwa kwenye mkataba wake. Asmarina alimpatia Agness kadi ya mawasiliano yenye jina lake kamili Asmarina Hanes, jina la taasisi na namba ya simu ya mkononi. Asmarina alimwambia ampigie simu mara atakapofanya maamuzi na asichukuwe muda mrefu katika kufanya maamuzi maana nafasi ni chache na fursa ni nzuri sana kwa yeye kuikosa.*

*Agnes alilifikiria pendekezo na alivutiwa nalo kwa sababu lilitoa njia ya kupata fedha za kutosha kwa ajili ya kulipia upasuaji wa mama yake. Lilionekana la kuaminika kwake kwa sababu alishasikia wanawake wanakwenda uingereza kwa ajili ya kufanya kazi za unesi na pia alivutiwa na wazo la kuweza kumaliza mafunzo yake.*

*Baada ya kushauriana na mama yake jioni ile, Agnes aliwasiliana na Asmarina kwa simu na kulikubali pendekezo. Asmarina alimuuliza Agnes kama ana hati ya kusafiria na akamjibu kwamba hana. Asmarina alimwambia kwamba hili sio tatizo kubwa na wakutane kesho yake saa nne asubuhi katika kituo cha biashara kilichopo Mayfair Hotel katikati ya mji wa Nairobi ili wajadiliane kuhusu nafasi ile ya kazi, mkataba na mipangilio ya safari. Asmarina alielezea kwamba ofisi yake ipo ndani ya hoteli katika kituo cha biashara na hoteli ipo karibu na wizara ya mambo ya nje hivyo wangeweza kufanya maombi binafsi kwa ajili ya hati yake ya kusafiria kesho yake.*

*Asmarina alimwambia alete cheti chake cha kuzaliwa au kitambulisho chake cha shule. Agnes aliomba ruhusa shule ili aweze kutimiza ahadi yake na Asmarina ambaye alimfahamisha kwamba kwanza watahitaji kupata hati yake ya kusafiria na visa ya kuingilia Tanzania ili Agnes aende kwanza Dar es Salaam. Agnes alipouliza kwanini atahitaji kwenda Dar es Salaam na wakati yeye anaelekea Birmingham, Asmarina alimwambia kwamba taasisi ina ofisi nyingine huko na mikataba na mipango ya safari itabidi ifanyike huko kabla hajaelekea Birmingham.*

*Asmarina alimpeleka Agnes kwa mpiga picha pale hotelini na kuamuru apigwe picha nne kwa ajili ya hati ya kusafiria na kuzilipia. Akampeleka katika kitengo cha hati za kusafiria na kumsaidia kujaza fomu za maombi. Ni dhahiri kwamba Asmarina alikuwa anafahamika na wafanyakazi wa kitengo kile kwa sababu hawakupanga foleni na walipata msaada wa haraka wa mahojiano kutoka kwa mfanyakazi wa kike ambaye Asmarina alimtambulisha kama Mary. Wakati Agnes alipogundua kwamba fomu itahitaji saini ya mama yake kwa kuwa hajatimiza umri wa miaka kumi na nane, Asmarina akaonyesha ishara kwa Mary ambaye alisema kwamba hilo sio tatizo kwa sababu anakaribia kufikisha umri huo na katika mazingira hayo hilo linaweza lisizingatiwe. Mary aliwaambia kwamba hati ya kusafiria itakuwa tayari baada ya mapumziko ya chakula cha mchana. Asmarina na Agnes wakachukua risiti ya maombi kutoka kwa mtunza fedha na Asmarina akalipia malipo ya hati ya kusafiria papo hapo na akapewa risiti nyingine kwa jina la Agnes.*

*Asmarina, ambaye alikuwa anatumia muda mwingi kuongea na simu yake ya mkononi, akamwambia ni lazima warudi hotelini ili wakachukue nukushi ya uthibitisho wa mkataba wake wa unesi kutoka Birmingham. Hivyo wakaenda na Asmarina kuichukua nukushi hio kutoka kwa mfanyakazi wa kituo cha biashara. Alimuonyesha Agnes nukushi hio iliyokuwa na nembo ya "Global opportunities Incorporated-Birmingham" ikithibitisha nafasi ya kazi kwa ajili ya Agnes kama mwanafunzi wa mafunzo kwa vitendo wa hospitali ya St. Lucia huko Birmingham anayeanza tarehe 11 mwezi Oktoba. Aliona kwamba nembo ya kampuni na anwani vimendikwa kwa lugha ya kiingereza na vimetoa anuani ya taasisi kama iko chini ya kituo cha biashara cha Mayfair hotel Birmingham.*

*Hapakuwa na sehemu yoyote iliyoonesha mshahara au masharti ya ajira. Agnes alipoulizia kuhusu hili, aliambiwa kwamba taarifa hizo zitakuwepo katika mkataba atakaousaini akiwa Dar es Salaam kabla ya kuelekea Birmingham. Alimwambia kwamba bosi wake, mwanaume anayeitwa Ameir Ahmed, ndiye anayehusika na kuandaa mikataba ya nchi za nje na hayo yote yatafanyika katika ofisi ya Dar es Salaam.*

*Baadae walirudi katika ofisi ya hati za kusafiria na kuchukua hati ya kusafiria ya Agnes ambayo Asmarina alibaki nayo. Alimpeleka Agnes katika ofisi ya ubalozi wa Tanzania iliyokuwa karibu na hapo ili kuomba viza ya kuingia Tanzania. Hapo tena, Asmarina alionekana kufahamiana vizuri na wafanyakazi na hawakuhitaji kukaa kwenye foleni. Asmarina alimsaidia kujaza fomu na kuambatanisha ile nukushi. Waliambiwa warudi kesho yake kuchukua hati ya kusafiria. Kama mwanzo, Asmarina alichukua risiti ya maombi na kulipa dola kumi za kimarekani kwa mtunza fedha. Wote wakaondoka katika jengo la ubalozi.*

*Nje, Asmarina alimwambia Agnes atoe taarifa shule na apaki vitu vyake usiku na kwamba kesho yake, angemchukulia hati yake ya kusafiria na angempitia jioni nje ya nyumba yao kwa safari ya masaa nane mpaka Arusha.*

*Agnes alifanya kama alivyoambiwa. Alipaki nguo zake, baadhi ya vitu vyake binafsi, picha za familia na vitabu. Ilipofika saa nne usiku, Asmarina alifika nje ya nyumba yao akiwa ndani ya gari aina ya Mercedes Benz nyeusi. Anakumbuka kwamba ni lazima ilikuwa usiku wa jumamosi alivyoondoka na Asmarina kwa sababu mama yake alimsindikiza kwenye gari na akawa anamtania kwamba ataikosa misa ya jumapili kesho yake asubuhi.*

*Asmarina aliendesha gari usiku kucha na walivuka mpaka wa Namanga kwenye saa tisa alfajiri. Agnes anakumbuka kwamba ilibidi wakae kwenye foleni kwa masaa karibu mawili na wote wawili walijaza fomu za kuingia katika upande mmoja wa mpaka. Agnes anakumbuka afisa uhamiaji alimuuliza sababu ya kuingia Tanzania na kuandika tarifa na kuanza kulikagua gari. Alionekana kuwa na wasiwasi hadi Asmarina alipomuelezea kila kitu kwa niaba yake na kutoa nukushi ya mkataba wa kazi.*

*Baada ya kuingia nchini, kwa haraka Asmarina alichukua hati ya kusafiria ya Agnes, akamuelezea itabidi akaenayo ili amsaidie kuomba kupata viza na kibali cha kufanya kazi Birmingham katika ubalozi wa uingereza uliopo Dar es Salaam. Agnes alichukuliwa na usingizi mpaka alipoamshwa na Asmarina wakiwa kwenye maeneo ya Dar es Salaam jumapili jioni.*

*Hatimaye Asmarina alisimamisha gari katika nyumba ya ghorofa katika eneo ambalo baadae Agnes alikuja kufahamu kwamba ni upanga. Asmarina alimwambia kwamba hapo ni makao makuu ya ofisi za Global Opportunities Incorporated kwa Afrika na atakutana na bosi wao anayeitwa Ameir Ahmed. Agnes akachukua sanduku lake na kuingia ndani ya nyumba akiwa pamoja na Asmarina ambaye alimruhusu kuingia kwa ufunguo.*

*Alionyeshwa sehemu ya kupumzika na kuambiwa asubiri wakati Asmarina anakwenda kumtafuta Ameir Ahmed. Baada ya muda mfupi, Asmarina alirudi akiwa na mwanaume aliyemtambulisha kama Ameir Ahmed, ambaye ni bosi. Alikuwa na umri wa kama miaka arobaini, mwenye umbo kubwa na hakuwa mweupe wala mweusi na alionekana kama ana asili ya uarabu na alivaa kawaida. Walisalimiana na Agnes na akajitambulisha. Alimwambia kwamba atashughulikia taratibu zilizobakia kwasababu Asmarina anahitaji kurudi Nairobi haraka kwa shughuli ya taasisi. Asmarina alimkabidhi Ameir Ahmed hati ya kusafiria ya Agnes na barua (nukushi) na kumuaga Agnes na kuondoka. Agnes hakumuona tena.*

*Agnes aliwasikia watu wengine ndani ya nyumba lakini hakuonana na mtu yoyote kwa wakati huo. Amir alimpa kinywaji ambacho alikikataa hivyo alimuonesha chumba chake kidogo kilichokuwa ghorofa ya pili ambacho angekaa kwa siku kadhaa wakati akimalizia mkataba wake, akisubiri viza na kununua tiketi. Kwa mara nyingine Agnes alisikia watu wakitembea katika ghorofa ya pili. Ameir Ahmed aliondoka chumbani na Agnes akaanza kupanga nguo zake.*

*Baada ya muda mfupi, Ameir alirudi chumbani na Agnes aliona kwamba safari hii amefunga mlango. Ameir Ahmed akaanza kuongelea kuhusu ada anayodaiwa na taasisi kwa kumtafutia kazi na kiasi gani atadaiwa kwa ujumla baada ya kuanza kazi Birmingham. Akaelezea wasiwasi wake kama Agnes ataweza kulipa fedha zote anazodaiwa. Agnes akajaribu kumueleza kwamba Asmarina alimwambia kwamba kila kitu kimeshashughulikiwa kwa sababu Agnes angewalipa fedha hizo kwa awamu kutokana na mshahara wake huko Birmingham.*

*Mwenendo wa Amir Ahmed ulianza kubadilika na alisema kwamba Asmarina alikua hajaidhinishwa kutoa taarifa hizo na taasisi haitaendelea kumsaidia Agnes mpaka kiasi fulani cha fedha kitakapolipwa. Agnes alimueleza kwamba hana fedha zozote na alishamtaarifu Asmarina kuhusu hili na asingeweza kuondoka nyumbani kama hawakukubaliana. Wakati huu, sauti ya Ameir ilibadilika na alianza kutoa vitisho. Ghafla alimwambia kwamba tayari amewekeza fedha nyingi kwake na hivyo anamdai. Alikuwa tayari kumsaidia katika kazi yake kama na yeye angekubali kumsaidia pia. Wakati Agnes anauliza ni kwa jinsi gani anatakiwa kutoa msaada huo, Amir Ahmed alimweleza idadi kubwa wateja muhimu katika biashara yake ambao wamekuja na wanategemea kupata huduma za kingono kutoka kwa wanawake ambao wanaishi kama wageni katika nyumba yake. Kwa mara ya kwanza, Agnes alicheka na kumwambia hayupo makini na wala hamjui kwa kina.*

*Bila onyo, Amir Ahmed alimkaba shingo na kumsukuma kwenye ukuta wa chumbani. Alimwambia kwamba atawahudumia wateja wake kama alivyomwambia. Agnes alianza kupambana na Amir ili ajiokoe lakini Amiri alimshinda nguvu. Amir alizidi kumtisha Agnes na kumwambia atakuwa chini ya miliki yake hadi amalize kulipa deni lake. Alimweleza Agnes kuwa atakuwa mmoja wa malaya kama wanawake wengine watatu wanaoishi kwenye nyumba hiyo, na ataamua ni lini deni hilo litakuwa limekwisha. Alimwambia kwamba ataendelea kuishi katika nyumba hiyo mpaka atakapoamua kumpeleka Birminghan ambapo ataendelea na umalaya ili kulipia gharama za usafiri na deni la mkataba kwa mfanyakazi wake wa taasisi. Pindi atakapomaliza kulipa madeni yake, ataruhusiwa kuchukua nafasi yake kama nesi mwanafunzi huko Birmingham.*

*Kwa kipindi hiki, Agnes alikuwa anapata shida kupumua na kupiga kelele lakini aliendelea kujaribu kujiokoa. Alimfokea na kumwambia kamwe hatafanya vile anavyoamriwa kufanya kwa sababu yeye ni msichana mwenye tabia nzuri. Wakati huu, Amir Ahmed alimtupa chini  na kuanza kuchana nguo zake huku akimwambia kuwa kitu kinachotaka kutokea ni mwanzo wa mafunzo yake ya umalaya. Agnes alimwomba Amir amwache kwa sababu alikuwa bikira, na kwamba tukio zima ni makosa na anataka kwenda kwao.*

*Amir Ahmed alimlaza kwenye sakafu na kumweleza kwamba kama akiendelea kukataa atamuumiza. Alimvua nguo zote na kuanza kumbaka. Agnes alimsihi amwache na kujaribu kumsukuma. Amir Ahmed hakumwacha bali aliendelea kufanya naye mapenzi kwa kutumia nguvu bila idhini yake. Hakutumia kondomu katika hatua yoyote.*

*Alipomaliza, Amir Ahmed alisimama mbele ya Agnes ambaye wakati huu alikuwa bado na mshituko akilia kimya kimya sakafuni. Nguo zake zilikuwa zilikuwa zimechanika na alikuwa akitokwa na damu. Baada ya kufunga suruali yake, Amir Ahmed alimuinamia Agnes na akamshika tena koo kwa mikono yake miwili halafu akamwambia asikilize kwa makini kile anachoenda kumwambia.*

*Alimwambia kuanzia hapo atafanya kile atakachomwambia afanye na atajuta sana kama atakaidi. Alimwambia kuwa sasa anammiliki na kama atakiuka na kujaribu kutoroka atahakikisha marafiki zake ambao ni mapolisi watamkamata kama mtu aliyeingia  Tanzania kinyume na sheria  na kwa kutokuwa na kibali cha kuishi nchini na kuwa ni malaya, mambo yote ambayo ni kinyume cha sheria na atapelekwa jela kwa muda mrefu. Pia alimwambia kwamba atamwambia Asmarina amweleze mama yake kwamba yupo jela nchini Tanzania kwa sababu alikamatwa na polisi akijihusisha na umalaya. Alimwambia kwamba akifanya kama alivyomwabia, atafuta madeni yake na kuendelea na kazi yake ya uuguzi na kulipwa fedha kwa ajili ya upasuaji wa mama yake. Kama hatafanya hivyo, ataozea jela akifahamu kwamba mama yake atamfikiria yeye ni malaya. Amir Ahmed alitoka chumbani na kumfungia.*

*Baada ya muda, Agnes alipanda kitandani na kutumia kitambaa laini kufuta damu iliyokuwa inamtoka. Alihisi maumivu makali na kushindwa kujizuia kutokwa na machozi. Aliangalia huku na kule na kuona dirisha pekee la ghorofa la pili limefungwa. Aliangalia mlango ambao bado ulikuwa umefungwa. Alishikwa na butwaa na kuhangaika kukubaliana na mazingira hayo. Hakuamini yale yaliyomtokea lakini alikuwa na hofu zaidi juu ya uwezekano wa mama yake kugundua mipango ya Amir Ahmed dhidi yake. Mama yake alikuwa kila kitu kwake na hakuweza kuvumilia mawazo mabaya ambayo mama yake atayapata dhidi yake. Zaidi ya hayo, alikuwa na hofu juu ya athari ya habari hizi kutokana na hali tete ya afya ya mama yake, kama mama yake atazidiwa, nini kitatokea kwa wadogo zake.*

*Hatimaye alipitiwa na usingizi mzito na aliamshwa baadae na sauti ya mlango wa chumba ukifunguliwa. Aligundua ni lazima itakuwa ni usiku kwa sababu kulikuwa na giza nje. Mwanamke aliingia chumbani. Alikuwa na umri wa kati ya miaka 35 na 40, mweupe aliyepaka rangi nywele zake na umbo kamili. Alijitambulisha kwa Agnes kama Dorothy na kukaa karibu naye kwenye kitanda. Alimweleza Agnes kwamba ni mwangalizi wa nyumba hiyo kwa niaba ya Amir Ahmed na kwa mara ya kwanza Agnes alielewa mazingira yake mapya.*

*Dorothy alimweleza kwamba wafanyabiashara hutembelea nyumba ile kwa ajili ya ngono na na kwamba Agnes, pamoja na wenzake watatu, ambao wana vyumba vyao katika ghorofa ya pili wanategemewa kuwapa huduma hizo za ngono. Alimweleza Agnes kwamba kwa kuwa hii ilikuwa siku yake ya kwanza katika nyumba ile, asingejihusisha na umalaya usiku ule lakini angeanza siku inayofuata. Alimchukua Agnes hadi bafuni na kumsimamia wakati akijisafisha damu zilizokuwa zimemtoka. Alimrudisha Agnes chumbani na kumwambia aziondoe nguo zake zilizochanika na apumzike. Dorothy aliondoka na kufunga mlango. Baadaye usiku huo huo, Dorothy alirudi na chakula kwa ajili yake na kumfungia tena. Usiku kucha, Agnes alisikia sauti tofauti za watu zikiita katika nyumba ile na watu wakitembea katika ghorofa ya chini.*

*Asubuhi iliyofuata, Dorothy alirudi chumbani na kumchukua Agnes kumpeleka chini katika sehemu ya kupumzikia na kukaa katika moja ya makochi. Agnes alimwona Amir Ahmed akiwa amekaa pembeni ya kompyuta katika chumba kidogo kilichoko karibu na sehemu ya mapumziko. Dorothy alimpa kifungua kinywa na kumwambia kwamba atamweleza sheria za nyumba ile.*

*Alimweleza kuwa hadi Amir Ahmed atakapoamua ni muda muafaka wa kwenda Birmingham, haruhusiwi kutoka nje ya nyumba na atafanya kazi kuanzia saa nane mchana hadi saa kumi alfajiri, akishirikiana na wasichana wengine. Alitakiwa akae nao kwenye makochi na kusubiria wateja waje. Dorothy alikuwa anapokea simu zote na alikuwa mtu pekee anayeruhusiwa kuwafungulia mlango wateja. Alielezea sheria za ndani na bei kwa wateja kabla ya kuruhusiwa kuingia eneo la kupumzikia.*

*Kulikuwa na mwajiriwa mmoja aliyeitwa Charles ambaye alikuwa kama mlinzi na dereva wa nyumba ile, na mara zote alikuwa karibu na mlango na sehemu ya mapumziko kwa tahadhari kama itatokea vurugu yoyote. Alimwambia atakutana na Charles baadae na alishauriwa asimuudhi kwa namna yoyote na kwamba Charles huchukua maelekezo kutoka kwa Amir na Dorothy tu.*

*Dorothy alimweleza Agnes kwamba yeye pamoja na wanawake wengine walitakiwa kuwaburudisha wanaume na kuwahudumia kwa vinywaji katika eneo la baa. Walitakiwa kuhakikisha muziki unapigwa na filamu za ngono zinaoneshwa kwenya runinga mbili zilizopo eneo la kupumzikia. Mara mteja anapochagua mwanamke aliyemvutia, humweleza Dorothy na kulipa kiasi kinachohitajika kulingana na huduma anayoitaka. Dorothy alimweleza Agnes nyumba ile inatoa huduma ya aina zote za ngono, ikiwemo ngono zembe kama mteja atakua anahitaji huduma hiyo. Hakuruhusiwa kumkataa mteja wa aina na huduma yeyote. Dorothy alitunza fedha na Amir Ahmed alipunguza kiasi fulani kwa ajili ya kulipa madeni yake. Agnes hakuelezwa ni kiasi kilitengwa na hakupewa fedha katika hatua yeyote.*

*Baadaye asubuhi hiyo, Agnes alitambulishwa kwa wanawake wengine watatu waliokuwa wakiishi katika nyumba ile. Walitambulishwa kama Maria, Stella na Adrienne. Agnes aliwaona kuwa wana umri mkubwa kuliko yeye lakini hakuwa na uhakika. Kutokana na lafudhi zao, alifikiri kuwa Maria na Stella walikuwa waluo kama yeye, lakini hakujua Adrienne alikuwa anatokea wapi. Wanawake wote watatu walionekana kutokuwa na mawasiliano na walionekana kama watu wenye mashaka na uwoga dhidi ya Amir Ahmed na Dorothy. Wakati wakiwa pamoja katika eneo la kupumzikia kwenye nyumba hiyo, hawakusemeshana sana. Agnes alifikiri kwamba inawezekana walikuwa wanawake wazuri kama yeye lakini walikuwa na hofu pia kama yeye. Baadaye asubuhi hiyo, Dorothy alimpa Agnes vitu mbalimbali ikiwemo nguo za ndani nyeupe na kumwambia azivae wakati nyumba ikifunguliwa kwa biashara kwa sababu wateja walizipenda. Alipelekwa tena chumbani kwake na kufungiwa.*

*Agnes alisikia uchungu. Alikuwa bado na maumivu yaliyotokana na kunyanyaswa kingono siku iliyopita na alikuwa na hofu juu ya yale ambayo wateja wangemfanyia. Hata hivyo, alikuwa na hofu kama mama yake akijua alichokuwa anafanyiwa na hakuona njia ya haraka ya kujinasua kwenye janga hili. Kwa kusita na hofu kubwa alikubali.*

*Agnes alitoa muhtasari wa yale aliyoyapitia kwenye nyumba ile. Kwa kawaida wateja walianza kufika kuanzia mchana mpaka usiku wa manane. Kulikuwa na simu za tatu zilizokuwa zinaita wakati wote. Biashara ilifanyika kama Dorothy alivyoelezea. Alifungua tu milango na kutunza fedha zote. Muda wote Charles alikuwepo eneo la kupumzikia pamoja na Amir Ahmed, lakini aliutumia muda mwingi kukaa kwenye kile chumba kidogo katika eneo la kupumzikia ambapo kompyuta zilikuwemo. Agnes alipata nafasi ya kuona kilichomo ndani ya kile chumba, aliona meza yenye kompyuta mpakato na mashine ya nukushi. Aliielezea kama ofisi.*

*Kwa wastani, wateja kati ya watano au sita kwa siku walimchagua yeye. Alitakiwa kutoa huduma mbalimbali za ngono kwa wateja hao, nusu ya wateja hao walitumia kondomu. Alichukia kujiingiza katika umalaya na alipatwa na maumivu ya mwili na akili yaliyotokana na kujihusisha na huduma hizo. Alijaribu kumkataa mteja mmoja kwa sababu alikuwa mlevi lakini Dorothy alikasirika na kumlazimisha amhudumie mteja huyo. Wateja walijumuisha wafanyabiashara wenyeji na wa mataifa mengine na wengi wao walikuwa watanashati. Baadhi yao hawakuwa wabaya sana na kati ya hao, mmoja au wawili hawakutaka kufanya mapenzi japo walilipia huduma hiyo kwa Dorothy. Walihitaji tu kuongea na mtu. Mteja mmoja aliwahi kulia na kusema hakuhitaji kuja katika nyumba hiyo ila mke wake hakuelewa mahitaji yake. Amir Ahmed hakujali kwa namna moja au nyingine ili mradi mteja ametoa fedha.*

*Daima Charles alikuwa karibu, aidha jikoni katika ghorofa ya chini au katika mlango wa kuingilia. Kazi yake ilikuwa ni kuhakikisha hakuna vurugu. Hakuwahi kuzungumza na Agnes.*

*Kamwe Agnes hakuona fedha yoyote kwa sababu Dorothy alikuwa ni mmiliki wa fedha hizo. Ilikuwa ni ratiba ya kawaida kwenye muda wa saa nane mchana Amir Ahmed kwenda kumwona kwa ajili ya makabidhiano ya nusu siku. Agnes hakufahamu kiasi cha fedha kinachotozwa zaidi ya ukweli kwamba huduma ya ngono ilikuwa sawa na dola za kimarekani hamsini- aligundua hili pale mteja alipolalamika kuhusu yeye kwamba hakutoa huduma vizuri na hakuona kama alistahili kutoa hiyo dola hamsini aliyotoa.*

*Baada ya tukio hili, Amir Ahmed alimuita na kumpa onyo. Alimwambia kwamba hatakuwa na tatizo naye kama atakuwa mtii, lakini kama asipowaridhisha wateja vizuri na kuwafurahisha, ataendelea kumtesa na kumfanyia kama siku ya kwanza alipowasili, hivyo uamuzi ni wake.*

*Agnes aligundua nyumba ile ilitangazwa kwa jina la 'Aristocrats High Class Services' na ilikuwa ikitangazwa katika magazeti ya kila siku ya kitaifa na katika mitandao. Alielewa hilo kwa sababu aliona kadi nyingi za wito na kitabu cha mechi chenye majina na nembo – ya paka wa pinki – katika eneo la kupumzikia kwa ajili ya wateja kuvichukua. Aliwaona Dorothy na Amir Ahmed wakiangalia gazeti kuona kama tangazo lilikuwa sawa na mteja alimwambia kwamba hakumbuki kuiona sura yake mahali popote kwenye tovuti.*

*Kwa ufahamu wake, yeye pamoja na wanawake wenzake watatu waliishi katika vyumba tofauti vya ghorofa ya pili na madirisha ya chumba chake yalikuwa yamefungwa. Hakuelewa kama Dorothy alikua akiishi katika nyumba ile au la. Daima alikuwepo katika eneo lile muda wote ambao nyumba ilikuwa wazi kwa ajili ya biashara, lakini hakuwa na uhakika kama aliishi pale. Kwa alivyofahamu, Amir Ahmed alichukua sehemu ya chini ya nyumba kwa sababu alikuwa na funguo za sehemu ya chini ya lile jengo na mara nyingi alimwona akielekea huko. Mara kadhaa alimsikia akibishana kwenye simu mida ya asubuhi na mapema, kwa hiyo alifikiri ni lazima alikuwa akiishi mule ndani. Kamwe hakuwahi kufika chini ya jengo hilo kwa sababu kila mtu aliwekewa mipaka isipokuwa Amir Ahmed – hata Dorothy hakuruhusiwa kwenda huko.*

*Agnes alieleza kwamba, baada ya tukio la kwanza hakuumizwa tena na Amir Ahmed. Hakufungiwa tena mlango baada ya siku mbili na hakujaribu kutoroka tena kwa sababu alimwogopa Amir Ahmed na vitisho ambayo alimpa. Aliwaza vitisho hivyo mara kwa mara lakini alipatwa na hofu ya kwenda jela na mama yake kugundua mambo aliyokuwa akifanya.*

*Hali ilimbadilikia siku ya Jumanne ya tarehe kumi na tisa mwezi wa kumi. Kabla ya nyumba kufunguliwa kwa ajili ya biashara, Amir Ahmed alimchukua yeye pamoja na wanawake wawili walioitwa Maria na Stella na kuwapeleka katika eneo la kupumzikia na kuwapiga picha. Aliwaambia alizihitaji kwa ajili maombi ya viza ya kwenda Birmingham kwa sababu wataondoka naye wiki ijayo pamoja na Asmarina na ndege ya Jumanne jioni. Aliwaambia kwamba atawaeleza kila mmoja anadaiwa kiasi gani kabla ya kuondoka, ili wajue ni kiasi gani bado wanatakiwa kulipa kwa kujishughulisha na umalaya baada ya kufika Birmingham.*

*Agnes alipatwa na waiswasi juu ya mabadiliko yanayotokea kila siku. Hakuweza kukabiliana na wazo la kuondoka Afrika kwenda Ulaya na aliamini kama ataishia Birmingham, atakuwa mtumwa wa ngono kwa miaka inayokuja. Hakuamini tena kama ataweza kulipa madeni yake kwa Amir Ahmed au kama ataweza kupata fedha kwa ajili ya upasuaji wa mama yake. Aliamua kutoroka haraka iwezekanavyo.*

*Alikwenda kwenye chumba kimojawapo na mteja yapata saa tisa na nusu alfajiri ambaye baada ya kupata huduma, aliondoka. Baada ya kila mteja kuondoka, ilikuwa ni mojawapo ya majukumu ya wanawake kusafisha na kuondoa karatasi laini zilizotumika n.k na kuweka karatasi laini nyingine safi juu ya kitanda, kwa hiyo ilikuwa ni kawaida kuchelewa kidogo kurudi eneo la kupumzikia baada ya mteja kuondoka. Alifahamu madirisha katika vyumba vya wateja yalikuwa yamerudishiwa tu na hayajafungwa. Alihamaki na kufungua kwa nguvu dirisha moja na kuruka chini kwenye kibaraza. Alikimbia bila kufahamu mahali alipo au mahali anapokwenda, akiwa amevaa nguo ya ndani tu (chupi). Alivyokuwa anakimbia kwenye mtaa wa karibu alisimamishwa na maafisa wawili waliovalia sare.*

*Kwa kumalizia, Agnes alisema kwamba aliumizwa sana kwa yale aliyotendewa na Asmarina, Amir Ahmed na Dorothy na alitaka waadhibiwe kwa vitendo vyao viovu. Kulingana na ushauri wa daktari Mosha, aliona njia bora ni kumweleza mama yake mambo aliyolazimishwa kufanya lakini alihofia usalama wa familia yake, marafiki, na wanajamii wake wa Kenya.*

*Anataka kwenda nyumbani kwa mama yake haraka iwezekanavyo lakini yuko tayari kutoa ushirikiano kwa mfumo mzima wa makosa ya jinai kwa njia yoyote itakayohitajika na kutoa ushahidi dhidi ya Amir Ahmed, Dorothy na Asmarina kama kuna umuhimu. Yuko tayari kurudi Tanzania kutoa ushahidi endapo wapelelezi watamuhitaji kufanya hivyo.*

**Zoezi 5a: Linaendelea**

Mkifanya kazi katika makundi yenu, kulingana na muhtasari wa maelezo muhimu ya mahojiano ya Agnes jibuni maswali yafuatayo:

- Nani anaweza kukumbana na hatari ya kiulinzi na usalama?
- Hatari ni zipi?
- Nini chanzo cha hatari hizi?
- Ni matukio gani yanaweza kuongeza kiwango cha hatari?
- Ni kitu gani kinaweza kufanyika kukabiliana na hatari hizi?

### 5.2.1 Maswala ya usalama na tathmini ya hatari

Kutoa msaada kwa watu waliosafirishwa ni kazi ya hatari na hakuna mfumo wa ulinzi, hata uwe wa hali ya juu wa kiasi gani unaoweza kutokomeza uwepo wa hatari. Uwezo wa wasafirishaji kuweka visasi dhidi ya waathirika ambao wameweza kutoroka na/ au wametoa ushahidi dhidi yao umehifadhiwa vizuri kwenye kumbukumbu. Kwa hiyo, hatari waliyonayo waathirika dhidi ya waliowanyonya haiwezi ikaongelewa zaidi. Daima kumekuwa na hatari kwa waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu na, kwa kiasi fulani kwa wale wanaowasaidia. Hatari inaweza kuongezeka pale ambapo mashirika yanayotoa huduma yanaendelea kuwasaidia waathirika wengi zaidi kuondoka kwenye mikono ya wanaowanyonya na waathirika wengi zaidi kutoa ushahidi dhidi ya wale wanaowasafirisha. Ili kutoa ulinzi kwa waathirika na wafanyakazi katika mashirika yanayotoa huduma ni muhimu kuhakikisha kwamba hatari zinatambuliwa na kufanyiwa tathmini katika kila hatua ya mchakato wa kutoa msaada, na kwa kuzingatia uhalisia na njia za msingi, hatua sahihi za ulinzi zichukuliwe ili kuhakikisha kwamba hatari zinaepukwa kiukamilifu. Mwongozo unaotolewa katika sehemu hii umetengenezwa ili kuelezea mchakato wa kufanya hivyo.

**Tathmini ya hatari**

Hatua ya kwanza ya kukabiliana na vitisho ni kutambua kwa umakini na kutathmini kiwango cha hatari. Tathmini ya hatari kwa ufanisi inajumuisha utambuzi wa hatari kwa ujumla unayofanyika katika nchi, unayoendelea kupitiwa na tathmini maalum kutokana matukio maalum. Kufanikisha mchakato huu, viashiria mbalimbali vya hatari vya kuzingatiwa vimeainishwa hapa chini. Hata hivyo, ikumbukwe kwamba, orodha hii si kamilifu na kulingana na mazingira ya kila nchi na kila kesi, hatari nyingine na viashiria vingine vya hatari vinaweza kuwepo ambavyo navyo vifanyiwe tathmini na wafanyakazi kulingana na utaalamu na ufahamu wao wa mazingira ya nchi zao. Pale ambapo kuna ushirikiano mzuri kati ya shirika linalotoa huduma na mamlaka husika za kitaifa za kutekeleza sheria, mchakato wa kutathmini hatari ufanyike kwa kushirikiana nazo.

**Tathmini ya hatari ya jumla**

Itakuwa ni muhimu baada ya kipindi fulani kurejea tathmini ya hatari ya jumla inayotokana na matendo ya wasafirishaji. Mchakato unaoainishwa hapa unalenga kuzitambua hatari hizo tangu mwanzo. Hatua ya kwanza ya kutathmini hatari ni kuangalia mazingira yanayoizunguka nchi husika. Viashiria vifuatavyo vizingatiwe.

**Viashiria vya tathmini ya jumla**

- Kiasi na athari za usafirishaji haramu wa binadamu katika nchi;
- Je nchi husika ni ya asili/mwanzo, ya kati au ya mwisho?;
- Je ni waathirika wangapi wa usafirishaji haramu wa binadamu wanategemewa kuomba msaada kutoka katika mashirika yanayotoa huduma?
- Kiwango ambacho usafirishaji haramu wa binadamu unadhibitiwa na makundi ya wahalifu ya kupangwa;
- Uwezo wao unaotambuliwa au kukadiriwa wa kupanga na kutekeleza visasi dhidi ya waathirika na/au wafanyakazi wa mashirika yanayotoa msaada;
- Uwezo wa vyombo vya ndani vya kutekeleza sheria;
- Kiwango cha kusambaa kwa rushwa na jinsi kinavyoongeza kiwango cha hatari;
- Kiwango cha dhamira na msaada wa serikali katika kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu.

**Kuendelea kurejea thathmini ya hatari**

Ni jambo la muhimu sana kufanya muendelezo wa kuthathmini hatari ya jumla. Haitoshi kufanya tathmini mara moja, bali tathmini ya mara kwa mara italeta ulinzi madhubuti. Vipindi vitatofautiana kulingana na mazingira husika.

- Kufanya tathmini ya hatari na kuwa na mpango wa kusimamia hatari ikitokea ni jukumu la kila shirika linalotoa huduma.
- Tathmini ya hatari ijerewe angalau kila mwezi. Kulingana na mazingira ya kesi, tathmini za hatari zirejewe kila wiki au kila siku katika vipindi ambavyo hatari iko juu.

**Tathmini maalum ya hatari kulingana na matukio maalum**

Mrejeo endelevu wa tathmini ya hatari ya jumla ni sehemu muhimu ya tathmini ya hatari yoyote, tathmini maalum pia inahitajika kila mara ambapo matukio maalum yanaongeza vitisho. Kila kesi huleta changamoto na hatari maalum, hivyo basi, kila kesi itahitaji kufanyiwa tathmini kulingana na taarifa na viashiria vilivyopo.

Orodha iliooneshwa hapo chini inatoa mfano wa matukio maalum mbalimbali ambayo yanatakiwa yafanyiwe tathmini maalum-tafadhali zingatia kwamba orodha hii ni mfano na isichukuliwe kama ni ya kina. Kwa kuongezea, kwa kila mifano hii, mambo yafuatayo yanayoweza kuathiri hatari yaoneshwe kwenye tathmini:

- Waathirika wote waliotoroka wapo katika hatari ya kulipiziwa visasi na waliosafirisha, bila kujali kama wanashirikiana na vyombo vya kutekeleza sheria au la;
- Hatari hizi huongezeka kwa haraka hasa kwa kesi zile ambazo waathirika hushirikiana na vyombo vya kutekeleza sheria na hivyo kuleta hatari kubwa hasa kuhusiana na uhuru wa wanaowasafirisha;
- Katika kesi yoyote ambapo imeshagundulika kwamba wasafirishaji wanafahamu muathirika anashirikiana au anataka kushirikiana na maafisa wa kutelekeza sheria, viwango vya hatari huongezeka kwa haraka;

**Mifano ya matukio maalum ya hatari:**

- Pale ambapo muathirika anapewa rufaa kwenda katika shirika la kutoa huduma kwa ajili ya msaada, hasa kama itaonekana kwamba sehemu ya msaada itajumuisha uhifadhi wake katika makazi salama au ushirikiano na vyombo vya kutekeleza sheria;
- Msaada wowote wa uhamisho kwa waathirika pale ambapo wameshatoa ushahidi kwa vyombo vya kutekeleza sheria na kama kuna sababu yoyote ya kuamini kwamba wasafirishaji wanalifahamu jambo hili;
- Kuhusiana na waathirika wanaotunzwa katika makazi salama, mpango wowote wa kutoa nje ya makazi kwa ajili ya kuwapeleka hospitali au katika miadi mingine kwa ajili ya msaada wa kijamii;
- Kuhusiana na muathirika yoyote aliye katika uangalizi wa shirika linalotoa huduma ambaye anashirikiana na vyombo vya kutekeleza sheria, matembezi yoyote yanayolenga kufanikisha ahadi zinazohusiana na uhusiano huo, kama vile kwenda kutoa taarifa, katika gwaride la utambuzi au uchunguzi wa kiafya;
- Maudhurio katika majengo ya mahakama, hasa mpango wowote wa kwenda kutoa ushahidi katika kesi ya wasafirishaji – kwa sababu wasafirishaji wanaweza kuwa wamepewa taarifa juu ya hili kama sehemu ya haki zao kama washtakiwa;
- Uhamishaji wowote wa muathirika au mfanyakazi wa shirika linalotoa huduma kutoka nchi moja kwenda nchi nyingine ili kumuwezesha atoe ushahidi dhidi ya wasafirishaji katika nchi hiyo-kwa mara nyingine, kiwango cha hatari kitakuwa ni kikubwa kwa sababu wasafirishaji wanaweza kutabiri muda na njia itakayotumika kumsafirisha, aidga katika nchi ya mwanzo, ya kati au ya mwisho au vyote;
- Tukio lolote ambalo litatafsiriwa kama jaribio la kumtisha muathirika au mfanyakazi wa shirika linalotoa huduma-kama vile simu za vitisho zinazotoka kwa mtu asiyefahamika, au simu zinazojirudia ambapo anayepiga anakata simu bila kuongea, kuonekana mara kwa mara kwa watu wasiofahamika nje ya makazi salama au magari au kumfuatilia kwa mbali muathirika au mfanyakazi.

**Mpango wa kukabiliana na hatari na kutunza nyaraka**

Kila tathmini ya hatari, iwe ya jumla, rejea au maalum, lazima ifuatiwe na mpango wa kukabiliana na hatari utakaotengenezwa ili kushughulikia maeneo ambayo yameainishwa katika mchakato wa tathmini:

- Marejeo ya jumla ya awali lazima yafuatiwe na mpango wa kupambana na hatari ukielezea kiwango cha chini cha usalama na njia sahihi za kufuatwa ili kuhakikisha kwamba hatari inapunguzwa sana na inasimamiwa kikamilifu;
- Kwa kuwa marejeo hufanyika kama mpango endelevu, mpango mpya wa kupambana na hatari utakuwa ni wa muhimu kama hatari imeongezeka au hatari mpya imegundulika;
- Kila marejeo yanapofanyika kuhusiana na hatari au tukio maalum, ni lazima yafuatiwe na mpango wa kupambana na hatari ulioboreshwa ili kukabiliana na hatari mpya. Ni lazima mpango uandikwe vizuri na ujumuishe tathmini ya hatari mpya ikifuatiwa

na mpango wa utekelezaji wa mikakati ya ziada ya ulinzi iliyotengenezwa kwa ufanisi kukabiliana na hatari mpya.

Kufanya tathmini ya hatari na kutengeneza mpango wa kukabiliana na hatari ni muhimu kwa mashirika yanayotoa huduma katika kuwalinda waathirika na wafanyakazi wanaowasaidia. Kila utaratibu uandikwe vizuri, aidha kielektroniki au kwa njia nyingine na utunzwe kwa siri kulingana na taratibu nzuri zinazohusu kushughulikia ulinzi wa taarifa binafsi za siri na za usafirishaji.

Katika kisa mkasa kilichotolewa katika sura hii, watu kadhaa wanawekwa katika viwango tofauti vya hatari.

**Agnes:** kuna maeneo muhimu mawili ya hatari kuhusiana na Agnes:

(i) Afya yake ya kimwili na kisaikolojia kutokana na manyanyaso aliyoyapata;

(ii) Usalama wake wa kimwili kutokana na visasi vyovyote ambavyo vinaweza kufanywa na Ahmed Ameir na wafanyakazi wake;

**Waathirika wengine watatu wanaofahamika:** kuna maeneo makuu mawili ya hatari kuhusiana na wanawake wengine;

(i) Afya yao ya kimwili na kisaikolojia kutokana na kuendelea kupata manyanyaso ya kimwili, kufungiwa na kufanyiwa vitendo vya kinyonyaji.

(ii) Wanaweza kuendelea kunyanyaswa kama watapelekwa mahali pengine kabla polisi hawajawaokoa.

**Watu wengine wanaoweza kuwa waathirika:** watu wengine wanaoweza kuwa waathirika wanakumbwa na hatari katika maeneo hayohayo kwa kuwa waathirika watatu wamebaki mahali ambapo Agnes alikuwepo.

**Je ni kwa kiwango gani hatari imetambuliwa?**

**Agnes:** Kiwango ni kidogo kwa sasa kuhusiana na maeneo yote mawili ya hatari iliyotambuliwa:

(i) Yupo katika uangalizi wa kituo na anapata ushauri wa kisaikolojia kutokana na sonona aliyopata;

(ii) Yuko salama kimwili chini ya uangalizi wa daktari Malanga kwenye shirika lake lisilo la kiserikali na hakuna taarifa kuonyesha kwamba Amir Ahmed anafahamu alipo sasa.

**Waathirika wengine watatu wanaofahamika:** kiwango cha hatari ya kuendelea kunyanyaswa kimwili na kisaikolojia ni kikubwa kutokana na taarifa alizozitoa Agnes na hali yake ya kisaikolojia, ni dhahiri kwamba Amir Ahmed anawaumiza waathirika wake kisaikolojia na hakuna sababu ya kufikiri kwamba ataacha.

Kama taarifa maalum itapatikana kuonyesha kwamba Amir Ahmed anahisi Agnes atakwenda polisi, kiwango cha hatari kitaongezeka.

**Watu wengine wanaoweza kuwa waathirika:**

Kuhusiana na waathirika wapya au wanaoweza kuwa waathirika, ni vigumu kupima kiwango cha hatari. Hata hivyo, kutoroka kwa Agnes kunaweza kusababisha Amir Ahmed ahitaji mtu mpya wa kuchukua nafasi ya Agnes ili aendelee kupata faida kama kawaida kwa kutumia wanawake wanne wanaojihusisha na umalaya. Kwa mantiki hii, kiwango cha hatari kichukuliwe ni kama cha kati kwa sababu ni vigumu kuwa na sahihi lakini kisitambuliwe kama ni kidogo.

**Kuongezeka kwa hatari iliyotambuliwa**

Hatari ya kimwili na kisaikolojia kwa waathirika watatu ambao bado wanaendelea kunyanyaswa na kunyonywa inaongezekakwa sababu polisi hawajachukua hatua zozote za kuwaokoa. Hii pia inahusisha wale wanaoweza kuwa waathirika.

**Zoezi 5b: Msaada wa moja kwa moja**

**Lengo:** Kuelewa utoaji wa msaada wa moja kwa moja kwa waathirika

**Muda:** Dakika 120

**Muwezeshaji:**

- Waombe washiriki wabaki katika makundi yao ya awali. Kama itahitajika unaweza kuwabadilisha washiriki wachache katika makundi ili kuruhusu kila mmoja kupata nafasi ya kufanya kazi na watu wapya.
- Kila kundi lichague mwenyekiti na muwasilishaji.
- Waombe waangalie maelezo ya kesi ya Agnes katika zoezi lililopita na wajibu maswali hapo chini.
- Toa dakika sitini kwa kazi ya kikundi.
- Sikiliza ripoti kutoka katika kila kundi na tumia nafasi kujadili hatua zinazotakiwa kuchukuliwa ili kushughulikia mahitaji ya waathirika.

**Maswali:**

Kwa kufanya kazi katika makundi yenu na kulingana na mambo muhimu katika mahojiano ya Agnes, jadili masuala yafuatayo:

- Kuhusiana na vipengele vya sehemu ya III na IV vya sheria, ni hatua gani zichukuliwe ili kushughulikia mahitaji ya muda mfupi na ya muda mrefu ya Agnes?
- Ni jinsi gani unaweza kushughulikia suala la uwepo wake na/au ukaazi Tanzania? *Angalia kifungu cha 21 hadi 23 cha sheria*
- Ni jinsi gani utahakikisha ustawi wake kwa ujumla na kumrejesha katika jamii yake? *Angalia kifungu cha 17 hadi 20 cha sheria*
- Ni nani ahusishwe katika mpango wa maandalizi ya kumrejesha katika jamii yake?
- Ni vitu gani viwepo katika mpango wa kumrejesha katika jamii yake?
- Kama Agnes anataka kwenda nchini kwake, ni hatua gani zichukuliwe? *Angalia kifungu cha 21 hadi 23 cha sheria*
- Kama Agnes angekuwa ni mkimbizi ni hatua gani ungechukua?

## 5.3 Msaada wa moja kwa moja kwa waathirika

### 5.3.1. Huduma za msaada kwa waathirika kuwarejesha katika jamii zao[35]

**Kuwarejesha katika jamii:** lengo la mchakato wa kuwarejesha katika jamii ni kuwasaidia waathirika kwa njia endelevu kuungana na jamii zao katika hali ya usalama na kuzingatia utu wao ili waendelee na maisha yao ya kawaida. Hivyo basi, msaada wa kuwarejesha waathirika katika jamii zao unaweza kujumuisha huduma mbalimbali kama vile msaada wa malazi, huduma ya matibabu na ya kisaikolojia, ushauri wa kisheria na kijamii, fedha za kuanzia maisha katika jamii, kurudishwa shuleni na mafunzo ya ufundi stadi. Baadhi ya misaada inaweza kutolewa moja kwa moja na shirika linalompokea muathirika au na shirika linalosaidia urejeshwaji wa muathirika. Hata hivyo, huduma nyingi zinaweza kutolewa mahali ambapo muathirika anakaa na shirika lisilo la kiserikali na washirika wa serikali. Huduma zote na msaada wa urejeshwaji ni lazima zitolewe kwa muathirika kwa hiari. Shirika la kimataifa linaloshughulikia masuala ya wahamaji-IOM linashauri kwamba mashirika yanayotoa msaada yapitishe sera kwamba wafanyakazi wao ni lazima wamuelezee muathirika uwezekano na changamoto zinazoweza kujitokeza katika msaada wote unaotolewa. Huduma zitolewe kwa kuzingatia ridhaa kamili ya muathirika, faragha yake na usiri mkubwa.

**Tathmini na mpango wa kuwarejesha katika jamii zao**

Tathmini kabla ya kuwarejesha waathirika katika jamii zao ni muhimu katika kutengeneza mpango wa kumrejesha kila muathirika. Aina mbili za tathmini zifanyike kwa kila muathirika:

- Tathmini ya mtu binafsi, ikizingatia mambo yanayomuhusu muathirika moja kwa moja;
- Tathmini ya mazingira ikizingatia mazingira maalum ya muathirika, kwa mfano, mazingira pekee ya kijamii na kiuchumi na miundombinu ya msaada wa urejeshaji katika nchi na/au mji ambao muathirika amerudi.

Kwa bahati mbaya, kiuhalisia, kuna uwezekano shirika linalotoa msaada lisiweze kukidhi mahitaji ya kutosha ya muathirika. Hivyo, ni muhimu kumpa muathirika picha halisi ya yale yanayowezekana na sio kumpa matarajio yasio ya kweli ambayo yanaweza kuharibu mchakato wa kumrejesha katika jamii yake.

35 Sehemu hii imechapishwa kwa mara ya pili kutoka katika chapisho la IOM linaloitwa "the IOM Handbook on Direct Assistance to Victims of Human Trafficking (2007) ukurasa 80-87

Mipango ya urejeshaji itengenezwe katika nchi zitakazo mpokea na sio zinazompeleka kwa sababu nchi zinazompeleka haziko kwenye nafasi ya kufanya tathmini ya kutosha katika nchi inayompeleka au kuzuia muathirika asielewe vibaya kitu chochote kitakachosemwa na shirika linalompeleka kama kahaidiwa kuchagua aina maalum ya urejeshaji. Badala yake, shirika linalompeleka limfahamishe muathirika kwamba mpango wa mwisho wa urejeshwaji utaamuliwa katika nchi itakayompokea. Hata hivyo, shirika linalompeleka lifanye tathmini ya awali kujua mahitaji ya msingi ya muathirika, kama inavyoelezwa hapo chini na kuyapeleka katika shirika la nchi anayokwenda pamoja na taarifa ya kuondoka kwake. Ustawi wa muathirika ni lazima uwe ni kitu cha kuzingatiwa katika mchakato wa urejeshwaji, hivyo, kipaumbeke kiwekwe katika usalama na afya yake hasa kama kuna changamoto za ufinyu wa rasilimali watu, fedha na muda uliopo.

**Tathmini ya mtu binafsi**

Mtu ambaye anafahamu zaidi kesi ya muathirika afanye tathmini. Hii inajumuisha mfanyakazi wa shirika linalotoa huduma, afisa ustawi wa jamii, mlezi wa mtoto, mfanyakazi wa shirika lisilo la kiserikali au mwanasaikolojia. Watu hawa watathmini fursa mbalimbali za urejeshwaji zinazolenga urejeshwaji wenye mafanikio na uingizwaji katika jamii wa kila muathirika kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo:

- Kwanza kabisa, mahitaji ya muathirika, ambayo yanajumuisha kimwili, kisaikolojia, kiakili, kisheria, kijamii na kiuchumi;
- Mahitaji hasa ya muathirika, mambo anayoyatamani kwa chaguo fulani la urejeshwaji au huduma ambazo zinaweza au zisiweze kuwepo;
- Uwezekano wa muathirika kuathiriwa na mazingira yake binafsi kama vile umri, jinsi, kiwango cha elimu au uzoefu wa kazi;
- Maono ya msukumo wa muathirika, kwa mfano, kwa kujihusisha na urejeshwaji na matokeo yanayohusiana na msaada wa urejeshwaji na/au mazingira yake binafsi;

Kwa rufaa ya kimataifa, tathmini binafsi ianzishwe na shirika linalompeleka lakini imaliziwe na shirika linalompokea katika nchi yake ya awali.

**Tathmini ya mazingira**

Tathmini ya mtu binafsi ni lazima iambatane na tathmini ya mazingira. Tathmini hii ifanywe na watu wanaofahamu zaidi kesi ya muathirika, pamoja na nyumbani kwa muathirka katika nchi yake ya asili. Hii inajumuisha mfanyakazi wa shirika linalotoa huduma, afisa ustawi wa jamii, mlezi wa mtoto, mfanyakazi wa shirika lisilo la kiserikali au mwanasaikolojia. Watu hawa watathmini fursa mbalimbali za urejeshwaji za kila muathirika kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo:

- Fursa zilizopo kwa urejeshaji wa mtu binafsi, kwa mfano: aina fulani za mafunzo ya ufundi stadi zinaweza zisiwepo katika mji fulani wa nchi ya asili ya muathirika na haziwezi kutolewa kwa sababu ya kutokuwepo fedha. Pia, malazi, huduma za matibabu, ustawi wa serikali au mipango ya elimu inaweza kuwepo au isiwepo mahali anapotoka muathirika;
- Umuhimu wa pendekezo la msaada wa urejeshaji kulingana na mazingira ya muathirika, kwa mfano, mafunzo ya ufundi stadi lazima yaendane na mahitaji ya muathirika katika nchi au mji anaotoka (kwa mfano mafunzo ya uhasibu yanaweza yasiwe na manufaa kama kuna ukosefu wa ajira kwa wahasibu au uhasibu ni kitu ambacho hakipo katika jamii ya muathirika).

**Mpango wa urejeshaji**

Kwa kutumia tathmini ya mtu binafsi na ya mazingira, mpango madhubuti wa kuwarejesha waathirika katika jamii zao unaweza kutengenezwa. Katika kutengeneza mpango huu, ni muhimu kwa shirika linalompokea au mdau wa shirika lisilo la kiserikali kuwasaidia waathirika kutengeneza malengo halisi sio tu kulingana na mahitaji yao, ujuzi na sifa, lakini pia kulingana na fursa zilizopo katika nchi, mikoa na maeneo wanayojereshwa, kulingana na tathmini iliyofanyika. Zaidi ya hayo, mpango wa urejeshaji lazima uzingatie huduma ambazo shirika linalotoa msaada na wadau wake wanaweza kuzitoa. Hili liangaliwe wakati wa kutathmini mpango wa urejeshaji. Hata kama mabadiliko yatafanywa baadae, inashauriwa mpango wa urejeshaji utengenezwe kama mpango wa maandishi kati ya shirika linalotoa msaada (kwa mfano, shirika lisilo la kiserikali na watoa huduma wa serikali) na muathirika. Muundo wake maalum utatofautiana kati ya nchi moja

na nyingine na shirika na shirika, lakini daima utajumuisha na kuzingatia vipengele vifuatavyo, kama vitakavyohusika:

- Upatanishi na familia/urejeshaji katika familia;
- Matibabu/afya;
- Fedha (ruzuku, msaada wa ruzuku kwa familia na wategemezi);
- Kisheria;
- Elimu/mafunzo ya ufundi standi/mafunzo;
- Shughuli za uzalishaji mali;
- Ulinzi.

Kama ilivyoainishwa hapo awali, huduma zitolewe tu pale ambapo muathirika ametoa ridhaa yake kamili. Hivyo, shirika lihakikishe muathirika anasaini fomu za ridhaa kwa kila kipengele hapo juu kama kitakavyohusika. Kwa kesi za watoto, wazazi wao au walezi wasaini fomu za ridhaa kwa niaba yao. Mpango wa urejeshaji pia unatumika kama chombo cha ufuatiliaji na utoaji tathmini kama inavyoonekana hapo chini.

**Mchakato wa urejeshaji**

Baada ya mpango wa urejeshaji kuamuliwa, uratibu wenyewe unawenza kuanza.

**Mikakati kutoa msaada wa urejeshaji**

Msaada wa moja kwa moja kwa waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu unaweza kujumuisha huduma mbalimbali kutoka malazi, msaada wa matibabu na wa kisaikolojia mpaka wa kijamii na ushauri wa kisheria na mafunzo ya ufundi stadi. Hata hivyo, kivitendo, huduma nyingi zinaweza kuhitajika kutolewa na mashirika mengine au serikali. Katika baadhi ya kesi, shirika moja linaweza kutokuwa na uwezo wa kutoa huduma zote au lisiwepo mahali ambapo muathirika anakaa na hivyo ni lazima kutegemea mashirika mengine kwa msaada. Kadhalika, ufuatiliaji utahitajika kufanywa na shirika lililopo karibu na mahali ambapo muathirika anaishi. Mikakati mikuu mitatu ya kutoa msaada wa urejeshaji wa waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu katika jamii zao ni:

- Msaada wa awali wa shirika linalompokea muathirika;
- Msaada wa muda mrefu wa shirika linalompokea au linalotoa rufaa kwa mashirika mengine au serikali;
- Msaada wa serikali kwa muathirika.

**Msaada wa awali wa shirika linalompokea muathirika**

Msaada huu unaweza kujumuisha msaada wakati wa kuwasili, msaada wa haraka na wa kina wa matibabu/uchunguzi wa kisaikolojia na matibabu, malazi ya muda mfupi na msaada wa mahitaji mengine ya kijamii, kisheria na kiuchumi ya muathirika. Shirika linalompokea lifanye kila jitihada kuchukua hatua kuepuka mazingira tegemezi yasitokee wakati wa kutekeleza miradi yake ya urejeshaji na lilenge kumsaidia muathirika aweze kuishi maisha yake ya kawaida kama awali na ajitegemee. Msaada wa muda mrefu, hata hivyo, lazima utolewe aidha na mashirika yasiyo ya kiserikali au miundo ya kutoa msaada ya kiserikali.

**Msaada wa muda mrefu wa urejeshaji**

Msaada wa muda mrefu kwa waathirika ni muhimu kwa ajili ya urejeshaji wenye ufanisi. Kama shirika linalompokea linatoa huduma sahihi, linaweza kutoa huduma nyingi kwa pamoja. Vinginevyo, huduma zinaweza kutolewa na kupitia shirika moja lisilo la kiserikali au zaidi. Mashirika yasiyo ya kiserikali yako katika nafasi nzuri siyo tu katika kutoa msaada wa moja kwa moja kwa waathirika, bali pia katika kufanya thathmini au kusaidia kufanya tathmini ya urejeshaji, kuandaa na kutekeleza mpango wa urejeshaji. Zaidi ya hayo, mashirika yasiyo ya kiserikali yana nafasi ya kutoa mchango mkubwa katika kuangalia maendeleo ya muathirika aliyerejeshwa. Shughuli ya kuhakikisha urejeshaji wa waathirika katika jamii kwa njia salama na ya kibinadamu inajumuisha:

- Matibabu/uchunguzi wa kisaikolojia na matibabu/ushauri kwa waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu kwenye sehemu zao wanazoishi;
- Upatanishi na familia/ushauri nasaha;
- Ufuatiliaji wa mchakato wa urejeshaji mahali ambapo muathirika anaishi;
- Ufuatiliaji malazi na mipangilio ya huduma kwa watoto waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu;
- Msaada wa kuwarudisha mashuleni;
- Kutengeneza mipango ya mafunzo ya ufundi stadi;
- Ushauri nasaha na mafunzo ya ufundi stadi kwa waathirika;
- Kuwasaidia kupata ajira na ushauri kuhusu ajira;

- Ruzuku wakati wa kurejea nyumbani na mafunzo ya ufundi stadi kwa waathirika;
- Msaada kupata nyaraka zilizopotea kama vile vitambulisho na hati za kusafiria;
- Msaada wa kisheria kuhusu masuala ya madai (talaka na kupata mali zilizopotea)
- Ushauri wa kisheria na uwakilishi kwa waathirika ambao ni mashahidi katika kesi za jinai;
- Kuhifadhi namba za simu dharura;
- Kuhakikisha usalama wa muathirika kwa kuwasiliana naye mara kwa mara;
- Kuwasaidia waathirika kupata msaada wa kihisia na huduma wanazozihitaji na kuhakikisha haki zao zinaheshimiwa;
- Kutoa msaada wa usafiri salama

Shirika linalompokea muathirika lisaidie na kufanya kazi kwa kushirikiana kwa karibu na mtandao wa mashirika yasio ya kiserikali ya kimataifa na yasiyo ya kimataifa. Msaada na ushirikiano huu una nafasi ya muhimu si kwa ajili ya urejeshaji wa waathirika wenye ufanisi bali pia kwa uendelevu wa michakato ya urejeshaji. Itasaidia kama shirika litarasimisha ushirikiano wake kwa kutumia mikataba ya makubaliano na/au makubaliano mengine ili kuhakikisha mashirika yote mawili yanaelewa majukumu na wajibu wao na wa wengine.

Shirika linalowapokea liangalie shughuli za mashirika yanayoleta rufaa za waathirika kwa ajili ya msaada ili kuhakikisha ufanisi na ubora wa huduma zinazotolewa.

**Msaada wa serikali kwa waathirika**

Mara nyingine, msaada wa kuwarejesha waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu hutolewa moja kwa moja kupitia miundo ya serikali. Kama ilivyo kwa misaada yote, mkataba wa makubaliano na serikali ambao unaainisha majukumu, wajibu na huduma zitakazotolewa husaidia. Mara nyingi msaada wa urejeshaji unaotolewa na serikali unahusisha ushauri wa kijamii na kikazi, mafunzo ya ufundi stadi, msaada unaohusiana na afya, ulinzi na njia mbalimbali za kurudishwa kwenye mifumo ya elimu.

**Aina za misaada ya urejeshaji**

Wakati msaada utakaotolewa kwa kila muathirika utategemea mahitaji yake binafsi, misaada inaoainishwa hapo chini imeonekana kuwa ni ya msingi kwa waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu:

- Matibabu/huduma za afya;
- Ushauri nasaha;
- Msaada wa kifedha;
- Kurudishwa kwenye mfumo wa elimu;
- Mafunzo ya ufundi stadi;
- Biashara ndogo ndogo na shughuli zanazoleta kipato;
- Kusaidiwa kupata kazi na mipango ya mafunzo kwa vitendo;
- Nyumba na malazi.

### 5.3.2 Msaada kwa waathirika chini ya vifungu vya sheria

Sheria ya kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu ina vipengele mbalimbali vinavyolenga kuhakikisha huduma za ulinzi kwa waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu. Huduma hizi zinajumuisha malazi, matibabu na msaada wa kisaikolojia, huduma za kisheria, kupata kibali cha kuishi na kuondoka nchini pamoja na msaada wa kurejeshwa kwenye nchi yako ya asili.

a. **Malazi na huduma zinazohusiana (kifungu cha 17 hadi 24)**

Sheria inaipa jukumu wizara ya afya na ustawi wa jamii (kitengo cha ustawi wa jamii) kuanzisha na kuendesha vituo vya waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu. Vituo vinatakiwa kuzingatia viwango na miongozo ya kitaifa. Vituo vya watoto waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu nchini Tanzania vitatoa ulinzi, msaada wa mahitaji ya msingi, ushauri nasaha, huduma za kuwarejesha katika hali zao za awali na elimu. Kituo cha waathirika ambao ni watu wazima kitatoa ulinzi kwa waathirika walio kweye hatari ya kulipiziwa kisasi, ushauri nasaha na huduma za kuwarejesha katika hali zao za awali, kuwarejesha katika familia na jamii zao, kuwaendeleza kulingana na ujuzi na elimu yao.

b. **Huduma za matibabu (kifungu cha 17(2) na kifungu cha 20(2)**

Sheria inawapa haki waathirika wote wa usafirishaji haramu wa binadamu kupata huduma za afya kama mtanzania mwingine yoyote.

c. **Kutafutwa kwa familia yake (kifungu cha 11 na 27)**

Sheria iko kimya kuhusu polisi kumsaidia afisa ustawi wa jamii kutafuta familia ya muathirika. Hata hivyo, sheria inamtaka polisi atoe msaada wote unaohitajika

kwa muathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu. Zaidi ya hayo, mfuko wa kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu unaanzishwa ili kusaidia kutafuta familia za waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu.

d. **Huduma za kisheria (kifungu cha 15)**

Sheria inatamka kwamba muathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu apewe fidia inayostahili kutoka kwa msafirishaji aliyehukumiwa. Fidia hii ni kwa ajili ya matatizo aliyoyapata kimwili na kisaikolojia au maumivu mengine, au uharibifu wa vitu pamoja na fedha, au kupoteza kipato au msaada.

e. **Kumsaidia kupata haki ya ukaazi**

Sheria ya Tanzania ya kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu ipo kimya kuhusu suala hili.

f. **Kurejesha (kifungu cha 21 hadi 23)**

Sheria inaitaka serikali kufanikisha kurejeshwa kwa waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu ambao hawana nyaraka muhimu kwa kuwapatia nyaraka za kusafiria au kibali kinachohitajika kwa ajili ya kuwarejesha. Zaidi ya hayo, mtoto au mtu mwenye ulemavu ambaye ni muathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu atarejeshwa katika nchi yake ya asili baada ya ridhaa ya mzazi, ndugu, mlezi kisheria au muangalizi wa mtu aliye na ulemavu au taasisi ya serikali au taasisi ya ulinzi wa mtoto kutoka katika nchi ya asili kutoa ridhaa na kuchukua jukumu kwa ajili ya mtoto au mtu mwenye ulemavu na kumpatia msaada na ulinzi wa kutosha.

g. **Kuwarejesha katika hali ya awali na kuwarejesha katika jamii zao (kifungu cha 17 na 24)**

Sheria inaipa jukumu wizara husika ya ustawi wa jamii Tanzania bara na Zanzibar ihakikishe urejeshaji katika hali ya awali na mipango ya ulinzi inawekwa wazi kwa waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu. Pamoja na hayo, wizara inajukumu la kutoa ushauri nasaha na malazi kwa waathirika ili kusaidia urejeshwaji katika hali ya awali na urejeshaji katika jamii zao.

## USHIRIKIANO NA VYOMBO VYA KUTEKELEZA SHERIA: TASWIRA

### 6.1 Utangulizi[36]

Waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu wanastahili kupata haki zao dhidi ya uhalifu waliotendewa kwa kupitia mahakama. Mashirika yanayotoa huduma yajadiliane na waathirika kuhusu haki zao ili kuhakikisha wanafanya maamuzi sahihi jinsi ya kudai haki zao. Usafirishaji haramu wa binadamu unaonesha kuongezeka kwa kiwango cha juu duniani kote na unaleta madhara makubwa kimwili na kisaikolojia kwa waathirika. Kutokana na utaalamu wao katika kuwasaidia waathirika, mashirika yanayotoa huduma yako katika nafasi nzuri kushiriki kwenye mikakati na kujenga mahusiano ya kiuendeshaji kwa vitendo na vyombo vya kutekeleza sheria ambavyo vinaweza kuwa na ushawishi katika kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu.

**Malengo:**

- Kufahamu umuhimu wa ushirikiano kati ya watoa huduma na vyombo vya kutekeleza sheria;
- Kutambua hatari zinazoweza kujitokeza kwa kushirikiana na vyombo vya kutekeleza sheria na jinsi ya kupunguza hatari hizo;
- Kufahamu mambo ya kuzingatia wakati wa kutoa taarifa kwa vyombo vya kutekeleza sheria.

**Matokeo Yanayotarajiwa**: Mwisho wa moduli, washiriki wataweza;

- Kuelewa umuhimu wa kushirikiana na vyombo vya kutekeleza sheria;
- Kutambua hatari zitakazoweza kujitokeza kwa kushirikiana na vyombo vya kutekeleza sheria na mambo yanayoweza kuongeza hatari hizi;
- Kuelewa msingi wa ridhaa kamili ya muathirika katika mchakato wa kubadilishana taarifa na vyombo vya kutekeleza sheria;
- Kubuni na kuweka mikakati ya kuzuia;
- Kupata ufahamu kuhusu vipengele vya sheria ya kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu Na. 6 ya mwaka 2008 kuhusu kutoa taarifa.

**Nyenzo za kufundishia:** Mwongozo huu, bango kitita, kalamu ya wino mzito, sheria ya kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu ya Tanzania kifungu cha 9 hadi 16.

**Muda**: Masaa 2

**Marejeo muhimu:**

**Machapisho ya IOM na umoja wa mataifa[37]**

- The Anti-Trafficking in Persons Act No. 6 of 2008, Government of the United Republic of Tanzania, 2008;
- The IOM Counter Trafficking Handbook for Law Enforcement Officers in Southern Africa, 2005;
- The IOM Counter Trafficking Training Modules Victim Identification & Interviewing Techniques, 2006;
- The IOM Handbook on Direct Asisistance for Victims of Trafficking, 2007;
- Anti-Trafficking Training for Frontline Law Enforcement Officers Training Guide ICMPD, 2006;
- The United Nations Global initiative to Fight Human Trafficking, UN-GIFT B.P.:006, The Vienna Forum to Fight Human Trafficking, 13-15 February 2008, Austria Center Vienna, Background Paper, 006 Workshop: Criminal Justice Responses to Human Trafficking, 2008.

36 Maelezo yote katika sura hii kasoro yale ya sehemu ya 6.10 yanatoka katika chapisho la IOM linaloitwa "the IOM Handbook on Direct Assistance for Victims of Human Trafficking, Chapter 6, Cooperation with Law Enforcement Agencies (2007)" p.273-302

37 Marejeo haya hayana tafsiri rasmi kwa lugha ya Kiswahili.

**Zoezi 6a: Ushirikiano na vyombo vya kutekeleza sheria.**

**Lengo:** Kutambua mambo ya kuzingatia wakati wa mchakato wa kushirikiana na vyombo vya kutekeleza sheria.

**Muda:** Dakika 120

**Muwezeshaji:**

- Anza kipindi kwa kuwaomba washiriki watoe mawazo yao juu ya umuhimu wa kushirikiana na vyombo vya kutekeleza sheria. Unaweza kutumia maswali yafuatayo kuongoza majadiliano:

  - Je ushirikiano una faida gani kwa:

- Watekeleza sheria?
- Mashirika yanayotoa huduma?

Baada ya faida kutambuliwa:

- Waombe washiriki watengeneze makundi ya watu wanne au watano.
- Kila kikundi kimchague mwenyekiti na mwandishi.
- Waombe washiriki wajadiliane maswali hayo hapo chini.
- Waandishi watawasilisha matokeo ya majadiliano ya kikundi.
- Wape dakika 45 za majadiliano.
- Wape kila kikundi dakika 8 hadi 10 kuwasilisha.
- Hitimisha majadiliano kwa kuelezea mambo ambayo yanaweza kuwa yameachwa, na kusisitiza umuhimu wa kupeana taarifa kati ya watoa huduma na vyombo vya kutekeleza sheria, pamoja na umuhimu wa ridhaa ya mwathirika katika ushirikiano huo.

**Maswali:**

- Je ni hatari gani zinazoweza kujitokeza kwa watoa huduma kutokana na kushirikiana na vyombo vya kutekeleza sheria? Eleza chanzo cha hatari hizi na sababu zinazoweza kusababisha kuongezeka kwa hatari hizi.
- Ni mipango gani iandaliwe kwa ajili yako kama mtoa huduma, ili uweze kushirikiana na vyombo vya kutekeleza sheria, kwa mfano polisi.
- Kama muathirika chini ya uangalizi wako akiamua kuwasiliana na polisi na kutoa taarifa kuhusu msafirishaji, utachukua hatua gani kuhakikisha usalama wake? (kifungu cha 10)
- Je unaamini kuwa una jukumu la kutoa taarifa kwa polisi kuhusu kesi ya usafirishaji haramu wa binadamu unayoifahamu ukiwa kama mtoa huduma? (sheria iko kimya)

Kutokana na taswira ya wanaotekeleza sheria, ushirikiano na muathirika, uzoefu wa mashirika yanayotoa huduma na uwezo wao kiutendaji ni muhimu katika nyanja mbalimbali:

- Kama sehemu ya kwanza ya mawasiliano na maafisa wanaotekeleza sheria wanaohitaji kuhakikisha usalama wa haraka wa waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu;
- Kutoa malazi na msaada kwa waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu, ambao nao huweza kusaidia katika uchunguzi kuhusu matendo ya jinai kwa kutoa ushahidi mahakamani;
- Kusaidia kupatikana kwa taarifa za kiintelijensia ambazo mara nyingi hazipatikani kwa maafisa polisi kwa sababu waathirika wanaweza wasiwaamini kiasi cha kuwapa taarifa hizi (angalizo: kuna hatari zinazohusiana na kutoa taarifa za kiintelijensia kuhusu usafirishaji haramu wa binadamu ambazo zinaelezwa kwa kina katika sura hii);
- Kutoa msaada wa kiutaalamu na kusaidia kuboresha uwezo wa vyombo vya kutekeleza sheria kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu.

## 6.2 Ushirikiano katika taswira ya mashirika yanayotoa huduma

Kama mashirika yanayojitoa kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu na kulinda waathirika wake, yanaweza kupokea taarifa za kiintelijensia kuhusu usafirishaji haramu wa binadamu kutoka kwa waathirika, au ndugu na marafiki wa waathirika. Taarifa

hizi zinaweza kuwa ni muhimu sana kwa vyombo vya kutekeleza sheria katika kufahamu mahali walipo waathirika na kuwaokoa. Taarifa za kiintelijensia pia zinaweza zikapelekea utambuzi na uchunguzi wa wasafirishaji. Uokoaji wa waathirika na utambuzi wa wasafirishaji ni vitu viwili vya muhimu katika mkakati madhubuti wa kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu. Ushirikiano kati ya mashirika yanayotoa huduma na vyombo vya kutekeleza sheria vinaweza kusaidia zaidi katika madhumuni haya. Pamoja na haya, uzoefu wa sasa unaonesha kuwa kiasi kikubwa cha waathirika ambao wapo katika uangalizi wa mashirika yanayotoa huduma wanataka kutoa taarifa za kintelijensia kwa kwa vyombo vinavyotekeleza sheria. Pale ambapo uwezo wa kutekeleza sheria ni wa kitaaluma na madhubuti, waathirika wanaweza kutoa taarifa moja kwa moja kwa polisi. Katika kesi nyingine, waathirika wanaweza wasitake kuonana na maafisa polisi na badala yake kuyaomba mashirika yanayotoa huduma kutoa taarifa hizi kwa niaba yao. Kwa kubadilishana taarifa za kiintelijensia na vyombo vya kutekeleza sheria katika njia sahihi, mashirika yanayotoa huduma yanaweza:

- Kumsaidia muathirika ajisikie kwa namna fulani ametoa taarifa kuhusu kesi yake ambayo inaweza kupelekea msafirishaji kupata adhabu au kuwasaidia wale ambao wanaweza kuwa waathirika; na

- Kuchangia vizuri katika kuwaokoa waathirika na/au kuwatambua wasafirishaji.

Kama kawaida, ridhaa kamili ya muathirika kimaandishi, na ukweli kuwa shirika litatoa msaada wakati wote likizingatia stahiki za muathirika viendelee kuzingatiwa kama kiini cha kubadilishana taarifa za kiintelijensia.

### 6.3 Hatari zinazoweza kujitokeza kutokana na mikakati ya mashirika yanayotoa huduma

Ushirikiano na vyombo vinavyotekeleza sheria unaweza ukawasilisha mlengo mpya kwa mashirika mengi yanayotoa huduma na matokeo yake, mambo nyeti ya kisera na hatari vinaweza kujitokeza. Uwiano wa makini unatakiwa uwepo kuhusu kiasi na aina ya ushirikiano na msaada unaotolewa na shirika. Kiasi cha msaada huo na ushirikiano vinategemea aina na ubora wa matunzo na ulinzi uliopo chini ya mfumo wa makosa ya jinai ya nchi husika, na kiasi ambacho viwango vya kimataifa vinazingatiwa.

Uwezekano wa changamoto za ushirikiano na watekeleza sheria hauwezi kujikita pekee katika uhusiano kati ya shirika na watekeleza sheria. Miingiliano yote lazima izingatie kwa mapana masuala yanayohusisha mahusiano baina ya shirika na serikali na mashirika ya kimataifa na mashirika yasiyo ya kiserikali. Mara nyingi hatari zinazoweza kujitokeza zinaweza kuzuilika kwa kujadiliana na kushauriana kwa misingi ya ushirikiano wenye faida. Hata hivyo, ushirikiano na mamlaka za kutekeleza sheria kama unavyohalalishwa na mazingira husika, kamwe usiharibu uadilifu wa shirika lililojitolea kuwasaidia waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu. Kitu cha msingi kuondoa wasiwasi huu kipo katika usimamizi wa kitaaluma kuhusu mahusiano na vyombo vya kutekeleza sheria chini ya masharti ya pamoja ya kuzingatia haki za binadamu na falsafa ya muathirika-kwanza, kama msingi wa mwitikio wa shirika katika kushughulikia masuala ya usafirishaji haramu wa binadamu.

### 6.4 Hatari zinazoweza kujitokeza kutokana na utendaji kwa mashirika yanayotoa huduma.

Jinsi mashirika yanayotoa huduma yanavyoendelea kutoa huduma kwa waathirika, ndivyo inavyozidi kuwa ngumu kukwepa kuuhusisha kwa karibu mfumo wa makosa ya jinai wa nchi husika. Jinsi huduma zinavyozidi kuwa madhubuti katika kuwasaidia waathirika wa usafirishwaji, ndivyo thamani kubwa na umuhimu wa jukumu la shirika unavyoongezeka, na maslahi makubwa kwa polisi yanapoongezeka kutokana na ushirikiano wao wa karibu katika kuwasaidia ili waweze kuwatambua na kuwafungulia mashtaka wasafirishaji. Ushirikiano wa karibu unaleta hatari kubwa kwa waathirika na wafanyakazi. Hatari hizo zinatoka katika chanzo kinachofanana: vitisho kwa waathirika na wafanyakazi vinavyoletwa na wasafirishaji waliojipanga na wakatili. Kwa wasafirishaji, kila uokoaji na urejeshaji katika hali ya awali kwa waathirika ambao haujaadhibiwa (na wasafirishaji), aidha dhidi ya muathirika au familia yake au watu wa karibu wa muathirika, ni "biashara mbaya" kwa sababu inapunguza nguvu zao dhidi ya waathirika ambao wanaweza kuwa wanajipanga kutoroka. Zaidi ya hayo, wakati waathirika waliookolewa wanaweza kuwa mashahidi, hatari ya biashara ya usafirishaji haramu wa binadamu inazidi kuwa kubwa kwa kuwa changamoto ya uhuru wa wasafirishaji na upatikanaji wa faida inaongezeka.

Ni kweli kuwa wasafirishaji wamekuwa na visasi dhidi ya waathirika ambao wameokolewa na wametoa ushahidi dhidi yao katika kesi na wanategemewa kuendelea kufanya hivyo, kwa kuwa biashara yao inaendelea kuwa katika hatari kutokana na juhudi za pamoja za kimataifa kuiachisha. Kwa mantiki hiyo, hatari kwa wafanyakazi wa mashirika yanayotoa huduma pia itaongezeka wakati wasarifishaji wakiendelea kutambua jukumu la mashirika hayo katika mchakato wa kuwaokoa waathirika na kuwarejesha katika hali zao za awali. Uhusiano wa

karibu na polisi, hasa katika kuhakikisha waathirika wanapata taarifa na ulinzi wakiwa kama mashahidi ni lazima utaongeza kiwango cha hatari kwa wafanyakazi wa mashirika yanayotoa huduma.

### 6.5 Ushirikiano na vitengo vya kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu.

Kwa kawaida, haja ya mashirika yanayotoa msaada kushirikiana na vyombo vya kutekeleza sheria itaongezeka katika maeneo yanayohusisha shughuli zifuatazo:

- Ushirikiano wa kitaalamu au kujenga uwezo, kwa mfano, semina, mafunzo maalum au mapitio ya kisheria;
- Kubadilishana taarifa za kiintelijensia kuhusu uokoaji wa waathirika, mahojiano na waathirika au rufaa.

Ili kuhakikisha ushirikiano katika maeneo haya unasimamiwa katika hali ya usalama na njia thabiti, ni muhimu kutambua na kutengeneza njia ya mawasiliano kati ya shirika linalotoa msaada na chombo cha kutekeleza sheria. Mipango ya ushirikiano kwa vitendo iwekwe katika mkataba wa makubaliano. Inashauriwa kwamba msimamizi ateuliwe kutoka katika shirika linalotoa msaada kwa ajili ya kuwasiliana na watekeleza sheria. Mkataba ueleze wazi kwamba maafisa watekeleza sheria lazima wawasiliane na shirika linalotoa msaada kwa kupitia msimamizi wa shirika aliyeteuliwa au msaidizi. Hii itapunguza migongano inayoweza kutokea kama wafanyakazi tofauti watatoa taarifa zinazokinzana au ushauri usio sahihi au kuliingiza shirika katika kitu kisicho sahihi.

Wakati haitarajiwi kukatisha tamaa mahusiano ya kikazi kati ya wafanyakazi wote na maafisa wa kutekeleza sheria, inashauriwa kwamba mawasiliano yote kuhusu ushirikiano wa kiuendeshaji na kiutaalamu yaratibiwe na msimamizi wa shirika aliyeteuliwa. Wasimamizi wote, kutoka shirika linalotoa masaada na watekeleza sheria wafanye kazi kwa masaa ishirini na nne.

Kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu ni kazi ya masaa ishirini na nne, na uzoefu unaonesha kwamba mambo ya haraka yanayohitaji ushirikiano, hasa kuhusu uokoaji wa waathirika au msaada kwa waathirika, yanaweza kutokea katika nyakati tofauti tofauti wakati wa mchana na usiku. Utaratibu wa ushirikiano kati ya shirika linalotoa msaada na vyombo vya kutekeleza sheria utakuwa madhubuti kama una uwezo wa kutoa msaada kwa masaa ishirini na nne. Mashirika yanayotoa msaada na vyombo vya kutekeleza sheria vimteue mtu ambaye ataweza kupatikana wakati wowote, mchana au usiku na ambaye atakuwa na simu ya mkononi kwa kazi hiyo tu.

### 6.6 Ushirikiano wa kitaalamu na kujenga uwezo.

Ushirikiano na vyombo vya kutekeleza sheria kwa misingi ya ushirikiano wa kitaalamu na/ au kujenga uwezo wa taasisi kwa kawaida hautahusisha kiwango kile kile cha ugumu au unyeti kama kubadilishana taarifa za kiintelijensia au msaada wa waathirika. Kadhalika, hatari zinaweza kujitokeza wakati wa kushirikiana na chombo kinachotekeleza sheria ambacho mwitikio wake kuhusu kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu hauendani na viwango vya kimataifa. Kushiriki katika ushirikiano wa kitaalamu au miradi ya kujenga uwezo pamoja na vyombo vya kutekeleza sheria ambavyo vinafanya juhudi ndogo au havifanyi juhudi kabisa kuzingatia viwango vya kimataifa katika kuwasaidia na kuwalinda waathirika kunaweza kupelekea shirika kukosolewa. Kwa upande mwingine, ufuatiliaji mdogo au wa mara kwa mara wa ushirikiano wa vyombo vya kutekeleza sheria visivyozingatia viwango vinaweza kulipa shirika nafasi ya kuvihamasisha na kuvisaidia kujiboresha katika kuzingatia viwango vya kimataifa. Ushirikiano mdogo katika mazingira hayo unaweza kuwa njia sahihi ya kufanikisha kuboresha msaada kwa waathirika kama inavyotakiwa na kanuni za msingi.

### 6.7 Mambo ya muhimu kutambua

Jukumu la mashirika ya kutoa msaada katika kurekodi, kusimamia na kusambaza taarifa kuhusu usafirishaji haramu wa binadamu na la kushirikiana na vyombo vya kutekeleza sheria kwa ujumla, ni eneo linalosababisha wasiwasi na mjadala baina ya wataalamu wa kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu. Kwa baadhi ya watu, ugumu unahusisha uwezekano wa mashirika yanayotoa msaada kuwa mawakala wa polisi na matokeo yake kuwepo kwa utata kuhusu uadilifu wa shirika. Zaidi ya hayo, kuna wasiwasi wa kueleweka kuhusu majukumu na ujuzi wa ziada unaohitajika kutoka kwa wafanyakazi wanaoshughulikia masuala haya. Yafuatayo ni baadhi ya mambo ambayo mashirika yanaweza kuyazingatia wakati wakitengeneza sera na misimamo yao kuhusu kusambaza taarifa za kiintelijensia kuhusiana na usafirishaji haramu wa binadamu kwa vyombo vya kutekeleza sheria.

- Ulinzi, usalama na kuheshimu haki za binadamu za waathirika au wanaoweza kuwa waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu kama kanuni za kuzingatiwa na zifuatwe wakati wote;

- Ushirikiano na vyombo vya kutekeleza sheria vinaweza kulisaidia shirika kufanikisha malengo yake ya kulinda haki za wasafirishwaji na kupunguza na hatimaye kuzuia matukio ya usafirishaji haramu wa binadamu;

